# F4 TOPICAL REVISION
# KISWAHILI

***A SERIES OF TOPICAL QUESTIONS IN FORM FOUR KISWAHILI***

***FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657***

**MR ISABOKE 0705525657**

# INSHA

# 1.INSHA ZA KIUAMILIFU

1. Kumetokea mzozo wa kisiasa nchini mwako. Mmealika msuluhishi kutoka nchi jirani. Andika mahojiano baina ya msuluhishi huyo na mwanasiasa.
2. Shule yenu ilishiriki hivi majuzi katika mashindano ya riadha ya shule za Sekondari wilayani. Ulikuwa mmojawapo wa washiriki. Andika ripoti kuhusu mashindano hayo.

3. Mhariri wa gazeti la **Jicho Pevu** ametangazia wasomaji katika toleo la Jumatano kutuma makala yao ili kuchangia katika kuandika tahariri itakayohusu mabadiliko ya hali ya anga na athari zake katika toleo la Jumapili. Andika makala yako.
4. Chagua mojawapo ya mazao yafuatayo na ueleze uzalishaji wake tangu kutayarisha shamba hadi kuvunwa.
   (a) Mahindi
   (b) Nyanya

5. Ganga ganga za mganga humlaza mgonjwa na matumaini.

6. Siku yangu ya kwanza katika shule ya upili.

7. Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo:
   " … dunia kweli wakati wa sasa imefikia kilele cha maendeleo ya teknolojia."

# 2.INSHA ZA KAWAIDA

1. Andika insha itakayomalizikia kwa: Baadaye niligundua kuwa kutotii wazazi kunaweza kuwa na madhara ya muda mrefu sana.

2. Bandu bandu huisha gogo.
3. Suluhu kwa matatizo yanayoikabili nchi yetu ni katiba mpya. Jadili,
4. Kamilisha mtungo wako kwa kifungu kifuatacho.
   ………………………………………………. Ni uso wa nani usiotahayuri kwa kisa kama hiki?
5. Mchumia juani hulia kivulini.
6. Uhalifu umekithiri sana humu nchini. Jadili sababu zinazochangia hali hii na upendekeze njia za kukabiliana nao.
7. Andika insha itakayomalizikia maneno haya-----------------------niliketi nikishika tama. Iliyokuwa nyumba yangu ikawa jivu tu! Sikuyazuia machozi yalionibubujika.
8. Andika Mtungo unaothibitisha ukweli wa methali: Jitihada haiondoi kudura.
9. Simu za rununu zina madhara mengi kuliko manufaa . Jadili.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

10. Andika insha itakayoisha kwa maneno yafuatayo: .............nilipogutuka niliangaza macho huku na kule. Aah! kumbe nilikuwa nikiota!

11. Fafanua njia mbalimbali za kukabiliana na umaskini nchini mwetu.

12. Samaki mkunje angali mbichi.

13. Hauchi hauchi unakucha. Naam, siku njema niliyosubiri kwa hamu na ghamu iliwadia. Nilifurahi ghaya ya kufurahi……. (endeleza insha hii).

# UFAHAMU

1. ***<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali</u>***

Licha ya kuwa na historia ya kiasi, maisha ya binadamu ni kioja kikubwa. Hebu jiulize jinsi uhai wako wewe mwenyewe ulivyoanza sembuse unavyoweza kupumua na kuishi siku nenda siku rudi.

Dini zimefahamisha kuwa sisi binadamu tumeumbwa na Mwenyezi Muumba. Hata hivyo muumba hutumia mume na mke kutuanzishia maisha yetu humu humu duniani. Uhai wa hapa duniani huanzia katika tumbo la mwanamke muda mfupi tu baada ya mume na mke kushirikiana katika tendo la kujamiana. Katika ngono hii yenye ufanisi, mbegu moja ya manii kutoka kwa mwanamume, hudunga na kujiingiza katika yai la mwanamke huku ikilirutubisha. Tangu hapo mtu huwa na mama akawa mjamzito. Hatua ya kwanza ya uhai!

Wanasayansi wametuthibitishia kuwa mbegu katika shahawa kutoka kwa mwanamume ina kromosomu ishirini na tatu (23) nalo yai la mwanamke lina idadi iyo hiyo ya kromosomu. Basi katika hatua ya kwanza ya uhai wake, binadamu ana kromosomu arubaini na sita (46).

Kromosomu hizo zote ndizo humfanya mtu kuwa mkamilifu kwa kukadiria mambo mbalimbali adhimu. Kwa mfano, kukadiria kama kiumbe kitakuwa cha kike au cha kiume, mtu mweupe au mtu mweusi, mwerevu au wa wakia chache, mwenye nywele za singa au za kipilipili, atakuwa na damu ya namna gani, michoro ya vidole vyake itakuwa vipi na hata utu wake utakuwa wa namna gani katika siku za usoni.

Elimu yote anayopata mtu kutoka kwa jamii na mazingira huweza tu kujenga juu ya yaliyokwisha kuanzilishwa na kromosomu katika yai lililorutubishwa tumboni.

Haihalisi kabisa kufikiria kwamba huwa katika **<u>hali ya ukupe</u>**. La hasha! Yeye hujitegemea kwa vyovyote na ana upekee wake. **<u>Hatangamani na mama yake</u>**. Roho yake humdunda mwenyewe na damu yake ambayo huenda ikawa tofauti kabisa na ya mama yake, humtembea na kumpiga mishipani mwake. Isitoshe, yeye si mojawapo katika viungo vya mwili wa mama yake vinavyomdhibiti katika **<u>himaya</u>** yake ndogo.

Amini usiamini, hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa kimaumbile na mwingine na wala hatakuweko. Hata watoto pacha kutoka yai moja la mama hawawi sawa, lazima watofautiane. Si nadra kusikia mtu amepata ajali akahitaji msaada wa damu, na pakakosekana kabisa mtu hata mmoja kutoka jamaa yake wa kimwauni. Basi ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni.

**<u>Maswali-</u>**

1. Ipe taarifa uliosoma anwani mwafaka

2. Mwandishi ana maana gani anaposema '**ngono yenye ufanisi**'?



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

3. Uchunguzi wa sayansi umekita mizizi imani gani ya kidini?

4. Taja majukumu yoyote **matano** yanayotekelezwa na kromosomu

5. Katika makala, elimu kutoka kwa jamii na mazingira yaelekea kuwa bure ghali. Kwa nini?

6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala:-
   (i) huwa katika hali ya ukupe…
   (ii) himaya
   (iii) hatangamani na mama yake

2. ***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali***

Kwa zaidi ya mwongo mmoja uliopita, ulimwengu mzima uliathiriwa na masaibu ya kifua kikuu kwa kiwango cha kuogofya kiasi kwamba katika mwaka wa 1993, shirika la afya duniani (WHO) lilitangaza ugonjwa huu kuwa swala dharura la kimataifa.

Ongezeko kubwa la visa vya kifua kikuu lililotokana na kuchipuka kwa **viini** vinavyosababisha maradhi hatari ya Ukimwi na magonjwa yaliyohusiana na punde baadaye ilibainika kuwa bara la Afrika lilikuwa ndilo lililoathiriwa zaidi na Ukimwi pamoja na maradhi ya kifua kikuu. Hii ndiyo hali inayotawala sasa ulimwenguni. Afrika likiwa bara linaloongoza kwa wagonjwa walioambukizwa viini vya Ukimwi lilikuwa likishuhudia visa vya maradhi ya kifua kikuu.

Viini vya Ukimwi vinapunguza uwezo wa mwili wa mgonjwa kupigana na vijidudu vya maambukizi. Swala linalowafanya wagonjwa hawa kutodhibiti maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Katika hali ya kawaida mwili wa mtu kama huyo unaweza kujikinga dhidi ya viini kama hivyo. Maambukizi kama haya kawaida hujitokeza kukiwa na nafasi duni ya kinga mwilini. Katika baadhi ya mataifa kama vile Kenya, maambukizi ya kifua kikuu hufanyika mapema katika umri mchanga maishani.

Kwa kawaida, viini hivyo huwa havisababishi ugonjwa wenyewe. Badala yake, kinga katika mwili wa aliyeambukizwa unaweza **kusitiri** maambukizi hayo bila mhusika kuwa mgonjwa kutokana na sababu mbalimbali. Viini hivyo baadaye vinaweza kuwa hai tena na kumfanya mgonjwa kukumbwa na ugonjwa. Swala hili kwa kawaida hujitokeza wakati mgonjwa anapoambukizwa virusi vya Ukimwi. Virusi hivyo pia huongeza hatari ya ugonjwa kujitokeza baada ya maambukizi au pengine kujitokeza tena baada ya mgonjwa kupokea tiba ya kwanza.

Kulingana na utafiti, inakadiriwa kwamba mmoja kati ya wagonjwa wawili au watu wenye virusi vya Ukimwi watapata kifua kikuu wakati mmoja katika maisha yao. Inakadiriwa kwamba karibu asilimia 50 hadi 60 ya wagonjwa wenye maradhi ya kifua kikuu nchini Kenya pia wameambukizwa viini vya Ukimwi. Kwa upande mwingine, maradhi ya kifua kikuu hujitokeza kama kawaida kwa wagonjwa wenye virusi vya ukimwi. Kwa hivyo, wakati wa kushughulikia wagonjwa ni lazima pia wafanyiwe uchunguzi wa kubaini ikiwa wameambukizwa kifua kikuu.

**Maswali**

(a) Ipe taarifa uliyoisoma kichwa mwafaka
(b) Ni nini hasa kilichochangia kuongezeka sana kwa maradhi ya kifua kikuu?

(c) Kwa kifupi, eleza ni kwa nini ugonjwa wa Ukimwi ni hatari mwilini



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

(d) Ukimwi na kifua kikuu una uhusiano mkubwa, eleza uhusiano huu kulingnana na taarifa uliyoisoma

(e) Andika urefu wa neno 'Ukimwi"

(f) Eleza mambo mawili ambayo yametokana na utafiti

(g) Ni jambo lipi ambalo ni la kushangaza kuhusiana na kifua kikuu

(h) Andika maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu hiki

(i) Kusitiri

(ii)Mwongo

(iii) Swala la dharura.

(iv)Viini

3. ***Soma makala yafuatayo kisha kisha ujibu maswali:-***

Waajiri wengi wanazilaumu taasisi za elimu kwa kukosa kutoa wafanya kazi wenye ujuzi tosha, hasa wa kiteknolojia za kisasa kama kutumia kompyuta kutenda kazi mbalimbali. Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha sana.

Ujuzi wa kuweza kutumia Kompyuta unaweza kumfaa mwanafunzi hata anapokosa nafasi ya kujiunga na chuo kikuu kwa vile anaweza kuendelea na elimu yake kupitia kwa elimu mtandao. Pia anaweza kufanya utafiti wa kina kupitia intaneti na kwa njia hii akaimarisha elimu yake.

Mojawapo ya njia ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia ni kuanzishwa kwa mikakati mipya ya kufunza. Somo la Kompyuta laweza kuimarika mashuleni endapo kwanza walimu watahamasishwa juu ya faida za ujuzi huu.

Kwa kutumia Kompyuta kufunza, walimu wanaweza kufunza madarasa kadhaa katika kipindi kimoja bila kulazimika kuyahudhuria. Hii itapunguza kiwango cha kazi kwa walimu kwa vile watapata muda wa kufanya utafiti mpana. Aidha, watapata habari na ufahamu zaidi wa mambo kwa kutumia mitambo ya Kompyuta kutoka kwenye intaneti, kupitia tovuti.

Hata hivyo mipango hii inakabiliwa na changamoto kama vile bei za juu za mitambo na vifaa vya Kompyuta, ukosefu wa miundo msingi itakayowezesha utumiaji wa mitambo hii na ukosefu wa walimu waliohitimu somo la Kompyuta.

Pia, kuna tatizo la ukosefu wa nguvu za umeme hasa maeneo ya mashambani; vile vile, katika maeneo yaya haya, wanafunzi na wazazi wengi huvichukulia somo la Kompyuta kuwa gumu na linalofaa wakaazi na wanafunzi kutoka maeneo ya mijini na linalofaa wakaazi muhimu kwao mashambani.

**<u>Maswali</u>**

(a) Ipe taarifa uliyoisoma anwani inayoifaa

(b) "Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha." Ni hali gani inayozungumziwa katika aya ya 1?

(c) Ujuzi wa kutumia Kompyuta unaweza kumfaidi vipi mwanafunzi?



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(d) Mikakati mipya ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia inakabiliwa na vizingiti vipi?

(e) Taja manufaa **mawili** ambayo mwalimu anaweza kupata kutokana na ujuzi wa teknolojia ya Kompyuta

(f) Andika msamiati mwafaka zaidi kwa maneno yafuatayo:

(i) **Kompyuta**

(ii) **Intaneti**

## 4. UFAHAMU.

**Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali.**

Turipoguria nyumba mpya, tulimkuta paka. Rehema hakuingiwa na kicho maana namjua itikadi zake. Mara angesema kuwa huyo si paka ni pepo na kuwa nyumba ile halikaliki. Paka yule mara akataka kuitamalaki nyumba, kuiimgia mapana na marefu. Mimi tabia yangu simpendi paka. Kwa hakika sipendi kufuga fuga vinyama, hunitia dhiki sana nami huona navikutisha mashaka tu. Zaidi ya yote, paka hunichemuza.

Lakini tulipoingia tu akafanya mazoea na Rehema akawa kila aingiapo amwandama unyounyo naye akawa ni mzungumzi wake mkubwa. Utamsikia Rehema asema naye kama asemaye na mtu." Paka wewe u roho mno, uonacho wataka? Siku moja utakuja niangusha huishi kuniingia maguuni?"

Mimi huku nakereka. Kila nikimwambia Rehema amtupe huniambia; "leo nitamshika". Nikirudi yu papo. Hata nilipomsikia akinung'unika kuwa, "Mtu humchukuaje kiumbe akaenda akamtupa bure?", nikajua hana azma ya kumtoa mle nyumbani.

Hayo yasitoshe, kila usiku takriban alikuwa akija na genge wakatuhanikiza kwa vishindo vyao huko darini wakikimbizana na kupapurana tukawa nyumba nzima hatupati usono. ' mapenzi ya kipaka yana vituko!' Hata Rehema akawa anamwambia: "paka wewe nawe watia aibu. Huna haya hata kidogo. Uingie kwa watu, uwalie vyao, uwatilie na wanaume pia! Basi hata humstahi mwenye nyumba! Ndipo mwenyewe akawa hana jicho la kukushuhudia."



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Ilikuwa sharuti nitafute mwenyewe tadubiri ya kumtolea mbali nduli yule. Kweli alikuwa nduli kwangu; mafua yakawa hayaniishi na pia zikawa zaingia ishara za pumu. Nikafikiri nimwambie kuwa nimekwenda kutazamia nikaambiwa kuwa yule ni shetani amekuja kutudhuru kwa kujitia urafiki.

Nikaona hivi sivyo. Kuchezacheza na itikadi na hofu za mtu kwaweza kuleta hasara usiyoikadiria. Nikawaza. Ikanijia fikira kuwa paka huyu lazima ni wa watu waliokuwa wakikaa humu kabla hatujahamia sisi. Akafanya mazoea sana humu ama akaachwa papa hapa au akachukuliwa akakimbia. Nikawaambia wenyewe. Ikasadifu kuwa nilivyofikiri ndivyo ilivyokuwa. Wenyewe walikuwa washakata tamaa kuwa watampata tena paka wao.

a) Kwa nini msimulizi hakumpenda paka? (alama 4)

b) Eleza njia ambazo msimulizi alifikiri kuzitumia ili kumwondoa paka kutoka mle nyumbani. (alama 3)

c) Fafanua hatima ya kila mojawapo ya njia ulizotaja katika swali la (b) hapo juu. (alama 3)

d) "Rehema ni mtu mwenye itikadi"thibitisha kwa mujibu wa taarifa. (alama 2)

e) Ni nini kinachoonyesha kuwa rehema alimpenda paka huyo? (alama 1)

f) Eleza maana ya mafungu haya kama yalivyotumiwa taarifani. (alama 2)

(i) Hakuingiwa na kicho.

(ii) Tadibiri ya kumtolea mbali.

(iii) **5.** **<u>UFAHAMU</u>**

***<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali</u>***



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Mzawa alikuwa mziwanda miongoni mwa ndugu zake wanne.  Alipopigwa darubini, alionekana kuwa mwanagenzi ambaye falau angemakinika angefikia upeo wa ufanisi masomoni kwa kuwa na vipawa adimu vilivyofaa kuchochewa, kufukutwa, kurandiwa na kapigwa msasa. Nia ingekuwepo njia ingepatikana. Wala hakuwa peke yake. Kulikuwa na wengi kama yeye. Na kisiki kilichomkingamia kilikuwa kipi?  Kisiki kilichokuwepo kilikuwa kwamba licha ya kuwa katika kidato cha tatu na mwenye umri wa miaka yapata kumi na sita, alikuwa mfano wa ajabu ya shingo kukataa kulala chini, hakukomaa. Na mtu ataitwa mtu vipi bila kukomaa? Wenzake darasani walimwita 'toto kuu' kwa kuwa japo alionekana katutumka, tena mlingoti, alidinda kukaramka. Nao utu mzima hufunzwa katika taasisi gani? Jawabu la swali hili lingalipatikana lingalimfaa sana Mzawa.

Na usidhani wasiokomaa ni waziwando tu, hata vifunguamimba na wanuna wao wote waweza kukomaa kutegemea misukumo, ari na mazingira yaliyo karibu nao. Mtoto azaliwapo, bongo lake huwa ombwe tupu na chochote kiingiacho humo huwa kama kinachoandikwa kwa wino usiofutika, hunata kama gundi. Ukomavu huanzia hapa na mzazi akifanya waa katika maneno na vitendo afanyavyo kwa mtoto, huenda akachangia kwa kutokomaa kwake.

Mzawa hakuwa na umbu. Hii ilionyesha kuwa, kwa kuwa wazaziwe walikuwa wamejikopoa wana wanne wa jinsia moja, walimngojea mwana wa jinsia tofauti kwa hamu na ghamu. Si ajabu kuwa pindi alipozaliwa waliamua kufikisha uzazi hatima yake baada ya kupata walichokikamia. Msisimko uliowapata wazazi wa Mzawa ndio uliowapeleka kumtendekeza. Na ni kwa nini wazazi wengi huwa hawatosheki kamwe kwa kuwapata watoto wa jinsia moja tu? Si ajabu kuwaona wengine wakijifungua hata zaidi ya wana kumi, tena katika karne hii ya upangaji uzazi, lengo likiwa kusaka jinsia wasiyojaliwa kuipata. Sijui ni nani atakayeuganga ukongo huu.

Mama Mzawa  alipofunga mkaja, walisitisha shughuli zao zote, wakawa wanasherehekea  kwa vigelegele, wakikipakata kitoto chao kwa zamu zilizorembeshwa kwa mashairi ya sifa za utanashati wa mwanao kwa mahadhi mbalimbali yaliyotiwa udamisi ajabu. Msisimko kama huu lazima uwepo huwatokea wampatao mwanao wa kwanza na hasa waliolimatia kujikopoa, hivyo baba mtu akaamua hataitwa tena jongoo asiyeukwea mtungi na mama hataitwa tasa. Hili huzua hatari ya kumdekeza mwana, naye atadeka milele kama huyu Mzawa.



**FOR MARKING SCHEMES     CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Wazazi wa Mzawa hawakumkomaza. Kila kuchao walimwita ‘mtoto’, naye akawa mtoto wa kweli hata akafikia kidato cha tatu. Yasemwa kuwa Mzawa alilikamata ziwa la mamaye hata akafikia darasa la tano. Haikuwa ajabu kumpata mamake akimsubiri njiani eti waziwa yanamwasha, naye mwanawe amekishika kilembe kadamnasi ya watu huko njiani, huku amepakatwa kiweoni. Kisha akishakinai kuama, angeelekwa kwa ubeleko hadi nyumbani alikomkuta babaye aliyemngojea kwa ilhamu na kwa nyimbo za kumuongoa hadi alale.

Hadi afike hapo alipokuwa sasa, Mzawa hakujua hata kunawa uso. Daima alioshwa na mvyele wake bila hata kuona soni kwa kuwa aliamini kuwa bado ni mtoto- mfikirie mtu aliyevunja ungo akioshwa na mamaye! Izara yafaa kumkumba, ila Mzawa alinyimwa soni. Ama ndiye aliyezua maneno, “waso haya wana mji wao?” Kama walisema avuliwaye nguo huchutama, ikawaje hata Mzawa avuliwa nguo na hata kukoshwa? Jitihada za nduguze kumkebehi na kumwambia ajitegemee na zile za majirani kuwasuta wazazi wa Mzawa ziliambulia patupu.

Hii sasa ni shule ya sita aliyosomea. Mzawa tangu aingize mguu wake katika shule ya upili. Kila aingiayo haimweki. Mara atasingizia kuwakosa wazazi wake, mara atalia eti chakula ni kigumu, atasema aona baridi akilala peke yake kwa kuzoea kulala mbavuni mwa wazae wake, homa ikimpata hulia kuwa hatunzwi, mwili haogi na hata anaposhikiwa shokoa na wenzake hajui kunawa hata uso! Huyaacha matongo yakiwamulika watu. Naye hunuka fee! Mahali alalamo ungedhani ni makao ya beberu kwa mnuko. Harufu aliyotoa viatuni mwake ingesababisha pua kung’oka na mapafu kurudi. Alimradi Mzawa au “toto kuu,” kama alivyobatizwa, alikuwa zaidi ya mtoto. Na ingawa ni mapema sana huyawaza haya, je, Mzawa atakomaa, atengenee, apate ajira, apate mbawaze arukie au atakuwa kinda milele? Atapata kufu yake hatimaye?
Wako wapi hawa vifungamimba, wanuna au waziwanda waliokomaa wawakomaze wawakomaze wasiokomaa? Ama wewe usomaye wasubiri kwenda likizoni kupakatwa na wazazio? Tabia zisizoafiki umri wa mtu huongonga, na wenye hekima walitufaa waliposema, “Mtoto akinyea kiweo hakikatwi,” tutakiosha ‘kiweo’ chenyewe mtoto aadilishwe aadilike, aadibishwe aadibike.

**MASWALI**

(a) **Yape** makala haya anwani mwafaka. ( alama 1)



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

(b) **Eleza** vile wazazi wa mzawa walivyochangia katika tabia yake (alama 3)

(c) **Kwa nini** shule mbalimbali hazikuweza kumweka Mzawa? (alama 4)

(d) Kwa kuitolea mifano, **taja aina nne** ya tamathali za usemi zilizotumika katika taarifa uliyoisoma. (alama 4)

(e) **Eleza** maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala. (alama 3)

(i) Mziwanda –

(ii) Kukaramuka –

(iii) Waa-

**6. UFAHAMU**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Siku hizi kuna vitambaa vya kushonea nguo aina aina na vingine vingi vinaendelea kutengenezwa. Kuna vitambaa vya pamba, hariri, vya mnato, nailoni, sufi na vinginevyo. Kadhalika kuna mitindo na rangi za kila aina.

Kutambua kitambaa cha kushonea nguo si jambo rahisi. Uchaguzi huo ni sharti ufikiriwe kwa makini sana. Mnunuzi wa vitambaa vya nguo anapaswa kufahamu kwamba kuna vitambaa tofauti tofauti vyenye sifa tofauti tofauti. Kwa mfano, baadhi ya vitambaa hukwajuka rangi na kuwa vyeupe, vingine huchanika vinaposuguliwa, vingine hurudi vikifuliwa na vingine ni teketeke au nyong'onyevu ilhali vingine hukunjana vinapofuliwa. Baadhi havipigwi pasi, na havifuliwi kwa maji baridi, vingine hufuliwa kwa maji yenye joto kiasi.

Mnunuzi anapaswa kuzingatia sifa hizi zote pale anapochagua vitambaa vya nguo. Hata hivyo, ni vizuri kufahamu kwamba sio watu wote wanaozifahamu sifa zote muhimu za vitambaa; na wale wanaozijua baadhi za sifa hizi hawazijui zote.

Kuna njia kadhaa anazoweza kutumia mnunuzi kujulia sifa za vitambaa vya nguo. Mnunuzi, kwa mfano, anaweza kuwauliza wauzaji. Ni vizuri hata hivyo, kutahadhari na kuyapima maelezo yanayotolewa kwa uangalifu. Ingawa chini ya kifungu cha sheria cha maelezo ya kibiashara wauzaji wanapaswa kutoa



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

habari sahihi kuhusu bidhaa zao, si wote wanaosema ukweli. Hii ni kwa sababu wengine huhofia kwamba wakitoa habari sahihi huenda wakakosa wateja wa kununua bidhaa zao.

Njia nyingine ambayo kwayo mnunuzi anaweza kujulia habari za vitambaa ni kwa kuangalia maelezo yanayopatikana kwenye vibandiko au vijikaratasi vyenye maelezo. Kwa mujibu wa sheria za nchi nyingi vibandiko vya aina hiyo vinapaswa kuwa sahihi na kutoa habari zisizo sahihi ni kosa linaloweza kumfanya mtengenezaji kuadhibiwa. Maelezo yanayopatikana kwenye vibandiko hivyo ni muhimu kwa sababu hutoa maelezo muhimu kuhusu aina ya vitambaa, namna vinavyoweza kufuliwa na kama vinapaswa kupigwa pasi au la miongoni mwa mambo mengine.

Mtu anaweza kujua aina ya kitambaa pia ikiwa ana ujuzi wa kushika au " kuhisi ". Mtu anaweza kushika kitambaa kwa utaratibu na kukadiria kama kinakunjanakunjana au la. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba sio wauzaji wote ambao wanapenda vitambaa vyao vishikweshikwe kwani vikishikwa sana huishia kuwa vichafu na kukosa wanunuzi.

Baada ya uchaguzi bora wa kitambaa, uamuzi wa kama mtu fulani atanunua kitambaa kizuri au la ni bei nafuu. Ni vizuri kutafuta vitambaa vizuri na visivyo vya bei ghali. Kufanya hivyo kutamsaidia mnunuzi kutotumia pesa ambazo angetumia kufanyia mambo mengine kununulia nguo tu.

**Maswali**

a) Toa kichwa mwafaka kwa taarifa hii. ( alama 1 )

b) **Mwandishi ana maana gani anaposema:** (alama 3 )

i) Vitambaa vya aina aina

ii) Baadhi ya vitambaa hukwajuka au huchujuka rangi

iii) Vingine hurudi vikifuliwa

c) Taja njia tatu zilizotajwa na mwandishi zinazomsaidia mnunuzi kuchagua kitambaa bora (alama 6)

d) Taja aina nne ya vitambaa vilivyotajwa na mwandishi katika taarifa. ( alama 2 )

e) Je, baada ya kuchagua kitambaa unachotaka, ununuzi wa kitambaa hicho utategemea nini ? (alama 3 )

## 7. UFAHAMU (ALAMA 15)



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

***Soma tarifa hii kisha ujibu maswali.***

Asifuye mvua imemnyea. Huu ni msemo wenye hakika isiopingika, na kutilia shaka ni sawa na kudai jua linaweza kubadilika na kuchomozea upande magharibi badala ya mashariki.Huu ndio ukweli uliodhihirika juzi katika vyombo vyetu vya magazeti.

Lisemwalo lipo, na kama halipo li njiani.Waama, pafukapo moshi pana moto. Mwanafunzi mmoja wa kike kwa jina P.N. katika chuo kikuu kimojawapo nchini alishangaza umma wa Kenya na ulimwengu kwa jumla alipodai kuwaambukiza wanafunzi wenzake wa kiume mia moja na ishirini na wanne virusi vya ukimwi.

Kisa na maana? Aliambukizwa ukimwi na mwanafunzi mwenzake aliyekuwa akifanya majaribio ya ualimu katika shule yao ya upili. Baada ya kushawishika sana alijuana naye kimwili, na matokeo yakawa kifo ambacho sasa alikuwa anawagawia wenzake.

Kisa kama hiki kinachangia kueleza kina kirefu cha kutamauka na upweke ambao maisha ya waja wengi yameingia kiasi cha kuwaacha wanyama ijapo wanaenda kwa miguu miwili bado. Katika mojawapo ya mafunzo ya kidini ambayo padre alinifunza mimi na wanafunzi wenzangu, tuliambiwa kisasi ni chake Mola, sisi waja wetu ni kushukuru tu. .Mbona basi mwanafunzi kama huyu kutaka kulipiza?

Ima fa ima, na waswahili husema, “mlaumu nunda na kuku pia”.Huyu mwanafunzi hawezi kuachiwa atende alivyotenda. Aliyekula naye raha alikuwa mtu aliyefahamika vizuri sana kwake. Isitoshe, huenda wakati huo alikosana na mama na baba kulala nje. Huenda alikosana na ndugu zake kwa kuepa nyumbani usiku wa manane kwenda kumwona huyu kalameni. Huenda alikosana na mwalimu wake kwa sababu kiburi kilianza kuingia. Kwa vyovyote vile, alikula raha na hastahili kuwaadhibu watu wasio na hatia kufidia makosa yake. Je, kama yeye na huyo jamaa wasingekuwa na ukimwi, raha kiasi gani wangezila hadi leo?

Jamii na watu wote kwa jumla hawana budi basi kulaani vitendo vya P.N. vya kuambukiza wanafunzi wenzake virusi huku akijua. Hili kosa ambalo linastahili adhabu ya kifo. Dawa ya moto ni moto ni adhabu inastahili kuchukuliwa haraka ili P.N. ambaye tayari amekiri hatia, atiwe nguvuni na adhabu itolewe.

Barua ya PN inafafanua jambo jingine sugu. Kwamba kiwango cha maadili katika vyuo vyetu kimezorota kiasi cha kufanyiana unyama usiosemeka.Vijana wengi siku hizi wanashiriki tendo la ndoa bila haya. Huu upotofu wa maadili katika jamii wapaswa kushutumiwa na wote. P..N. hana sababu yoyote ya kibinadamu, kidini au kitu chochote kile kudai haki kwa uovu huo wake.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

## Maswali

1. **Taja** kichwa mwafaka kwa makala haya. (alama 2)
2. Katika aya mbili za kwanza, mwandishi anamlaumu mwanafunzi kwa kosa gani? (alama 2)
3. **Eleza** chanzo cha tabia za P.N. (alama 2)
4. Mwandishi wa taarifa hii anataka P.N. achukuliwe hatua gani? Kwa nini? (alama 4)
5. Barua ya P.N. bila shaka imeonyesha uvumbuzi mpya. **Utaje** (alama 2)
6. **Eleza** maana ya vifungu hivi kama vilivyotumiwa katika taarifa: (alama 3)
   (a) Kina kirefu cha kutamauka
   (b) Ima fa ima

Kufudia makosa yake

## 8.UFAHAMU ( ALAMA 15)

**Soma makala yafutayo kisha ujibu maswali**

Limeibuka suala kwamba polisi waliokuwa wakiongoza mashtaka mahakamani sasa watakuwa chini ya himaya ya mkuu wa sheria wala si kamishina wa polisi. Ni hatua iliyo na mashiko katika utekelezaji na usimamizi wa sheria.

Hatua hiyo itasaidia kuhakikisha kwamba washtakiwa watapata haki kamili na kuzuia visa ambapo polisi wakati mwingine walikuwa wakiwasingizia washtakiwa madai ya uongo na kisha kuwatolea mashtaka.

Polisi hawapaswi kutekeleza majukumu fulani katika maongozi ya sheria kwa kuruhusiwa kuwatia nguvuni washtakiwa, kuwatayarishia mashtaka na halafu kuwafikisha mahakamani.

Maofisa husika sharti wafunzwe upya kuongoza mashtaka kuambatana na sheria, wala si kanuni za polisi wanaoongoza mashtaka, wawe mawakili waliosomea wanasheria ipasavyo sawa na mawakili hao wengine. Hali hii itazuia visa ambapo wakili huwa anafahamu sheria kuliko kiongozi wa mashtaka.

Mawakili zaidi wa umma wafaa kutengewa washtakiwa wasio na pesa za kuwalipa mawakili wa kibinafsi kuwatetea.

Hatua hizo zitaharakisha kesi zirundikanazo mahakamani na pia kupunguza idadi ya washtakiwa wanaowekwa rumande kutokana na hitilafu za kisheria.

**Maswali**

a) Yape makala anwani mwafaka Alama 1

b) Utekelezaji wa sheria mahakamani umetiwa sura mpya . Fafanua kwa mujibu wa makala. Alama 2

c) Dhihirisha kuwa washtakiwa nchini Kenya wamekuwa wakikosa haki. Alama 2

d) Shughuli za mahakama na utekelezaji sheria zahitaji kuboreshwa. Eleza. Alama 3

e) (i) Orodhesha majukumu ambayo polisi hawafai kuyatekeleza kisheria. Alama 3

(ii) Eleza sababu muhimu inayowakataza polisi kutekeleza majukumu uliyoyaorodhesha katika sehemu ya e (i) Alama 1

f) Eleza maana :- Alama 3

i) Kuwatia nguvuni
ii) himaya
iii) rumande



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

**9.UFAHAMU ( ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho halafu ujibu maswali uliyoulizwa**

Tsunami, tetemeko la ardhi baharini, iliyotokea Desemba mwaka 2004 katika bara la Asia ilikuwa na athari kubwa sana. Watu wasiopungua 170,000 walipoteza maisha yao kutokana na mawimbi yaliyotufulia na tsunami hiyo katika Bahari ya Hindi. Madhara na maafa hayo yalitanda hadi maeneo ya mbali kama upwa wa Afrika Mashariki ulio na umbali wa takribani kilometa 7,000 kutoka kitovu kikuu cha tsunami hiyo. Janga hili limeibua mjadala kuhusu madhara yanayotokana na nguvu za kimaumbile. Nguvu za kimaumbile zina uwezo wa kuzua majanga yasiyoweza kutarajiwa. Mlima wa volkeno uliotulia unaweza kuvuvumka na kutapakaza zaha ambayo inaweza kuua maelfu ya watu kama ilivyotokea huko nchini Kongo.

Majanga ya kimaumbile huweza kusababisha maafa, misiba na tanzia isiyokuwa na mshabaha. Sio rahisi kuweza kutasawari akilini kiwango cha madhara ya majanga haya hadi yanapotokea. Baadhi ya majanga ya kimaumbile ni kama vimbunga vya vumbi, zilizala, mafuriko, tufani, radi, ukame na hata moto.

Licha ya kuwa binadamu hawana uwezo wa kuzuia kutokea kwake, zipo hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa. Kwa mfano, yapo maeneo ambako kutokana na historia ni rahisi kujua ni majanga yepi ambayo huweza kutokea. Kuna maeneo ambako mafuriko hutokea kila zinaponyesha mvua za mvo. Jamii inayojikuta katika mazingira hayo inapaswa kujua ni hatua zipi za kuchukua. Mathalan ujenzi wa matuta, kuhimiza wakazi kusakini katika maeneo ya juu, kuwepo na huduma za dharura za kupambana na maradhi yanayochimbukana na ungi wa maji na kadhalika. Vivyo hivyo na ukame. Ni muhali kuweza kujua ukame utatokea lini. Hata hivyo, jamii inaweza kuchukua hatua fulani ambazo zinachangia kwenye ukame kamaukataji holela wa miti. Uchimbaji wa chemchemi ni njia nyingine inayoweza kutumiwa hasa kuhakikisha kuwa taraa ukame utazuka, watu hawataathirika kutokana na kuyakosa maji ya kutumia.

Wataalamu wameafikiana sasa kuwa baada ya tsunami iliyotokea lazima uwepo mfumo madhubuti wa kuweza kuudodosa mtikisiko wa ardhi ambao hutokea kwa muda kabla ya tetemeko lenyewe. Kwa njia hii watu wataweza kuonywa mapema na labda hasara kama iliyotokea kupunguzwa.

**Maswali**

(a) Toa kichwa mwafaka kwa makala haya. (Alama 2)

(b) Ni nini maana ya tsunami? (Alama 2)



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

(c ) Ni lipi lililokuwa tokeo kuu la tsunami? (Alama 2)

(d) Eleza hatua zozote nne anazoweza kuzichukua binadamu kupambana na majanga ya kimaumbile.

(Alama 4)

(e) Taja methali inayoweza kuufumbata ujumbe wa kifungu hiki. (Alama 2)

(f) **Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu hiki.**(Alama3)

(a) Kuvuvumka

(b) Kutasawari akilini

(c) Mvua za mvo

# 10.UFAHAMU

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.***

Teknolojia mpya ni tawi la maarifa linalohusiana na sayansi kwa upande mmoja na uhandisi (uinjinia) kwa upande mwingine. Sayansi ni elimu inayotokana na uchunguzi na majaribio katika maabara nao uhandisi ni ujuzi wa kuunda mitambo. Maarifa ya sayansi yanapotumiwa kutengeneza vitu viwandani, hali hii inakuwa teknolojia.

Zao mojawapo la teknolojia mpya ni simu tamba. Watu vijijini sasa wanawasiliana na jamaa zao walio mbali. Akina nyanya wanapopanda njugu, kupalilia migomba, kukama ngamia au kukuna nazi, wanaweza kuzunguuza na wajukuu zao walio uingereza, uchina au kwingine kule.

Hakuna mahali ambapo hapajajafikwa na teknolojia mpya. Tukitembelea baadhi ya nyumba tutaona vifaaa kama vile tanuri la miale au mikrowevu ambalo linapika maharagwe yakaiva kwa dakika chache tu. Majokofu nayo yanatusaidia kuhifadhi vyakula bila kuharibika. Hata maiti na mizoga inaweza kuhifadhiwa kwa miaka mingi kwa ajili ya utafiti bila kuoza katika ufuo au mochari.

Kwa upande wa kilimo, teknolojia imefanya makubwa. La kustaajabisha ni mtu mmoja kulima eneo kubwa la shamba kwa trekta halafu akapanda kwa tandazi, akanyunyizia dawa kukausha magugu, akavuna na kukoboa mahindi akiwaa peke yake. Siku hizi inawezekana kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu kwa sababu ya teknologia mpya.

Teknolojia hii imewezesha watu kuvumbua aina nyingi za nishati. Badala ya kutegemea umeme unaotokana na maji tu, sasa watu wanatumia mvuke, nguvu za upepo na nishati ya



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

jua kupata umeme. Kwa sababu hii, hata mababu zetu vijijini wanatazama televisheni bila shida wala wahka.

Kwa upande mwingine, teknolojia ina madhara yake. Kwa mfano, uundaji wa silaha kali unaendelea kuwaangamiza watu wengi. Mabomu ya kitonoradi yaliyoangushwa Hiroshima na Nagasaki Japan mwaka 1945 ni zao la kisayansi. Haya yaliwaua watu wengi na madhara yake bado yanadhihirika hata leo katika maumbile ya watoto wanaozaliwa na upungufu. Tena magaidi na wahalifu wa kimataifa wanatumia teknolojia mpya kuimarisha mbinu zao za kutenda maovu. Isitoshe, inawezekana kutumia teknolojia kuagizia benki kutuma pesa nje ya nchi ya bila mwenye hazina kujua.

Wahalifu wanaweza kusikiza mawasiliano ya watu kwa simu hata ikiwa ni baina ya polisi. Kisha matatizo mengi ya kiafya yasemekana yanatokana na vyakula vilivyokuzwa kutumia teknolojia mpya.

Katika usafiri, kuna gari moshi lenye kutumia stima badala ya makaa. Hili ni zao la teknolojia mpya vile vile. Ingawa mwendo wake ni wa kasi, kasi hiyo na stima huweza kusababisha ajali mbaya mno.

Ingawa madhara yapo lakini manufaa ya teknolojia ni mengi zaidi kuliko madhara yenyewe. Faida ni kuwa teknolojia hurahisisha shughuli za watu kama vile kufua na kusafiri. Pia hufanya matokeo ya shughuli kuwa bora zaidi. Kazi iliyopigwa chapa kwa kompyuta huwa safi na bora. Vile vile, vitu vinavyotengenezwa siku hizi ni vidogo na vyepesi lakini bora zaidi. Tukichukua mfano wa magari tunaona kuwa ni madogo lakini yenye muundo wa kuvutia. Tatizo tu ni ile kasi kubwa ambayo ni moja ya mambo yanayosababisha ajali nyingi.

Gharama ya vitu vinavyotengenezwa kutumia teknolojia mpya ni nafuu. Teknolojia hii inatumia malighafi ya kisasa na hivyo kuhifadhi madini yetu. Pia huunda vitu ambavyo matumizi yake yanadhuru mazingira.

Tusisahau kuwa hata hapa kwetu matekinia wa ‘jua kali’ wanapiga hatua. Wanajitahidi usiku na mchana kuunda vitu vya kutuuzia kwa gharama nafuu. Mitambo ya kusukuma maji sasa inapatikana. Vyombo vya kusafirisha mizigo, vifaa vya kunyunyizia maji, tanuri ya kuoka inayohifadhi nishati na vingine vingi, sasa vinaundwa ili kuimarisha sekta hii. Ikiimarika, Kenya inaweza kuwa nchi yenye uwezo wa viwanda.

**Maswali**

**Eleza** umuhimu wa teknolojia mpya kwa zaraa (alama 2)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

"Kwa hakika uhandisi umepiga hatua." **Thibitisha** kauli hii kulingana na taarifa. (alama 2)

**Unga mkono** kauli kwamba hakuna mahali ambapo hapajafikiwa na teknolojia. (alama 2)

Uvumbuzi wa teknolojia **umeisaidiaje** ulimwengu kupunguza gharama ya uzalishaji wa bidhaa? (alama 3)

**Taja** athari zozote mbili za kughasi za uvumbuzi. (alama 2)

**Eleza** jinsi uvumbuzi umeibuka na anasa ya kipekee. (alama 2)

**Eleza** maana za maneno haya jinsi yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 2)

Malighafi

Matekinia

## 11.UFAHAMU

Bi mwenyekiti , wataalamu wa lugha, waamuzi na washiriki waliojumuika kwenye mdahalo, mabibi na mabwana. Si vema niwapotezee wakati wenu kutetea mjadala kwa madhumuni ya kuteta tu. Sijaja hapa kupiga makelele mithili ya mbwa mdomo wazi (makofi). Nimefika hapa kuwaandalia hoja madhubuti zitokanazo na kina cha mawazo na maoni murua moyoni mwangu. Mada ya mjadala inasema kuwa Kiswahili inatosheleza matakwa yote kimawasiliano.

Bi mwenyekiti, Swali tunalopaswa kujiulizwa ni, Je, mawasiliano ni nini? Fafanuzi mbalimali zimetolewa. Aidha wavumbuzi wa kisayansi / kiteknolojia wameasisi mbinu za kisasa zinazorahihisha mawasiliano na kuufanya ulimwengu kuwa kama kijiji. Tukijikita kwenye muktadha wa mjadala huu, twaweza tukaafiki kwamba mawasiliano ni kupasha ujumbe namna unavyoeleweka na mpokezi. Hivyo ni kusema kwamba mja aweza akatumia lugha, ishara au alama kumfikishia mwenzake ujumbe uliokusudiwa. Pindi mpokezi akosapo ufahamu wa jambo linaloangaziwa, basi hapo mawasiliano yatakuwa <u>muhali.</u>

Mawasiliano huwezesha makabila mbalimbali kutangamana huku yakiendeleza biashara. Maazimio na miradi ya taifa yaweza kusambazwa kotekote kwa Kiswahili kupitia radio, magazeti na runinga. Huu ni ukweli wa wazi usiopingika. Kiswahili bila shaka, chajitosheleza kimawasiliano.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Bi mwenyekiti, niliyoyadokeza yana ithibati. Naomba kutajiwa muktadha wowote, si nyumbani, si ofisini, si kanisani ambamo mawasiliano kwa Kiswahili yangekwama. Duru za kuaminika zashikilia kuwa mtaalamu wa tarakilishi ulimwenguni, Bill Gates, ameunda mitambo itumiayo misamiati na lugha ya Kiswahili. Ajabu!

Bi mwenyekiti, hawa wapinzani wana upungufu mmoja, nao ni yamkini hawajimudu katika lugha ya Kiswahili. Wanatumia upungufu wao huo dhidi ya mjadala unaojitetea wenyewe. Mmoja wa wanenaji amejikanganya na kujipinga kwa kusema, "mwacha mila ni mtumwa." Kauli hii inazidi kuthibitisha kuwa Kiswahili kina ukwasi wa kutosheleza mawasiliano. Wapinzani wangekuwa weledi wa Kiswahili wangegundua kuwa usemi huu unaafikiana na mjadala (makofi). Ama kwa kweli fumbo mfumbie mjinga, mwerevu atalifumbua! Aidha uneni usisitizao kuwa "Alalaye usimwamshe, ukimwamsha utalala wewe" unao mashiko. Bi mwenyekiti, tamati nimefika nikiwasihi wenzangu wasisite kuvuka sakafu ili tuufanikishe mjadala. Asanteni.

a) Upande wa upinzani ulishikilia mada ipi? (alama 1)

b) Msemaji wa upinzani amejikanganya anapotumia msemo: "Mwacha mila ni mtumwa ." Fafanua. (alama 2)

c) Mwandishi anasema, "Alalaye usimwamshe ukimwamsha utalala wewe." Thibitisha ukirejelea muktadha wa hotuba uliyoisoma. (alama 4)

d) Kunapatikana shangwe (makofi) zaidi ya mara moja katika taarifa. Eleza chanzo cha shangwe hizo. (alama 2)

e) Mbali na mbinu za mawasiliano zilizozungumziwa katika taarifa, zitaje mbinu nyingine za kisasa ambazo zimerahisesha mawasilano. (alama3)

f) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya msamiati huu:

Yamkini--------------------------------------------------------------------------------

Ithibati--------------------------------------------------------------------------------

Muhali--------------------------------------------------------------------------------

**12.UFAHAMU:**
**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali:**

Mwangeka Mwachoni alizaliwa mwaka wa 1930 katika tarafa ya Mwanda, Wilaya ya Taita-Taveta. Angalikuwa hai leo bila shaka angalikuwa mmoja wa watu mashuhuri wenye kuheshimiwa kwa ujasiri wao.

Mwangeka alipata taabu mno utotoni wake kwa sababu ya malezi ya shida ya wazazi wake ambao walishindwa hata kumpeleka shule. Juu ya hivyo aliweza kuinuka na kuwa kijana mahiri sana tena mkakamavu na mchanga-mfu. Alikuwa akiwatii wazazi wake na kuwaenzi. Alijitwika jukumu la



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

kuiangalia ile milki yao ndogo waliyokuwa nayo na kuwatumikia bila kinyongo. Ustadi aliokuwa nao Mwangeka umeweka kumbukumbu ya vitendo vya ushujaa wake wakati angali ni mdogo. Wakati huo, kila siku alikuwa akichunga ng'ombe wa baba yake milimani kulikokuwa na hatari za kila namna za wanyama wa mwitu. Siku moja alipowapeleka ng'ombe wao malishoni aliwaona simba wawili katika mlima Vuma waliotaka kuwashambulia wale ng'ombe. Mwangeka alipambana nao kwa uta na mshale na akaweza kuwaua. Hapo ndipo sifa zake za ujasiri ziliposambaa Taita nzima.

Mwangeka alikuwa mtu mwenye hekima na busara nyingi na alikuwa mwenye maarifa ya mambo mengi ya ajabu. Mojawapo ya mambo aliyoyajua ni vipi kajipinga na kujihami na shari za maadni wasiweze kumwona au kumjua alipo na hali yeye amewakabili na kuwatazama. Basi alipofika umri wa miaka ishirini na tano alianza kuwa mashuhuri na sifa zake zilizagaa kila mahali. Wakati huo alikuwa amekwisha oa. Alimwoa mwanamke aitwaye Magema, bibi ambaye mwanzo wa kuolewa alionyesha hubo nyingi kwa mumewe. Lakini baada ya miaka michache alianza kubadilika <u>hulka</u> na kuwa na umbeya na udadisi mwingi. Kila mara alikuwa akimsaili mumewe kuhusu ushujaa wake na mengi mengine yasiyostahili kuulizwa, bali mradi aelezwe tu. Alikuwa akistaajabu kumwona mumewe akiweza kuishi msituni kwa muda wa mwezi mzima bila chakula, na vile alivyoweza kwenda kwa miguu kutoka Kasigau mpaka Mwanda, mwendo wa kilomita mia mbili, bila kuchoka. Pia, ilikuwa ikistaajabisha vile alivyoweza kupotea asionekane na maadui zake (ambao wakati huo walikuwa ni wazungu) akiwacha nyuma kivuli chake ambacho ndicho kikiwashambulia na kuwaua maadui hao.

Siku moja bibi alimbembeleza sana mumewe amweleze maarifa na miujiza atumiayo, lakini Mwangeka alikataa kabisa kumdokezea habari hiyo. Mwishowe kero lilizidi na Mwangeka hakuweza tena kumkatalia.

Aliona heri amweleze lakini alimkanya asiweze zabizabina na kumweleza mtu yeyote, kwani hiyo ilikuwa siri yake. Akitoa siri hiyo kumwambia mtu, maisha yake yatakuwa hatarini, <u>mahasimu</u> zake wakikipiga kivuli chake.

Mwangeka alifanya kazi kubwa katika kuupigania uhuru wa Kenya. Aliwafukuza wazungu na kuwaua wengi. Huu ndio wakati ambapo Taita, na Kenya kwa jumla, ilipomtambua Mwangeka kuwa ni kiongozi asiye na kicho, aliyejitolea maisha yake yote kwa ajili ya nchi yake. Yeye ndiye aliyekianzisha chama cha vijana wa kitaita kilichopigania usawa wa wataita. Alitembelea sehemu nyingi za Kenya na akakutana na Jemadari Dedan Kimathi, mmoja wa viongozi wa Mau Mau, wapiganaji wa vita vya uhuru. Viongozi hao wawili walizungumza na kushauriana namna ya kupambana na taabu zilizo wakabili na wakaahidiana kwamba watakuwa wakitembeleana mara kwa mara.

Huku nyuma nyumbani kwa Mwangeka mambo hayakuwa mema kama alivyofikiria. Baada ya yeye kuondoka wazungu wawili walifika na kumbembeleza mkewe awaeleze jinsi Mwangeka alivyokuwa akifanya. Kwanza mkewe alikataa kuwaeleza lakini baada ya kupewa gunia moja la mchele na shilingi kumi pamoja na kuahidiwa mambo mema kadha siku za mbele, aliwaeleza siri zake zote!

Ilikuwa usiku, tarehe 23 Machi 1966, Mwangeka alipoonekana amelala juu ya jabali kubwa, maiti, kiwiliwili chake kiasi cha maili tatu hivi kutoka kivuli chake.

(a) Kisa gani kilimfanya Mwangeka kusifiwa kwa ujasiri katika Taita? (alama 2)
(b) Eleza sifa moja ya ajabu ya Mwangeka ambayo ilikuwa ikiwakanganya maadui zake. (alama 2)
(c) Eleza mabadiliko ya tabia ya mke wa Mwangeka. (alama 3)
(d) Eleza sifa za Mwangeka zisizopungua tano. (alama 3)
(e) Wale wazungu wawili walifanya nini hata Mwangeka mwishowe akauawa?(alama 2)
(f) Mwangeka alipokufa alikuwa kijana au mzee? Toa sababu. (alama 2)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa namna yalivyotumika katika taarifa.(alama 6)
    (i) Mahiri: ______________________________________________________



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) Bila kinyongo: ________________________________________________
(iii)Hulka: _______________________________________________________
(iv) Mahasimu: ____________________________________________________
(v) Akijitwika jukumu: _____________________________________________
(vi) Akimsaili: _____________________________________________________

**13.** ***Soma kifungu kifuatcho kisha ujibu maswali.***

Takwimu ambazo zimetolewa na shirika la kazi la kimataifa (ILO) zinaonyesha kuwa ulanguzi wa watoto umetangaa hususan katika mataifa yanayoendelea. Ipo tumbi ya sababu za kuelezea kwa nini biashara hii imeshamiri.

Athari mojawapo ya utandawazi ni kuunda mtandao mpana ulimwenguni. Mtamdao huo unaweza kutumiwa kwa njia chanya au njia hasi. Njia chanya ni zile zinazokiliwa kuwafaidi wanajamii kwa kuendeleza ubinadamu na kuboresha hali ya maisha kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Maarifa yanayosambazwa huweza kuwa chachu ya kuumua ari ya maendeleo, elimu na mafanikio katika mataifa mengi ulirnwenguni. Njia hasi ni zile ambazo maarubu yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi.

Kuwepo kwa mtandao kunawapa wenye nia tule kama usafirishaji na ulanguzi wa watoto fursa ya kuzitosheleza hawaa zao. Wanaoshiriki katika biashara hii huongozwa na pashau ya utajiri. Hawachelei kuwalangua watoto wanaochimbukia mataifa ya kimaskini huko ughaibuni wanakozongomezwa kwenye madanguro kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi na kuishi maisha duni.

Asilimia kubwa ya watoto hurubuniwa kwa ahadi ghushi za kujiendeleza kimasomo. Wengine huuzwa kutokana na msaada wa jamaa zao wanaotovukwa na utu na kuwa mawakala katika amali hii ya kusikitisha. Biashara hii huweza kusahilishwa kwa kuwepo kwa mfumo fisadi wa kisheria, msambaratiko wa muundo wa jamaa na ubinafsi wa kijamii.

Ipo haja kubwa ya ushirikiano wa mataifa alkulihali kuikomesha biashara hii haramu. Jamii ya ulimwengu isipofanya hivi, itakuwa imekitia kizazi kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri. "

**Maswali**

a) Ni kwajinsi gani utandawazi umechangia katika biashara ya ulanguzi wa watoto?

(alama 2)

b) Mwandishi wa kifungu anapendekeza hatua zipi kusuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto?

c) Elezajinsi watoto wanaolanguliwa wanavyoishi huko ughaibuni. (alama 3)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

d) Kulingana na muktadha, kifungu "chachu ya kuumua ari ya maendeleo" kina maana gani? (alama 2)

e) Jamii isiyosuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto itakuwa na hatima gani? (alama 3)

f) Eleza maana ya

i) maarubu ii) pashau

(alama 2)

14.

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Kuna aina kuu za hisia zinazotawala na kuongoza maisha ya mwanadamu: kuona,kusikia, kugusa, kuonja na kunusa. Ni vigumu kusema ni hisia gani muhimu kuzidi nyingine ingawa ni dhahiri athari kubwa humuangukia mahuluku asiyeweza kuona. Inasemekana kuwa mishipa ya fahamu inayounga ubongo na viwambo vya masikio. Na katika maisha na nyendo za kila siku kuona hupewa uzito mkubwa **mighairi ya kusikia**. Pengine bad sio ajabu, kama itakavyobainika punde baadaye, kuwa kazi nyingi za fasihi andishi zimeelemea mno katika hisia hii kana kwamba zile nyingine kuu hazipo kabisa. Hakika hili ni kosa. Maana kusikia, kugusa, kuonja na kunusa nako ndiko humkamilisha mwanadamu aweze kuyafaidi maisha yake. Na hata mbele ya sheria, ushahidi huweza kutolewa mintaarafu ya kusikia, kugusa kuonja na kunusa alimradi shahidi awe amesikia,kugusa, kuonja, au kunusa mwenyewe. Ushahidi wa kuambiwa haukubaliwi.

Kwa hiyyo basi kazi ya sanaa ambayo itazituma fikira za msomaji zihisi kuona, kusikj a, kuonj a, kugusa, na kunusa matendio na mazingira yanayosimuliwa humpeleka msomaj i huyo katika rnipaka na nyanj a za j uu za ufahamu na furaha.

Kila hisia ina umuhimu wake kutokana na mazingira ya tukio linalohusika au kusimuliwa. Maana kazi zote za sanaa hutokana na matendo na rnaisha ya watu ambao katika matukio, visa na mazingira yao hutumia hisia zao zote tano ama kwa pamoja au kwa nyakati mbalimbali. Ili basi msomaji aweze kupata mandhari kamili, na hata yeye mwenyewe ashiriki katika matukio yenyewe kwa kuchukia, kuonea huruma, n.k., muhimu, kabla ya yote, apate hisia zote hizo tano. Kazi ya sanaa inayojihusisha na hisia mojatu au mbili huwa **muflisi kisanii** kwa vile inashindwa kuwasilisha mandhari za hali ha|lisi kwa msomaji. Je, mara ngapi nyoyo zetu husononeka au kuripukwa kwa rnaya kwa sababu ya sauti ndogo tu ya ndege aliaye pekee nyikani, au nyimbo ya zamani? Sauti ya ndege huweza kuleta majonzi ya miaka mingi mno ya utotoni wakati ambapo mtu alifiwa na *mzazi*, ndugu, j amaa, au sahibu wake. Kadhalika nyimbo ya kale huweza kuchimbua ashiki ya



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

zamani baina ya wapenzi, au kutonesha **jeraha la masaibu** na madhila yaliyopita. Na wala sio nyimbo na sauti ya ndege tu, pengine hata harufii ya maua huwa na nguvu za kumbukumbu kubwa mno.

Licha ya yote hayo, iriatumizi ya hisia nyingi yanazidia kujenga mandhari kamili ya tukio katika akili ya msomaji. Mathalan badala ya kuelezwa tu kuwa paliandaliwa chakula kizuri, msomaji anaelezwa vitu ambavyo vimeandaliwa pamoja na harufu yake. Au badala ya kuambiwa mtu fulani alikuwa na wajihi wa kutisha, huelezwa na kuelewa vyema zaidi kwa kuainishia jinsi pua, macho, rangi, nywele, mdomo na meno ya mtu huyo yalivyo. Na hivyo hivyo kwa mifano mingine kadha wa kadha kama vile hasira na ucheshi. Kutokana na maelezo ya kutosha ya hisia msomaji huweza **kuinuashiki janabi**, au akadondokwa na ute kutamani chakula ambacho hakipo mbele yake.

Na sio hivyo tu. Hisia zinazotumiwa huweza kumfanya msomaji atafakari zaidi. Ataweza kufikia uamuzi kuhusu picha zinazochorwa kutokana na hisia mbalimbali na wala sio kauli za mkatomkato za mwandishi kama ilivyogusiwa hapo juu. Kauli za mkatomkato sio tu hudumaza sanaa, bali pia hudhalilisha hata akili ya msomaji: kwani **umbuji** wa mwandishi ni pamoja na kufanya matendo na mazingira anayoyasimulia yawasilishe na kuwakilisha fikira za wahusika wake na hata zake mwenyewe.

Hivyo ni dhahiri kuwa hisia humsaidia msomaj i kuzama katika matendo na kuelewa fikra za mwandishi mwenyewe, asilinamakazi yake, kuwadadisinakuwaelewa wahusika wenyewe,n.k.

**Maswali**

a) Taja na ueleze uwanja ambao hutilia mkazo hisia zote

(alama3)

b) Kwa mujibu wa kifungu hiki,ni nini matokeo ya kusisitiza hisia ya kuona katika fasihi andishi?

(alama2)

c) i) Mwandishi ana maonigani kuhusu kazi nzuriya sanaa. (alamal) ii) Maoni hayo yana umuhimu gani? (alama4)

d) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu ulichosoma

i) muflisi kisanii......................................................................................



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

ii) jereha la masaibu...............................................................................

iii) kumuashiki janabi...........................................................................

iv) umbuji...................................................................................  (alama 4)

# UFUPISHO

**1.** ***Soma taarifa kisha fupisha kwa mujibu wa maswali yafuatayo.***

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kutoka kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza ubongo hunasa jambo kisha huliihifadhi. Baadaye huanzisha mfumo wa kutoa kilicho hifadhiwa. Ubongo ukiathirika kwa namna yeyote katika moja wapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitajika mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini), bidhaaa za soya, matunda, maziwa, ,bidhaa za ngano, samaki, pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madina haya ni mboga za kijani, mawele, ndengu, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja na nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini. Kwa hivyo, vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu  na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisicho hatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kumvuruga kiakili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na pia namna ya kukitoa.

Halikadhalika, mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa na mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na taratibu ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya hayo, mazoezi ya kiakili, kama vile kusoma makala



FOR MARKING SCHEMES    CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo, vitenzi ndimi ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo kuyakumbuka mambo ni ya jamii iliyopiga hatua kimaendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

**Maswali:**

a) Kwa maneno 60 – 65 fupisha mchango wa chakula katika uimarishaji wa uwezo wa kukumbuka.

b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 80 – 90

2. ***Soma taarifa kisha fupisha kwa mujibu wa maswali yafuatayo.***

Faragha ni muhimu kwa binadamu kwani huwa ndio wakati ambapo mtu atakuwa akitulia pekee mahali na huku akijiuliza ni mema mangapi ameyatenda siku hiyo, maovu mangapi ameyafanya, na kama siku hiyo ilikuwa ya manufaa au la.

Si binadamu wote ambalo wanapendelea kutumia wakati wao wa faragha kwa kupiga domo, nyumbani, kustawisha mabustani yao ya maua au mimea, au hata kuchukua kitabu au magazeti ya kusoma na kujifunza. Watu kama hawa huwa na fikira na mawazo mbalimbali juu ya umuhimu wa thamani ya wakati wa faragha. Watu kama hao utawakuta wakikusanyika katika makundi kwa matarajio ya kujinufaisha kwa mapato fulani au kujiingiza katika upigaji wa kamari. Wengine hunufaika wakasifu mafanikio yao ya siku ya mkusanyiko na baadhi yao ambapo hufanya mhanga wa michezo hii huibuka huku wakilaani na kuapiza bahati zao mbaya.

Kuna kundi jingine ambao hustahabu vilabu vya usiku kwa kujiliwaza au kujitumbuiza ili wapate kujituliza mawazo yao, wakayatafuta makali na kileo. Mwanzo wa ushirika kama huu huwa mzuri, watu huongea na kutoleana mawaidha yenye muafaka kiungwana kabisa. Lakini mara tu baada ya kuyakata makali haya kwa muda hivi, washiriki wake hupumbazwa na huanza kuyakata matindi mithili ya komba mpaka kiasi cha kubwata maneno ovyo ovyo na hatimaye kupoteza mbali fahamu. Ndipo kuruka kwa akili na kuanza zahama zenye kuonyesha utoto badala ya utu uzima. Kadiri makali hayo yanavyosiliwa kwa kuiva kwake, ndivyo wafuasi na mashabiki wake huyatumia kwa wingi na hata kuyaabudu, huyaabufu; huyabugia bila kujali uzito.

Na iwapo ndio kwanza wapokee mabunda yao, hakuna la kutia kikomo tafrija hizo ila uzito wa matendo ya ubadhirifu hujitokeza baada ya kurudi nyumbani, kulala fofofo na wazindukanapo siku ya pili yake ndipo wagundue walivyo taabani.

Mtindo wa matumizi ya faragha hutokea tangu mwanzo wa mazingira ya mtu; hivyo tangu utoto wake; tabia njema na zipasazo huhitajiwa kufunzwa. Sehemu kubwa ya mafunzo haya muhimu hutokana na malezi ya nyumbani chini ya uongozi wa mama na baba. Kama wasemavyo wahenga, mtoto akuavyo ndivyo alivyolelewa. Na mama mtu awe nyoka, hapana budi kuwa mwanawe naye atainuka kustahabu unyoke" wa mama yake. Hivyo ni wajibu wa wazazi kujenga mazingira yanayofaa kwa vizazi vya kesho kwa kuelekezwa namna yake. Ingewezekana himizo kubwa lingesisitizwa katika marekebisho ya tabia za wazazi kuwezesha manufaa yake. Ingewezekana, himizo kubwa lingesisitizwa katika marekebisho ya tabia za wazazi kuwezesha watoto kuiga mtindo au mitindo ya maisha yanayofaa. Kielezo chema ni kuwa na mzazi mwenye tabia njema kwa mtoto wake, rafiki zake na kwa jamii yake.

(a) Ni nini umuhimu wa faragha kwa binadamu kwa mujibu wa aya ya kwanza?(maneno 20)

(b) Eleza jinsi watu wengine wanavyoharibu wakati wao wa faragha kwamambo ya upotovu



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

kwa kurejelea aya ya pili na ya tatu (maneno 30) (al. 5 al. 1ya utiriko)

(c) Eleza mchango wa mzazi kwa mwanwe kuhusu matumizi bora ya wakati wa faragha. Zingatia aya ya mwisho

3. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kulingana na maagizo***

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia huletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo. Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

(a) Fupisha aya mbili za mwanzo (maneno 50 -55)

b) Bila kubadili maana, fupisha aya mbili za mwisho (Maneno 55-60)

Utiririko ni alama 3

4. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Kwa hali nyingine , tunaweza kusema kuwa uchafuzi wa mazingira ni uharibifu wa vile vitu vinavyowazunguka binadamu na wanyama maishani mwao. Kuna uchafuzi wa aina mbalimbali na kila uchafuzi humhusu binadamu kwa njia fulani.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Maendeleo ya viwanda duniani ni sababu mojawapo ya uchafuzi wa hewa. Mitambo katika karakana huwa inatoa moshi mwingi wakati bidhaa zinapotengenezwa. Moshi husambaa eneo kubwa na kuchanganyika na hewa inayovutwa na binadamu. Uchafu hutupwa ovyo ovyo na kuwa hatari kwa afya ya binadamu. Maji machafu huweza kutiririkia mtoni, maziwani na hata baharini. Yale yanayotiririka mitoni na maziwani huchafua maji ambayo hutumiwa na watu wa eneo hilo kwa kunywa, kupika na kunywesha mifugo wao. Yale yanayotiririka baharini huwa ni hatari kwa samaki wanaotegemewa na binadamu kuwa kitoweo muruwa.

Ongezeko la watu pia ni hali nyingine ya uchafuzi wa mazingira. Halaiki ya watu hufanya uharibifu wa misitu ya asili. Hii ni kwa sababu ya kutaka kuongeza ekari za mashamba. Hili husababisha mmomonyoko wa udongo ; hivyo basi kuiacha ardhi bila rutuba yoyote. Katika hali hii, kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa nchi nyingi duniani huzoroteshwa. ‘‘Maisha ya binadamu hutegemea kilimo kwa kila hali kwa hivyo kilimo kinapozoroteka hata uchumi nao huathirika. Kila uchao tunasikia kwamba nchi fulani imekabiliwa na njaa.

Ufugaji wa wanyama wengi bila mpango maalum pia huharibu mazingira ya asili kama nyasi na vichaka. Watu wengi hufuga ng’ombe, mbuzi na kondoo. Kwa kuwa hawana mahali maalum pa kuwalisha, huzunguka nao huku na huko kutafuta nyasi na majani ya kuwalisha. Wanyama wanaotangishwatangishwa namna hiyo humaliza majani na nyasi zote na kuacha ardhi tupu ambayo hatimaye huyabisika kwa jua. Ardhi ya namna hii haishiki maji mvua inyeshapo. Nchi iliyoneemeka huweza kuwa jangwa lililo na chungu ya mchanga.

Watu wanapoongezeka huko mashambani huwabidi wakate misitu ili waanzishe maskani mapyapamoja na mashamba yao. Miti hukatwa bila hadhari na mabiwi ya matawi pamoja na majani huchomwa moto. Jambo la kusikitisha ni kwamba miti hiyo inapokatwa hakuna mingine inayopandwa kuchukua mahali pake.

Mahitaji ya binadamu ya kuendeleza njia za mawasiliano pia huzusha balaa nyingine. Barabara zinazidi kuongezeka na pia watu wanaozidi kuongezeka pamoja na mazao yao. Kwanza, barabara zinapotengenezwa misitu hukatwa mahali zinapopitia. Pili, wingi wa magari huzidi na baadhi ya hayo hutoa moshi unaoharibu hewa.

Njia kadha wa kadha za kuzuia uharibifu wa mazingira zimependekezwa. Ingawa suluhisho timamuhalijafikiwa, Serikali nyingi duniani zimo katika harakati za kutafuta suluhisho la uchafuzi huo.

Njia mojawapo ni kukomesha ujenzi wa viwanda katika miji mikuu na mahali palipo na watu wengi.Wenye viwanda pia wanahimizwa kufikiria jinsi ya kutupa takataka na maji machafu bila kudhuru afya ya binadamu.

Watu wakizingatia suala la upangaji wa uzazi na kuwa na familia ndogo ndogo, idadi ya watu haitaongezeka kwa kasi kwa hivyo itakuwa hakuna haja ya kuanzisha makao mapya mara kwa mara.

Serikali nyingi zimechukua jukumu la kuwaelimisha raia juu ya madhara yanayotokana na uharibifuwa mazingira. Raia wanahimizwa kupanda miti kwa wingi.

Jitihada zinazofanywa kuzuia uchafuzi wa mazingira hukumbana na matatizo. Tatizo kubwa ni fedha za kuendeleza miradi inayopendekezwa. Shida nyingine ni kwamba juhudi zingine huwa zinamwingilia binadamu na mali yake.

**<u>Maswali.</u>**

(a) Fupisha aya za kwanza sita za taarifa uliyosoma (maneno 50-60)

(b) Fupisha aya za mwisho tano kwa maneno 40-45



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

5. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Vijana wa siku hizi hujifikiria kuwa wao ni bora kuliko wazee wao. Wao hujifikiria kuwa wameelimika zaidi, wana busara zaidi, wanauelewa ulimwengu vizuri zaidi na wanaweza kujiamulia hatima yao bila uongozi wa wazazi wao. Wazee kwa upande wao, hawakubali kabisa madai ya aina hiyo. Kwao ni maasi tu. Wanachojua wazee kwa hakika ni kuwa vijana wa siku hizi hawaajibiki kwa lolote, wamedekezwa mno na wanapenda sana nafsi zao. Kwa sababu hiyo, vijana wanahitaji uongozi na ushauri wa wazeee.

Je, kuishi kwingi ni kuona mengi? Ingawa wazee wanafikiria wanajua mengi kwa sababu ya umri wao, vijana hupenda sana kukosoa fikira za wazee wao. Hawakubali imani na itikadi za wazee wao. Kwa mfano; vijana hupendelea mitindo ya mywele ambayo wazee wao hufikiria kuwa kichaa tu.

Wazee husifiwa sana enzi zao. Husifia jinsi walivyolelewa kwa kuchapwa na kufanyishwa kazi zinazohitaji uvumilivu mkubwa kama vile kuchanja kuni, kufyeka misitu, kutayarisha mashamba, kuwinda na kadhalika. Kwa sababu ya malezi hayo, wazee husema wao walirithi nidhamu nzuri na ushujaa. Vijabna kwa upande wao hawaoni chochote cha kujivunia katika zama za wazee wao; wao hufikiria kuwa wazee wao walilelewa kwa ukatili kwa sababu zama zao zilikuwa enzi za giza, kabla ya majilio ya uungwana na ustaarabu wa kisasa.

Wazee husifia kuwakumbusha vijana ule msemo mashuhuri wa wahenga usemao kuwa 'mwacha mila ni mtumwa.' Kwa maoni ya wazee, vijana wengi wamekuwa watumwa kwa sababu wao huonyesha kwa vitendo kuwa hawadhamini desturi za wazee wao. Ka mfano; vijana hawafuati miiko ya jadi, hawapendi kuhudhuria sherehe za kienyeji, kwa mfano sherehe za kutoa makafara. Vijana pia hawapendi ngoma za kitamaduni, na isitoshe vijana hawazionei fahari koo zao. Vijana hawakubali kuwa wao ni watumwa wa mtu yeyote. Mila wanazosifia wazeee wao si vitu vyenye umuhimu wowote kwa vijana. Kwa mfano; baadhi ya miiko ni kisayansi. Kuhusu ukoo, si vijana wengi wanaona umuhimu wake. Ukoo na kabila zilikuwa muhimu zamani wakati ambapo kulikuwa hakuna serikali, bima na hata kazi ya mtu binafsi. Mambo haya sasa ni kama masalia ya zamani ambayo yamepitwa na wakati.

Je, vijana hupenda sana burudani na anasa tu kama wanavyodai wazee! Wazee wengi hufikiria kuwa vijana hupoteza muda wao mwingi kujitafutia anasa na burudani kwa mfano vijana wengi hurandaranda barabarani au mitaani wakisingizia kupunga hewa. Wengine huenda sinema na kuhudhuria dansi na karamu zisizo na manufaa. Vijana kwa upande wao hawaoni kinachowawasha wazee wao; pilipili wasioila yawashia nini?

1. Katika makala haya wazee wana malalamiko yapi kuhusu vijana? (maneno 50-60)
2. Msemo unaosema "Mwacha mila ni mtumwa" unathibitishwa vipi katika maoni ya wazee katika makala haya? (maneno 15- 25)

6. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo itokeapo amali, shughuli na harakati zote za kiuchumi ghairi ya zile ambazo ni za lazima kwa serikali au dola kama ulinzi, sheria na mpangilio wa jamii huwa huria kwa watu binafsi. Msingi wa soko huria, sifa kuu ya utandawazi, ni kuibua na kudumisha mazingira na hali zinazochochea na kumruhusu mtu yeyote kuongozwa na hawaa, au matamanio ya kibiashara anayoyaona sawa pasi na hofu ya kuingilia na udhibiti wa serikali.

Mazingira hayo yanawapa watu satua ya kufanya maamuzi kuhusu hatima yao ya kiuchumi, uamuzi kuhusu suala la ajira yao, matumizi ya mtaji kipato na harija zake, na uwekezaji mzima. Suala mojawapo linaloibuka kuhusiana na mfano wa soko huria ni kuweka



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

mipaka bainifu na wazi baina ya amali na shughuli zinazohusishwa na serikali na zile ambazo huachwa huria kwa watu. Kwa mfano, inaaminiwa kuwa haki ya kuishi na kulindwa dhidi ya shambulizi, liwe la kijambazi au la kigaidi, ni ya kimsingi ambayo haiwezi kuhusishwa na uwezo wa kiuchumi wa mtu binafsi. Aidha huduma za kimsingi za afya nazo zinaingia katika kumbo hili. Ikiwa huduma hizi zitaachwa huria pana uwezekano mkubwa kuwa zitaishia kuwa istihaki ya wenye mtaji na kipato cha juu tu.

Licha ya kuwepo kwa sheria au kanuni huria kutoka nyanja maalum, hutokea hali ambapo adhibiti wa kiserikali ni lazima. Hii hutokea pale ambapo ipo haja ya kuyalinda mazingira hasa kutokana na uchafuzi wa viwanda au tasnia. Aidha udhibiti huo ni lazima pale ambapo haki za watu wengine zinahusika: yaani ikiwa uhuru wa hata mtu mmoja unaadhirika kutokana na sera hizo pana haja ya kuingilia ili kuisawazisha hali yenyewe.

(a) Andika kwa muhtasari maana ya uchumi wa soko huria kulingana na taarifa hii.
(maneno 25-30) (al. 5, 1mtiririko)

(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya pili na ya tatu.
(maneno 70-75) (al. 10,3 za mtiririko)

**7.** **WAJIBU**

Sisi vijana ni wa taifa. Hatuna budi kutumikia umma kwa moyo wetu wote.Hakuna haja ya kulaza damu ikiwa taifa linatuhitaji. Ni lazima tuwe shupavu kwa mambo yote. Tuwe wenye busara, adabu njema na ari ya kutenda kazi kwa moyo wa utu. Ni muhimu kabisa kulinda, kutumikia na kuendeleza taifa hili changa katika mbinu zake na mipango yake yote kuhusu zaraa, elimu, uchumi, ulinzi na mipango yote ya maendeleo ya ustawi wa nchi na jamii. Inatupasa tuelewe ujamaa wetu na jinsi ya kupambana na ubepari, ukabila, ukupe, unyonyaji na ukoloni mamboleo. Hii itaondoa kabisa jasho letu. Inatubidi sisi vijana tujifunze jinsi na namna ya kuwa watu bora.

Elimu tuipatayo kutoka nyumbani, shuleni na katika jamii, lazima igeuze fikira zetu. Elimu hiyo lazima tuitumie ili itupatie uwezo wa kuelewa mema na mabaya maishani mwetu. Ni bora tujue wajibu wetu katika kufikiri, kusema na hata kutenda kufuatana na wajibu huo kwa mioyo na dhamiri safi. Tuwe vielezo kwa wengine. Hasa tujitayarishe kuwa wazazi na viongozi bora wa kesho. Mno mno tuwe wazalendo na raia wema wa taifa hili changa. Tuhimize na kuendeleza utamaduni wetu wa lugha yetu ya taifa. Hatimaye tutambue usawa wa kila binadamu, popote alipo bila kujali taifa, kabila, rangi na hata dhehebu yake.

Tujifunze kujishutumu. Pia tukubali kusahihishwa makosa yetu na watu wengine. Hasa tuwe nguzo, kinga na ngao ya nchi yetu inapopigwa adharusi.

Acha nirudie kusema tena kuwa ni shabaha yetu sisi vijana kuwa na nidhamu njema. Nidhamu njema ni chanzo cha asili cha siha ya ujamaa na kujitegemea. Kwa hivyo, uongozi bora na bidii, ushirikiano mzuri na kujishughulisha. Uchaguzi bora wa viongozi na mifano mizuri ni kurunzi ya maendeleo ya ustawi wetu.

(i) Ni nguzo zipi ambazo kifungu hiki kimezipa kipaombele kwamba zitasimamisha ustawi na maendeleo ya nchi kutokana na vijana? Jadili kwa maneno thelathini

(ii) Vijana wameshauriwa wafanye mambo mengi mema. Jadili kinyume cha ushauri huu ukitumia maneno yako mwenyewe



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

# **8.** MUHTASARI

Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu huathirika na biashara ya kimataifa. Biashara hiyo inaweza kuwa inafanywa kwa uagizaji ama uuzaji wa bidhaa nchi nyingine.

Biashara ya kimataifa ina umuhimu mkubwa. Kwanza, inaiwezesha nchi kupata bidhaa ambazo haizitengenezi mbali na kusaidia kuwepo uhusiano kati ya nchi mbalimbali. Uhusiano huu huiwezesha nchi kupata bidhaa kwa bei rahisi kuliko ambavyo ingekuwa kama zingetengenezawa kwao, hasa wakati nchi inayohusika haina malighafi yanaohusika katika utengenezaji wa bidhaa hizo. Pia, husaidia wakati nchi imekumbwa na dharura au majanga kwani itaauniwa na nchi nyingine ingawa hali kama hii haihakikishwi. Ushirikiano huu vilevile huchochea upatikanaji wa nafasi za kazi kwa wengi.

Kwa sababu za kushughulikia utengezaji wa bidhaa na utoaji huduma nyingine kutakana na uzoefu wa muda mrefu na kuwepo raslimali, nchi huwa na uzoefu fulani. Ni kwa sababu hii ndio nchi inaiwezesha kupata pesa za kigeni na kuuza bidhaa za ziada.

Hata hivyo, kuna matatizo yanayozikumba nchi za kiafrika katika biashara hii, yanayotokana na ukosefu wa usawa baina ya nchi zinazoshiriki biashara. Kwanza, biashara ya aina hii hutatiza viwanda vichanga katika nchi zinazoendelea kwa ushindani usio sawa. Ajabu ni kwamba nchi ziliozoendelea zimetumia biashara hii 'kutupa'bidhaa za hali ya chini ama zenye athari kwa hali za kijamii. Urafiki haukosi. Ikiwa nchi inategemea uagizaji wa bidhaa, haitaweza kuikosa ama kuhitilafiana na nchi ambayo inaitegemea, hivyo kuathiri uhuru wa nchi kama hiyo.

Hata hivyo, nchi mbalimbali zimeweka mikakata ya kulinda viwanda vichanga kutokana na athari za biashara kama hii. Baadhi ya nchi zimeweka ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kwa wasio washirika wao kibiashara. Licha ya hayo, baadhi ya bidhaa zinazonuiwa kwa nje kwa matumizi ya kielimu, urafiti wa kisayansi na bidhaa za maonyesho huagizwa bila ushuru huo. Wakati mwingine ni Banki kuu ndiyo hutoa leseni kwa niaba ya serikali kama njia ya kudhibiti bidhaa kutoka nje. Njia nyingine za kuvisaidia viwanda nchini kuuza bidhaa kwa ya chini ya kuvipunguzia ushuru, usafirishaji nafuu na kuvipa mikopo.

Serikali nyingine huhakikisha kuwa ni bidhaa kiasi Fulani tu ambazo zinaweza kuagizwa kwa kipindi Fulani. Kwa mfano, kuna idadi fulani ya magari kutoka nje yanayoweza kuagizwa kuja Kenya kwa mwaka mmoja. Hata hivyo, wakati mwingine, serikali husitisha uagizaji wa bidhaa kama vile dawa, sinema, maandishi ya kisiasa na vitabu kutokanje; bidhaa ambazo zinachukuliwa kuwa hatari kwa nchi.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

a) Fafanua mambo yote muhimu yanayozungumziwa katika aya za kwa kwanza tatu

( maneno 40-50)

**Matayarisho** (alama 8, 1 ya utiririko)

Jibu

b) Fupisha aya za mwisho mbili bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi.

(maneno 45)

(alama 7, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

Jibu.

## 9.UFUPISHO

***Soma makala yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.***

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu; kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa idhini maalum ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama. Hawa ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizo nazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati ipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari; amefika mwezini; amevumbua uyoka; amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambacho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri dunia kwa kila lilo jema kwa siku sita mtawalia na kumpa binadamu mazingira murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri, akamwambia binadamu, "haya, twende kazi."

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji – taka ovyo hadi mitoni, maziwa na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambayo ni urithi aliopewa na muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya 'maendeleo' yake. Moshi kutoka katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozoni ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya asidi inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa 'tsunami' bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi. Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorokea wapi?

Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe.

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengine kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya basafu!

**Maswali**

(a) Bila kupoteza maana asilia, **fupisha** aya ya kwanza na ya pili. (maneno 50-60).
(alama 5 – alama1 ya Mtiririko).

**Matayarisho**

**Jibu**



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(b) **Eleza** mambo muhimu yaliyoshughulikiwa na mwandishi katika aya nne za mwisho.

(maneno 90-100) (alama 8- alama 1ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

## 10. UFUPISHO

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Sehemu muhimu ya elimu tamaduni ilikuwa ile ya maisha ya ndoa. Vijana wake kwa waume, kwanza walifunzwa umuhimu wa kujiheshimu kimwili kabla ya kuolewa ama kuoa. Ilikuwa mwiko na aibu kwa msichana kupata mimba nyumbani, au kwa mvulana kumtunga mimba msichana kabla ya ndoa. Kwa hivyo shida ya watoto wa haramu haikuwepo katika jamii. Mafunzo kuhusu mpango wa uzazi yalikuwa muhimu. Ilikuwa ni aibu kwa mume na mkewe kuzaa watoto kabla ya miaka miwili au zaidi kupita. Wakati wa kunyonyesha mtoto, mume na mke walitarajiwa kutoonana kimwili, na hii ilisaidia katika kumlea mtoto.

Vijana wanaume kwa wake waliaswa kuhusu kuchagua wachumba wao kwa kuelezwa ni ukoo au mbari gani ingefaa kuoa au kuolewa nao. Ndoa zote zilihitaji vibali vya wazazi wa mume na mke. Haya yalipunguza shida za talaka kwenye jamii.

Vijana walifunzwa kuyaelewa mazingira yao, hasa kuhusu hali ya anga, ili wafahamu majira ya mvua na ukame. Walifunzwa kuchunguza na kufafanua hali za miti, ndege, nyota na wanyama wengine kujua ni majira gani ya hali ya hewa wanayotarajia ili kujiandaa nayo. Mafunzo ya hali ya hewa yaliwasaidia baadaye maishani katika shughuli zao za ukulima, ili waweze kutofautisha baina ya udongo wenye rutuba na ulio dhaifu, na pia waweze kujua mimea iliyoweza kumea katika aina mbalimbali za ardhi. Kutokana na mimea ya asilia mbalimbali, walijifunza ubora wa ardhi mbalimbali katika sehemu walizolima.

Elimu tamaduni haikuacha kuwafunza vijana jinsi ya kuyakabili magonjwa kati ya jamii. Kwa hivyo vijana wengine walikulia kuwa waganga waliotegemewa na jamii yao. Matibabu ya mitishamba



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

yalihitaji mafunzo mahususi yahusuyo kuitambua miti ifaayo kwa matibabu na matumizi katika kuponya magonjwa mbalimbali.

Elimu tamaduni ilitolewa na kufunzwa kwa dhati na watu waliofahamu mahitaji ya jamii yao vyema, kwa wakati ufaao kwa vijana wa umri mbalimbali. Mambo muhimu ni kuwa elimu tamaduni ilisadifu matakwa ya maisha ya jamii. Ilikuwa elimu ya maisha yake ya baadaye katika mazingira alimoishi.

**Maswali - .**

a) Eleza jinsi ukosefu wa elimu tamaduni ungeweza kuathiri jamii. (maneno 30) (alama 4)

**Matayarisho**

**Jibu**

b) Eleza umuhimu wa elimu tamaduni katika jamii ya kale. (maneno 80) (alama 11)

**Matayarisho**

**Jibu**

## 11. UFUPISHO (ALAMA 15)

Sisi vijana wa Kenya inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii, na kwa dhati ya mioyo yetu tuweze kupata ufanisi, na uwezekano wa kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu.Tukumbuke,”Ajizi ni nyumba ya njaa ”. Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja.Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu.Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbali mbali ya maendeleo.Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao mashambani, kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeke. Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo pia lazima tujishugulishe na biashara ambapo kwa sasa ni wakenya wachache sasa ambao wanatambua umuhimu wa biashara. Wengi ni wale wenye mawazo ya kwamba lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wengine ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayopata majumbani, shuleni, na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu ya kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwanakenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu lazima washirikiane na kufikiria kwamba wao ni wamoja,"Utengano ni uvundo". Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu ,wakati tunapokosea, lazima tukubali tumekosa na kufanya masahihisho mara moja kwani, "Usipoziba ufa utajenga ukuta".Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujishugulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia ya kutatua matatizo hayo siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashutumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu.Utamaduni wa asili unakariri sana kuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo, lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo.Tukiwa viongozi ambao hawajishugulishi na maendeleo,basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kama kwa utajiri wake.Kwa hivyo, basi tuchagueni viongozi ambao watatuletea ufanisi badala ya viongozi wanaotokana na nasaba kubwa au tajiri.

(a) **Eleza** dhamira ya mwandishi kwa taarifa hii (maneno 20) (alama 2)

**NAKALACHAFU**

**NAKALA SAFI**

(b) Kwa mujibu wa aya ya kwanza, mwandishi awahimiza vijana kufanya nini ili kuleta maendeleo nchini? (maneno 70) (alama 4)

**NAKALA CHAFU**

**NAKALA SAFI**

(c) Kulingana na taarifa hii ni mambo gani hasa ambayo yamechangia maendeleo kuzorota nchini Kenya? (maneno 40 - 50) (alama 6)

**NAKALA CHAFU**



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

**NAKALA SAFI**

## 12. MUHTASARI

**Soma makala haya kisha ujibu maswali**

Ni dhamira ya mwanafunzi yeyote kupata matokeo mazuri katika mtihani wa kitaifa punde tu anapojiunga na shule iwe ni ya sekondari au msingi.

Matokeo hayo hutokea baada ya miaka minane katika shule za msingi na miaka minne katika shule za sekondari. Hata hivyo, punde tu matokeo yanapotangazwa, wengine hujipata wanyonge kwa kugundua kuwa wamefeli au wameambulia nunge kwa mtihani wao wa mwisho.

Miongoni mwa mambo yanayosababisha hali kama hii ni mwelekeo mbaya wa wanafunzi katika baadhi ya masomo. Tunajua kweli kuwa palipo na ushindani lazima kuwe na mshindi na mshindwa. Iwapo ungemwuliza mtahiniwa akueleze jinsi anavyohisi baada ya kushindwa kwenye mtihani wa kitaifa, hatakuwa na la ziada ila kukueleza kuwa hajaridhishwa na matokeo.

Wengine wao hata huvuka mipaka na kuyataja matokeo yao mabaya kusababishwa na vizingiti fulani au kuwakashifu walimu kwa kudai kuwa kulikuwa na hali ya kuonewa darasani. Unapochunguza zaidi, utakuta ya kuwa wanaodaiwa kuwa werevu ni walio stadi katika masomo ya sayansi yanayofikiriwa kuwa magumu.

Wakati wanaofikiriwa kuwa werevu wanapofanya vyema katika mitihani yao, wale wanaokisiwa kuwa wajinga ambao wamefeli hujipata wakiomboleza kwa huzuni kwa muda mrefu.

Swali la miaka mingi kuhusu elimu limekuwa ni kwa nini wanafunzi wote hawawezi wakafanya vyema na kufaulu katika mitihani ya kitaifa. Utafiti uliofanywa umebainisha wazi kwamba kunazo sababu kadhaa zinazochangia matokeo mabaya.

Mojawapo ya sababu hizo, na ambayo ni muhimu sana ni ukosefu wa nidhamu shuleni. Mwanafunzi wa aina hii hajali anachoambiwa na walimu na aghalabu muda wake mwingi unapotelea katika adhabu. Wakati mwanafunzi anapokosa nidhamu iwe kwa wazazi au walimu wake, masomo yake huathirika. Matokeo yake katika mitihani hayatakuwa mazuri. Ni Lazima tabia ya mwanafunzi iambatane na matokeo yake. Sababu nyingine ni mshituko unaowapata punde tu wanapoketi kwenye viti vyao kufanya mitihani ya kitaifa. Mtahiniwa anapojikuta katika hali hii, kuna uwezekano asifaulu katika masomo yake.

Kuna uwezekano wa wanafunzi aliyefeli katika mtihani wa darasa la nane kufanya vyema katika shule ya upili na kupita mtihani wake wa kidato cha nne. Ilibainika pia kuwa wale waliofaulu katika mtihani wa darasa la nane hulegeza juhudi zao masomoni na huwa hawapati alama zinazoambatana na zile walizopata katika shule za msingi.

Sababu nyingine ya kuwafanya wanafunzi kutofanya vyema katika mtihani ni kubaguliwa kwa wanafunzi hafifu na walimu na kukosa kushughulikiwa ipasavyo. Baadhi ya walimu wanapogundua kuwa wanafunzi fulani hawafanyi vyema katika masomo fulani, hawatumii muda wao mwingi kuwasukuma ili kuyaboresha matokeo. Badala yake huwashughulikia wanaoelewa haraka darasani.

Kuna wanafunzi wengine wanaochukua muda mrefu kuelewa, si ya kwamba ni wajinga, la, ni katika somo moja tu. Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha mwanafunzi kama huyu anapata nafasi ya kuelewa anachofunzwa.

Wanafunzi wengine hawafanyi vyema kwa sababu wazazi wao hawamudu kuwalipia karo kwa sababu ya umaskini, hawawezi hata kulipia masomo ya ziada kwa shule zinazosomesha wanafunzi wakati wa likizo.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Kulingana na takwimu za elimu, muda wa kawaida hautoshi kukamilisha mtaala wa masomo ya mfumo wa 8-4-4, kwani ni mpana sana. Walimu wanaombwa kushughulikia mafunzo ya ziada.

**MASWALI**

a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za mwanzo. Maneno (55 – 60). Alama 7

**Matayarisho**
**Nakala safi**

b) Fafanua sababu zinanzowafanya wanafunzi kutofua dafu katika masomo yao. Maneno ( 50 – 55) Alama 6)

**Matayarisho**
**Nakala safi**

(utiririko alama 2)

**13.MUHTASARI (ALAMA 15) .**

**Soma taarifa hii ifuatayo kisha ujibu maswali**

Kufaulu kwa lugha ya Kiswahili kutumika katika nyanja za sayansi na teknologia kunategemea sana utekelezaji wa mpango wa kwanza wa kutumia Kiswahili kufundisha elimu ya juu. Wanafunzi wakiwa weledi wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kujifunza masomo ya sayansi, ufundi itawasaidia kujenga moyo wa udadisi, moyo wa kujiamini na moyo wa kutafuta maarifa ya ziada, wao wenyewe kwa kusoma vitabu mbalimbali vikiwemo vitabu vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

-

- Moyo huu wa udadisi ndio msingi wa mtu kuwa mbunifu na mvumbuzi wa vitu mbalimbali. Wanafunzi hujenga moyo wa udadisi na kujiamini ikiwa lugha inayotumika kufundisha inaeleweka vizuri kwao. Hali hii hujidhihirisha pale wanafunzi wanapouliza maswali ya kutaka kujua zaidi kuhusu mada wanazofundishwa darasani au mambo wanayosoma wenyewe katika vitabu vya rejea. Ari hii ya udadisi miongoni mwa wanafunzi huweza kuonekana kwa kupima aina ya maswali yanayoulizwa. Kimsingi, maswali yote yanayofikirisha na yasiyohitaji jibu la wazi, la moja kwa moja, yanasaidia sana kukuza moyo wa udadisi na kujiamini.
- Kiswahili kinapaswa kuchukua dhima hii mpya ya kutumika katika nyanja za sayansi na teknolojia kwa sababu maendeleo ya jamii hupimwa kwa teknolojia ya kisasa iliyopo. Zamani ulimwengu ulionekana kuwa ni mkubwa lakini sasa hivi kwa kutumia teknolojia mpya ya mtandao wa mawasiliano, ulimwengu sasa unaonekana kuwa sawa na kijiji. Ili tusiachwe nyuma na wenzetu kimaendeleo, hatuhitaji tu kuwa watumiaji bali pia kuwa wachangiaji wa teknolojia hii mpya ya kisasa.
- Tunahitaji teknolojia hii kwa lugha ya Kiswahili ili watu wengi zaidi wasiojua kutumia lugha za kigeni (Kiingereza, Kifaransa n.k) waweze nao kujifunza teknolojia hii mpya kwa Kiswahili. Mathalani,



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

kwa kuanzia tunahitaji teknolojia iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili yaani jinsi ya kutengeneza: *'Spellcheck'* ya Kiswahili kwa kutumia kompyuta, '*machine translation'* ya lugha ya Kiswahili na kutumia lugha nyingine muhimu duniani, mawasiliano ya mtandao kwa kutumia *barua–e* na jinsi ya kutengeneza programu mbalimbali za kompyuta kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Jamii itanufaika sana na teknolojia hii mpya ikiwa tu itakuwa imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

- **2. MASWALI**
- a) Andika anwani mwafaka kwa taarifa uliyosoma. (Maneno 5 –6)(Alama 1)
- **Matayarisho**
  - **JIbu**

b) Kwa nini Kiswahili kinafaa kuafiki mabadiliko katika nyanja za sayansi na teknolojia?

(Maneno 55 – 65) (alama 8)

**Matayarisho**

**Jibu**

**c) Fupisha aya ya kwanza na ya pili.**

(Maneno 50 – 60) (Alama 6)

**Jibu**

## <u>14.SWALI LA PILI UFUPISHO</u>

***<u>Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali yanayofuata</u>***

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza, ubongo hunasa jambo kisha hulihifadhi. Baadaye huanzisha mfuno wa kutoa kilichohifadhiwa. Ubongo ukiathirika kwa namna yoyote katika mojawapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitaji mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini) bidhaa za soya, matunda, maziwa, bidhaa za ngano, samaki pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madini haya ni mboga za kijani , dengu, mawele, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati, awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini kwa hivyo vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisichohatarisha maisha.  Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa na kuhusisha jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kuvuruga kiakili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na namna ya kukitoa.

Hali kadhalika mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa kuwa mazoezi ya kuyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na ratiba ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya haya mazoezi ya kiakili kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo, vitanza ndimi, ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo wa kuyakumbuka mambo ni jamii iliyopiga hatua kimendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

(**Ijaribu na uikarabati Isaac Ipara/ Francis waititu Uk 180 – 181**)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

## Maswali

Kwa maneno 60 – 65, **fupisha** mchango wa chakula katika uimarishaji wa uwezo wa kukumbuka.

## Matayarisho

## Jibu

**Fupisha** aya tatu za mwisho za mwisho kwa maneno 80-90

## Matayarisho

## Jibu

# 15.MUHTASARI:

***Mzee Kondoo***: Wenyeji wa kijiji cha maendeleo; mabibi na mabwana pokeeni salamu zangu na shukrani kwa kuhudhuria mkutano huu. mimi pamoja na wazee wenzangu tuliamua kwa kauli moja kuwaita nyote hapa ili kujadili maendeleo ya kijiji chetu. Jambo linalotukera sisi wazee ni kwamba hali ya kijiji chetu inazidi kuzoroteka. Kijiji chetu kiliitwa maendeleo sisi wazazi wake tulipokuwa na rai ya kuleta maendeleo. Wake kwa waume tulijifunga vibwebwe na kwa kweli juhudi zetu zilitoa matunda mema. Sasa nguvu zimeanza kutuishia; leo tupo, kesho tutakuwa hatupo. Ninyi ndio mtakaoshika usukani. Kama tunavyoona, mambo yakiendelea namna hii, watoto wenu wataishi maisha ya dhiki. Tungependa ninyi wenyewe mtueleze kwa nini kijiji maarufu cha maendeleo kinarudi nyuma badala ya kuendelea mbele. Kila anayetaka kutoa hoja zake atapewa fursa ya kufanya hivyo. Lakini kwanza mzee mwenzangu ana machache ya kusema.

***Rojo***: Asante sana mzee Kondoo. Kwa upande wangu naona kwamba tumekuwa pweza kujipalia makaa na kwa mintaarafu hii, maendeleo ya kijiji chetu yakaanza kuzoroteka. Kwa ufupi, tunazaa watoto tusioweza kuwalea. Ni hivi majuzi tu tulipomkuta mtoto mmoja amezirai …

***Jara***: Wee! Kaa chini. Usituletee aibu hapa. Sisi ni watu wa kuheshimiwa. Ufahamu kwamba hukupewa fursa ili uanze kuchambua nyumba za wengine. Mungu mwenyewe alitoa amri kwamba watu wazae mpaka waijaze dunia.

***Jilo***: Mimi namwunga mkono Jara. Anayosema Rojo hayafai kuruhusiwa kuzungumzwa tena.

***Mzee Kondoo***: Hatukuwaita hapa mje mgombane. Rojo hajataja jina la mtu wala hajamaliza kutoa hoja zake. Endelea bwana Rojo.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

***Rojo***: Nashukuru Mzee Kondoo. Ndugu, mimi nitatoa ule ukweli. Humu kijijini mwetu mna watoto ambao hawaendi shule. Kazi yao ni kuzurura kila mahali na kuokotaokota mali za watu. Hata huingia mashambani mwa watu wakaiba matunda, mihogo, mahindi na mazao mengine wakapeleka mijini kuuza. Mimi kitendo kama hiki nakilaani kwani ndicho kinachorudisha maendeleo ya kijiji chetu nyuma.

***Uledi***: Hayo usemayo ni kweli. Juzi walikuja usiku mwenyewe siko wakavunja mlango wakafagia nyumba yangu fyu! Vitendo vya vijana hawa vinadhihirisha ukosefu wa malezi bora. Mabwana na mabibi, mimi sipingi uzazi lakini yule azaaye atambue jukumu lake la kuwalea vizuri watoto hao hata kama ni ishirini: awalishe, awavishe, awatibu wawapo wagonjwa, awafunze tabia njema na kupelekwa shuleni ili wakuapo waweze kujimudu na kushirikiana nasi katika kuendeleza kijiji chetu.

***Heri***: Mabibi na mabwana mtaniwia radhi kwa vile ambavyo sina mke wala watoto. Hata hivyo sitasita kutoa maoni yangu. Wasemayo wenzetu ni ya kuungwa mkono. Watoto wakosao malezi bora ndio hatari katika kijiji chetu. Wakazi wa kijiji hiki wamekuwa waoga hata hawawezi kujenga maduka wakaendesha biashara zao humu.

***Rojo***: Mbali na uhalifu wa vijana wetu sisi watu wazima pia twafaa kulaumiwa. Kwanza tumeshindwa kutimiza wajibu wetu kwa ajili ya ulevi. Tumeshiriki ulevi hata kwamba hatudiriki makazini wala mwetu majumbani. Vipi tutadumisha nidhamu katika jamii zetu? Pia tusisahau kwamba ili kuwa na jamii ya kuimudu siku hizi hali ya maisha imepanda juu na tusipokuwa na busara yatatushinda.

***Uledi***: Zaidi ya hayo inatupasa tuzingatie miradi mbalimbali itakayotuletea maendeleo …

**Maswali:**

1. Kwa nini wazee walikereka kuona kijiji chao kikizoroteka? (maneno 15)(alama 3)
   **NAKALA CHAFU**
   **NAKALA SAFI**

2. Wanakijiji cha maendeleo wamekuwa pweza kujipalia makaa kwa vipi? (maneno 50) (alama 8)
   **NAKALA CHAFU**
   **NAKALA SAFI**

3. Uledi ana wazo gani kuhusu mpango wa uzazi? (maneno 15). (alama 2)
   **NAKALA CHAFU**
   **NAKALA SAFI**

4. Eleza mambo yanayozorotesha kijiji cha maendeleo? (maneno 50). (alama 7)
   **NAKALA CHAFU**
   **NAKALA SAFI**



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

## 16. MUKHTASARI

**Soma taarifa ufuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo**

Ponografia ni tendo, maandishi, picha au mchoro unaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, video, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, wavuti, DVD, n.k.

Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea ulimwenguni kote mithili ya moto katika mbuga wakati wa kiangazi. Uenezi umechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Matumizi ya tarakilishi, mdahilishi na viungambali vya picha yamesambaza ponografia ilivyoanza. Hata hivyo, hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbali mbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la ama kuvuruga maadili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu. Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Hivi sasa, kundi kubwa ni lile la wanotumia matusi haya kama njia ya kuchuma. Kwa mfano, wanamziki ambao hutumia ponografia kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji ponografia kuna athari kubwa kwa jamii na hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushahidi kuonyesha kuwa wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kuwa kinachoonekana na jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama masomo watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera. Hivyo basi huanza kuiga wanayoyaona na kusikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Kutokana na uchafu huu, watu wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni mengi. Haya ni pamoja na ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa. Wengine nao huambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo huwaletea mauti.

Inasemekana kuwa akili za binadamu hunata zaidi mambo yanayowasilishwa kwa picha. Si ajabu vijana huyadumisha matusi haya katika kumbukumbu zao na kuyasanya sehemu ya maisha yao. Wengi huanza kuandama tabia mbovu kama ushoga, ubasha na usagaji. Kuna wale ambao huanza kujichua. Kujichua ni hali ya mwanamke au mwanaume kumaliza haja za kimaumbile bila kufanya mapenzi na mtu mwingine. Ponografia imechangia pakubwa kuenea kwa haya.

Jambo hili limegeuza mielekeo ya vijana. Wanaiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Halikadhalika, huiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono. Yote haya yanapingana na desturi za Mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kila kukuchapo.

Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama unywaji wa pombe, matumizi ya dawa za kulevya, uvutaji sigara na utumiaji wa dawa za kuchochea uchu wa ngono. Mambo haya huwapa vijana tabia za unyama.

Jambo hatari ni kuwa kuendelea kutazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, yaani huondoa makali. Hata katika utu uzima, mtu atapoteza mhemko wa kawaida na kugeuzwa kuwa



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na maenezi haya yasio na kizuizi.

Jambo la kwanza ni kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi. Kwa namna hii itawezekana kupunguza mahitaji na uuzaji wa pnografia. Aidha ni vizuri watu wazima wawajibike ile wawalinde hasa vijana kutokana na athari hizi. Inapasa wenye midahilishi, video na sinema wasiwaruhusu vijana kutazama uchafu huu.

Tatizo la kuenea kwa ponografia limeendelea kuwepo kwa sababu ya udhaifu wa sheria. Kilichoko basi ni kuweka sheria za kuzuia utengenezaji na usambazaji wa upujufu huu. Kuambatana na haya, hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja sheria hizi. Hali kadhalika, ushirikiano wa karibu baina ya wadau uimarishwe katika ulimwengu mzima. Serikali na wanaohusika wakabiliwe ipasavyo. Jamii ingependa kuona michakato ya kuharamisha utengenezaji, usambazaji na utangazaji wa ponografia ikiwekwa.

Wazazi nao wasijipweteke tu bali nao wasaidie. Ni muhimu washikilie kwa shati juhudi zao za kuwaelekeza na kuwashauri watoto kuzingatia uongofu na kukwepa picha hizi najisi. Watoto lazima waeleweshwe kuwa haifai kutazama picha au michoro michafu. Itikadi na imani za kidini na utamaduni wa Kiafrika unakataza vikali mtu kuona uchi wa mtu mwingine. Matokeo ya kuasi makatazo haya yana madhara makubwa kwa watu na jamii.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu, fanya muhtasari wa aya ya pili naya tatu. (maneno 20 – 25) (alama 6, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya nne hadi ya tisa. (Maneno 55-60) (aama 9, 1 ya utiririrko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## 17.<u>UFUPISHO</u>

**<u>Soma makala yafuatayo kisha uiibu maswali yanavofuata.</u>**

UGONJWA wa utando wa ubongo ambao kwa kiingereza unafahamika kama *meningitis* huzua hofu miongoni mwa watu wengi. Ugonjwa huo pia hujulikana kama homa ya uti wa mgongo.

Hofu kama hizo zinaeleweka kwa sababu utando wa ubongo ni ugonjwa unaoathiri ngozi inayofunika ubongo na uti wa mgongo na kwa hivyo ni rahisi mno kusababisha kifo ikiwa mgonjwa hatahudumiwa haraka iwezekanavyo.

Utando wa ubongo ni ugonjwa unaosababishwa na virusi na bakteria, Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, utando wa ubongo unaosababishwa na virusi sio hatari sana kwa uhai wa mtu ikilinganishwa na bakteria. Japo watu wengi wanaougua utando wa ubongo hutibiwa na kupona, baadhi yao huachwa wakiwa bubu au vipofu na wengine kufariki.

Shida kubwa ya ugonjwa huu ni kwamba unatokea bila kutarajiwa. Kwa mfano mtoto au mtu wa umri mkubwa anaweza kuwa mzima kwa muda wa dakika kadha ila baadaye kuwa mgonjwa mahututi baada ya kukumbwa na ugonjwa huo. Shida nyingine ya ugonjwa huu ni kwamba huwa vigumu kutenganisha dalili za ugonjwa huu na dalili za magonjwa mengine ya kawaida kama vile



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

maumivu ya kichwa. Kwa hivyo kuna baadhi ya watu wanaomeza dawa za kupunguza maumivu ya kichwa bila kujua wanaugua utando wa ubongo.

Dalili za watoto wanaougua utando wa ubongo ni homa, kutapika, mtoto kukataa kula na kulia kwa uchungu. Mtoto anayeugua ugonjwa huu kadhalika huwa anaonyesha dalili za kufura kichwa, kupumua kwa haraka na kutupatupa miguu huku mwili wake ukiwa umejikunyata. Watu walio na umri mkubwa nao huonyesha dalili za maumivu makali ya kichwa, kuwa na shingo nzito (stiff neck) na mgonjwa kuepukana na mwangaza. Kadhalika mgonjwa hushikwa na homa na pia kutapika kando na kukosa ufahamu.

Utafiti umeonyesha kwamba watu walio na umri mkubwa kadhalika huonyesha dalili za kuwa na mikono au miguu baridi, maumivu ya misuli na tumbo hasa kutokana na damu kuwa na sumu. Ni muhimu kufahamu kwamba sio kila mtu anahisi dalili hizi, ikiwa yeyote atashuhudia baadhi ya dalili hizi itakuwa bora kufika hospitalini haraka kupata usaidizi wa daktari kabla ya ugonjwa huo kuzidi sana.

Yeyote anayeshuku kwamba anaugua utando wa ubongo anapaswa kupelekwa hospitalini mara moja. Hii ni kwa sababu ni rahisi mno kwa madaktari kutibu mgonjwa anayepelekwa hospitalini punde tu anapoonyesha dalili ikilinganishwa na yule anayepelekwa huko kama amechelewa.

## Maswali

Bila kubadilisha maana fupisha aya nne za mwanzo (Maneno 70-80)
( alama 7, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, eleza dalili za ugonjwa wa utando wa ubongo na huduma kwa mhasiriwa (Maneno 55-65) (alama 6, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## 18.UFUPISHO

Vipindi mbalimbali vya historia vimeshuhudia kuibuka kwa magonjwa ya ajabu. Magonjwa hayo yamehahangaisha watu na kuzishughulisha bongo za wanasayansi na madaktari katika kutafuta tiba. Magonjwa kama vile tauni, kifua kikuu, homa ya matumbo na ndui ni baadhi ya yale yaliyotisha saria nyakati fulani za historia ya binadamu. Magonjwa haya yaliwauwa maelfu ya watu nakutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Hata hivyo magonjwa hayo yaliweza kuchunguzwa na kutafutiwa tiba kabla ya kumaliza kabisa kizazi cha binadamu. Lakini hii baada ya kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. Ulimwengu wa sasa unashuhudia janga jingine la maradhi sugu ya Ukimwi. Neno "UKIMWI" lilitolewa kutokana na athari za ugonjwa huo mwilini. Neno' "UKIMWI humanisha Ukosefa wa Kinga mwilini, ambapo herufi za kwanza za maneno matatu ziliunganshwa pamoja na kuunda neno hilo. Ugonjwa huu ambao tayari umewaua mamilioni ya watu kote ulimwenguni unazidi kuenea kwa kasi, mfano wa moto katika kichaka. Kutokana na kasi yake ya kuua watu, ugonj wa wa UKIMWI umepewa majina kama vile 'umeme' 'napia 'ugonjwa wa vijana'. Watu wengi wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI ni wale walio na miaka kati ya 15 hadi 49. Kundi hili kwa kweli ndilo, linalohesbiwa kuwa na nguvu za kutunza jamii kwa njia nyingi. Iwapo wengi katika kundi hili watakumbwa na maradhi haya, watasalia wakongwe na watoto wasioweza kujimudu.

Nchini Kenya, UKIMWI uligunduliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa

1984. Kufika mwezi wa Juni 1996, inakisiwa kuwa ugonjwa huu ulikuwa umewaua watu wapatao 65,647 nchini. Hivi sasa, inasemekana kuwa takriban watu zaidi ya 500 hufa kila siku nchini Kenya kutokana na janga hili. Aidha, imethibitishwa kwamba takriban watu milioni mbili u nusu tayari watapoteza maisha yao kutokana na kuambukiza virusi vya ugonj wa huu humu nchini. Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa.

Kutokana na kuongezeka kwa visa vya UKIMWI, hospitali na zahanati nyingi kote nchini zinashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa. Kwa hivyo makundi ya kujitoleanamashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahudumia wagonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya makundi hayo hutoa tiba ya kisaikolojia pamoja na kuwapa ushauri wa hima yakuishi,badala ya kukata tamaa. Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani kwao.

Lakini jambo la kuzingatia ni hili, tujifunze kutokana na historia. Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba ya ugonj wa huu itapatikana. Hii ni kwa sababu tumethibitishiwa haya kutoka katika historia yetu wenyewe. Ikiwa magonjwa yaliyosababisha vifo vya wengi kutokana na ukosefu wa tiba yalitokomezwa kupitia juhudi za kimatibabu, sembuse huu ugonjwa tulio nao sasa? Huku tukijikinga kutokana na maradhi haya tusife moyo bali tuwe na matumaini kwani subira huvuta heri.

(a) Kwa kutumia maneno yako mwenyewe na bila kupoteza maana, fupisha aya nne za mwanzo (maneno 90-100 ) (alama3kwamtiririko) (alama 12)

(b) Eleza mambo yanayoleta matumaini kwa wagonjwa wa UKIMWI kulingana na aya tatu za mwisho (Maneno40-50) (alama 1 kwa mtiririko) {alama 4)

Nakalachafu

Jibu



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

# MATUMIZI YA LUGHA

**1.** (a) Andika vinyume vya vitensi vilivyopigwa mistari

(i) **Alikashifiwa** kwa kazi aliyofanya

(ii) Kuimba **kulifurahisha** hadhira

(b) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi

(i) Abiria waliojeruhiwa sana walipelekwa hospitali haraka

(c)Eleza maana **mbilimbili** za sentensi zifuatazo ;

(i) Bibi yake amefika

(ii) Alimpigia mpira

(d) Kwa kutoa mifano, onyesha namna mbili vile kiambishi –j- hutumiwa

(e) irabu **a, i,** na **u** hutamkwa wapi kwenye ulimi?

(f) Kamilisha na kueleza maana ya methali hii

(i) Mfinyanzi -......................................

**(g) Andika usemi huu kwa usemi wa taarifa**

"Kefule! Mtoto huyu ni kaidi kama kirongwe. Hamheshimu babake!" alisema mzee Kamau.

(h) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentenzi ifuatayo

(i) Darasa lililojengwa limefunguliwa rasmi

(ii) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo;

(j) Kanusha sentensi ifuatayo kwa udogo

(i)Mbuzi wake ana manyoya mengi na harufu kali

(k) Onyesha maana **mbili** ya neno taka (ala. 2)

**(l) Andika kwa umoja** (ala. 2)

(i) Tumewaondoleeni matatizo yenu, yafaa mtushukuru

(m) Eleza maana ya misemo:- (ala. 2)

(i) Fuga mtu –

(ii) Kuwa na faragha -

(n) Panga nomino hizi katika ngeli mwafaka (ala 2)

(i) Kipofu- .

(ii) Uyoga- .

(o) Bainisha viwakilishi katika sentenzi kisha useme ni vya aina gain. (alama

i) Mimi nitaondoka kesho

(ii) Huyo alichaguliwa na wengi

2. (a) Tumia kiulizi kifaacho kukamilisha maswali yafuatayo:

(i) Waashi wale wanaishi kwa

(ii) Mtoto alitaka majina…

(iii) Wanitania hivyo

(b) Tambua mzizi katika neno:

Tuliwalimia :



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(c) Andika sentensi **tatu** ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii

Pale ndiko alimoingia

(d) (i) Nini maana ya yambwa (shamirisho)

(ii) Taja aina ya yambua iliyoipigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:

**Mama amempikia baba wali kwa sufuria**

(e) Neno "**mlango**" lina maana ya "uwazi wa kuingilia nyumba." Tunga sentensi **mbili** kubainisha matumizi mawili ya neno hili

(f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya **"ndivyo**"

(g) Chai hiyo iliwavutia watahi **(*Anza* : Watahi…………..)** (al. 2)

(h) Tumia neno **"haraka**" katika sentensi kama: (al. 2)

(i) Nomino (ii) Kielezi

(i) Andika maana **mbil**i za sentensi:

(i) Nenda ukamwone mwenyewe, usiogope.

(j) Onyesha maana za '**ni**' zilizopigiwa mstari

Nihamrishe "**Tokeni darasani**"

(k) Atakapokuja atamletea mlinzi uta na upote

(l) Maneno hayo yako katika ngeli gani?

(i) Ridhaa (ii) Nanasi

(m)Andika mifano ya sauti zenye sifa zifuatazo:

(i) Kipasuo cha kaakaa laini (ii) Nazali ya ufizi

(n) Tumia neno "**ngali**" kutunga sentensi kuonyesha

(i) Kitenzi kisaidizi (ii) Kitenzi kishirikishi

(o) Tumia kirejeshi kuonyesha mazoea katika sentensi ifuatayo:

(i) Mtoto anayelia ni huyu (ii) Neno maana ya kiwakilishi?

(q) Tambulisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani?

1.Nani alikukasirisha?... 2. Huyu huwashinda wote

(r) Tunga sentensi **moja** itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano

3. (a) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi

(i) Kishirikishi kipungufu

(ii) Kikuu

(b) Akifisha

je, unaipenda hali ilivyo mwenzake alitaka kujua

(c) Eleza matumizi ya '**ka**' na '**hu'** katika sentensi zifuatazo.

(i) Nilienda kanisani nikamkuta, nikamwamkua, nikamwomba msamaha.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) Baba hufika nyumbani usiku wa manane

(d) Yakinisha sentensi ifuatayo :

Mama hakutuchapa, hakutupa chakula wala maji

(e) Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti si ghuna huku ukitolea mifano miwili kwa kila aina

(f) Tunga sentensi mbili kutofautisha matumizi ya vitate hivi: Dua na tua

(g) **Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi**

Njia nyembamba ni hatari kwa usafiri wa gari

(h) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia matawi**

Mzee ambaye hukuza pamba amefaidika sana

(i) **Ainisha mofimu zinazojitokeza katika kitenzi hiki**

Waliochekeshwa

(j) **Andika sentensi zifuatazo kulingana na kauli ulizopewa katika mabano**

(i) Ugonjwa wa saratani hufanya watu **wafe** polepole. (kauli ya kutendesha)

(ii) Mkulima **alisuka** kamba ndefu. (Kauli ya kutendata)

(k) **Tunga sentensi moja inayojumulisha sehemu hizi, Ala, kipozi, kitondo na chagizo**

(l) Neno kijana linaweza kutumiwa kama kivumishi au nomino, tunga sentensi kudhihirisha***U**

(i) Kivumishi

(ii) Nomino

(m) **Sahihisha sentensi zifuatazo**

(i) Mtoto ambaye aliyekuwa anacheza ameanguka.

(ii) Vitabu hizi ambazo zimesahihishwa ni za wanafunzi.

(n) Tunga sentensi mbili ukitumia vielezi vya namna mfanano na viigizi.

(o) Bainisha maneno yafuatayo yapo katika ngeli gani kisha tunga sentensi mwafaka:

(i) Manukato (ii) Uwati

(p) Eleza maana ya methali ifuatayo:

"Avunjaye nazi ni lazima aafaidi tui.

**4.** A) **Eleza maana mbili za:**

Mwanaida alikwenda sokoni peke yake.

B) **Akifisha sentensi hizi.**

i) Hodi hapana wenyewe nini Juma alimwaka nitarudi kesho.

C) **Andika maana ya methali ifuatayo.**

Achanikaye kwenye mpini hafi na njaa.

D) **Tumia "O" rejeshi katika sentensi hii.**

Mwanafunzi ambaye hudurusu ndiye hupita mtihani.

E) **Andika sentensi ifuatayo kwa kunyambua maneno yaliyo kwenye mabano kwa usahihi.**

Dhambi za mwanadamu zilim____________ (fa) Bwana Yesu.

F) **Eleza maana ya misemo ifuatayo.**

i) Teka bakunja.

G) **Taja maana ya maneno yaliyopigwa mistari**.

Tulipogawa mkate kila mtu alipata sehemu moja kwa nane tu kwani tulikuwa wanane

H) **Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maelezo.**

i) Sikusoma kwa bidii ndiposa sikufaulu katika mtihani ule.

(Anza: Ningalisoma …………………………………………)

ii) Anakuja (andika katika wakati ujao hali timilifu)

I) **Eleza maana ya neno chungu kama lilivyotumiwa katika sentensi zifuatazo.**



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

i) Chungu yule ni mkubwa.
ii) Chungu kile ni kikubwa.

J) **Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo kama vivumishi.**
i) Sote. i) Zote.

K) **Andika nomino mbili kutokana na kitenzi safari.**

L) **Tumia viunganishi mwafaka kuunganisha sentensi hizi ziwe sentensi moja.**
Alikimbia kwa nguvu zake zote. Alishindwa, kulikuwa na mtu mwenye mbio kumliko.

L) **Eleza maana ya matumizi ya "ka" katika sentensi ifuatayo.**
Aliingia ndani, akaoga, akala kisha akalala.

N) **Taja sauti mbili za ving'ong'o**

O) **Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.**
Juma ameinjika chungu mekoni.

P) **Andika sentensi ifuatayo katika wingi wa udogo.**
Mtu/ mchoyo hamfai mwingine kwa vyovyote vile.

Q) **Kanusha sentensi hii;-**
Ukionana naye mwambie aje anione.

R) **Eleza na udhibitishe kwa mfano, matumizi mawili ya tu.**

S) **Changanua sentensi ifuaatayo kwa kielelezo visandu.**
Mwanafunzi aliyeleta kitabu chake amepongezwa

T) **Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo**
Soroveya atapima wanunuzi viwanja.

U) **Nomino zifuatazo ni za ngeli gani?**
i) Insi … ii) Soksi

5 **MATUMIZI YA LUGHA**

a) **Kamilisha kwa mnyambuliko sahihi.** (alama 1)

kitoto kichanga kilipo………….. kilichangamka sana (oga).

b) Majina mengi katika ngeli ya U-ZI huchukua kiambishi U katika umoja lakini viambishi tofauti katika wingi.

Andika majina matano ukionyesha viambishi hivyo tofauti katika umoja na wingi.

(alama 2 ½ )

c) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo: (alama 2)

Chakula chote kitaharibika.

Chakula chochote kitaharibika.

d) Zifuatazo ni amri gani za konsonanti na hutamkiwa mahali gani? (alama 2) (i) /h/

(ii) /r/

e) Sahihisha sentensi: (alama 2)

Mama mwenye alikufa amezikwa katika kaburini.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

f) Ainisha sentensi ifutayo kwa mfumo wa mstari (alama 3 ½ )

Ng'ombe waliovamia shamba letu wamesababisha uharibifu mkubwa.

g) Sentensi hizi ni za aina gani? alama 2) (i)

Mkulima aliyekata rufani atasaidiwa kesho.

(ii) Walimu na wazazi wanatengeneza bweni.

h) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa. (alama 2) (i)

Ngome ya wanajeshi ilifanyiwa ukarabati.(Andika katika hali ya mazoea).

(ii) Gali hili lapendeza. ( tumia kivumishi kisisitizi).

i) Bainisha virai nomino, virai vivumishi kisisifizi katika sentensi ifuatayo:(alama 3)

Yule mwalimu mwenye ndevu amewasili ukumbini sasa hivi.

j) Kanusha sentensi ifuatayo: alama 1)

Wao wangeniazima kalamu tungemaliza kazi kwa wakati.

k) Tunga sentensi kwa kutumia 'msemo kuwa' mauza'ili kutoa maana sahihi.(alama

l) Kamilisha methali ifuatayo (alama 1)

Kuku akiacha wana………………………………………

m) Andika kinyume cha: (alama 2)

Benati yule alifanya kazi polepole.

n) Tofautisha vitate vifuatavyo kwa kuvitungia sentensi moja (alama 2)

Kucha na kuja.

o) Andika udogo na ukubwa wa neno; Mwana. (alama 2)

p) Andika visawe vya maneno haya: (alama 2)

(i) Mwehu-

(ii) Mahuluku-

q) Bainisha shamirisho kipozi na shamisisho kitondo katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Onyango alimnunulia simu mpenzi wake.

r) Andika katika msemo halisi. (alama 2)

Maina alisema kwamba njiani kulikuwa kumenyesha sana ndio sababu walichelewa.

s) Eleza matumizi ya vile katika sentensi hii: (alama 1)

Vile vile seremala alitengeneza meza.

t)(i) Jumla ya ishirini huitwa…………………………….. (alama 1)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) Jumla ya miaka kumi huitwa …………………………….. (alama 1)

u) Chea cha mtu afanyaye kazi katika maktaba huitwa…………………..(alama 1)

**6.Matumizi ya lugha**

(a) **Akifisha** kifungu kifuatacho

mimi naona ni kazi ngumu nilimjibu si kazi ngumu ni mboga tu aliniambia huku akiniangalia kwa jicho la kunirai ( alama 4)

(b) **Sahihisha** sentensi zifuatazo:

(i) Kikombe ya mwalimu yetu ambacho kilichovunjika kilikuwa ndani ya kabatini. (alama 2)

(ii) Mgeni alikodisha chumba cha kulala baada ya kuburudika na muziki. (alama 1)

(c) **Eleza** maana ya sentensi hizi:

(i) Alitukimbia kabisa. ( alama 1)

(ii) Alitukimbilia kabisa (alama 1)

(d) **Andika** katika usemi wa taarifa.

"Rejelea maelezo katika kitabu ili kuhakiki majibu yako." Mwalimu alimwambia mwanafunzi. (alama 2)

(e) **Tumia** nomino zifuatazo katika sentensi kama vivumishi.

(i) mlevi (alama 2)

(ii) huru (alama 2)

(f) **Onyesha** fungu nomino na fungu tenzi katika sentensi ifuatayo:

Anapenda kusoma gazeti lenye maswala ya kijamii. (alama 2)

(g) Majina yafuatayo hupatikana katika ngeli gani?

(i) Chumvi (alama 1)

(ii) Nyama (alama 1)

(h) **Onyesha** silabi inayawekwa shadda kwenye maneno haya:

(i) Karatasi (alama 1)

(ii) Samahani (alama 1)

(i) **Onyesha** chagizo na yambwa katika sentensi ifuatayo:



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Mwanafunzi amesoma kitabu vizuri sana. (alama 1)

(j) **Tumia** –amba katika sentensi hii:

Ua limealo huwa limetiwa mbolea. ( alama 1)

(k) **Andika** sentensi zifuatazo kulingana na maagizo:

(i) Barmasai huzungumza kilatini vizuri sana.(Tumia wakati usiodhihirika).(alama 1)

(ii) Mtoto huyu hula chakula kingi sana. ( Kanusha katika hali ya ukubwa)(alama 1)

(l) **Unda** nomino kutokana na vitenzi hivi:

(i) Hakiki (alama 1)

(ii) Subiri (alama 1)

(iii) Sajili (alama 1)

(m) **Andika** sentensi ifuatayo katika wingi hali ya kukubali

Mgonjwa hasemi hajanywa dawa. ( alama 2)

(n) **Tambua** aina za maneno katika sentensi ifuatayo:

Walicheka sana walipoambiwa hadithi hiyo. (alama 2)

(o) **Tunga** sentensi ukitumia semi zifuatazo:

(i) Kula uhondo (alama 2)

(ii) Regea parafujo za mwili (alama 2)

(p) Tumia neno "mpaka" katika sentensi kueleza dhana ya:

(i) Wakati (alama 1)

(ii) Mahali (alama 1)

(iii) Kiwango (alama1)

(q) Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha pekee 'o-ote' katika ngeli ya u-u (alama 1)

## 7. MATUMIZI YA LUGHA

a) **Unda nomino kutokana na utenzi.** (alama 1)

i) Chelewa

ii) Andika

b) **Neno 'huyu' limetumikaje (kumaanisha nini katika sentensi hizi)** alama 2)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(i) <u>Huyu</u> amekuja kwangu

(ii) Mgeni <u>huyu</u> amekuja kwangu

c) **Tambua aina ya vishazi katika sentensi ifuatayo.** (alama 1)

Wanafunzi wanasoma darasani

d) **Tunga sentensi ukitumia kielezi cha**

(i) namna/jinsi. (alama 1)

(ii) Idadi. (alama 1)

e) **Yakinisha sentensi ifuatayo.** (alama 1)

Usipomsamehe nduguyo hutasamehewa.

f) **Kanusha sentensui ifuatayo.** (alama 1)

Mlevi alitembea kiholela halafu akaanguka chini pa!

g) **Tunga sentensi tatu zitakazoonyesha matumizi haya matatu ya 'ki'.**(alama 3)

i) Kwonyesha wakati wa masharti

ii) Kiambishi cha ngeli

iii) Kuonyesha mahali

h) **Andika katika usemi wa taarifa.** **(**Alama 3)

"Karibu Bakari, tafadhali kaa', Juma akasema.

" Asante, Je, habari za nyumbani?" Bakari aliuliza

i) **Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi; kisha eleza ni vielezi vya aina gani.**

i) Alilala jioni. (alama 1)

ii) Mchezaji huyu ni hodari sana. (alama 1)

j) **Tumia kielelezo cha jedwali kuchanganua sentensi.** (alama 3)

Kandanda inapendwa na watu wengi sana.

k) **Andika udogo wa sentensi zifuatazo**

i) Sahani zetu ni nzuri kuliko zao. (alama 2)

ii) Njia hii inaelekea kule mlimani. (alama 2)

l) **Akifisha sentensi ifuatayo.** (alama 2)

nilimkuta mkuu wa wilaya ya fahari akisoma kitabu kiitwacho utubora mkulima.

m) **Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya vitenzi vifuatavyo katika jinsi ya kufanyiwa.**

(alama 3)

i) -ja



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

ii) -cha

iii) -Nywa

n) **Andika methali zinazowakilisha maadili yafuatayo.** (alama 4)

(i) Mvi ni dalili ya busara

(ii) Kushika hatamu huleta adha nyingi.

o) **Andika kinyume cha;** (alama 1)

walizama walipokuwa wakikusanya mchanga

p) **Eleza maana ya misemo ifuatayo.** (alama 4)

i) Msumari wa moto juu ya kidonda

ii) Giza la ukata

q) **Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu tofauti.** (alama 3)

Hapo ndimo alikofia

## **8.**<u>MATUMIZI YA LUGHA:</u> **( ALAMA 40)**

(a) **Ziandike** sentensi zifuatazo ukitumia kiwakilishi cha pekee o-ote. (alama 2)

(i) Ufunguo wowote ufunguao ni wetu.

(ii) Ngozi zozote zirarukazo ni za kifaru.

(b) Taja sauti zozote nne zinazotamkiwa katika ufizi. (alama 2)

(c) **Andika** sentensi inayoonyesha 'ki' ya masharti. (alama 1)

(d) **Onyesha** viambishi awali na tamati katika kitenzi: Alimkemea. (alama 1)

(e) **Bainisha** matumizi ya 'ni' katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Ondokeni.

(ii) Kiptoo ni mwizi sugu

(f) **Eleza** maana nne zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

(i) Alimpigia simu

(g) **Changanua** sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (alama 3)

(i) Vile vingali vikitengenezwa

(h) **Akifisha** sentensi ifuatayo. (alama 3)

(i) puka chaka hata wewe siamini.

(i) **Eleza** tofauti kati ya sentensi hizi mbili. (alama 2)

(i) Ungesoma kwa bidii ungepasi mtihani.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) Ungalisoma kwa bidii ungalipasi mtihani.

(j) **Andika** sentensi moja kwa kutumia 'licha ya'. (alama 2)

(k) Andika ukubwa na udogo wa neno rununu. (alama 1)

(i) Ukubwa ………………………………………………………………………………

(ii) Udogo ………………………………………………………………………………

(l) **Andika** sentensi zifuatazo kwa wingi. (alama 3)

(i) Domo limepinduliwa.

(ii) Kiwiko kimejigonga ukutani.

(iii)Ukimwi umeangamiza wengi duniani.

(m) **Unda** vivumishi kutokana na maneno yafuatayo. (alama 2)

(i) Imani

(ii) Ubora

(n) **Nyambua** vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendesha. (alama 2)

(i) – nya ………………………………………………………………………………

(ii) - cha ………………………………………………………………………………

(o) **Taja** maana mbili ya neno 'mjomba'. (alama 2)

(p) **Andika** sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Ala! Huna heshima wewe mtoto!"

Mama alimkaripia bintiye

(q) **Kamilisha** methali zifuatazo. (alama 2)

(i) Ukuni juu ya uchaga ..................................................................

(ii) Simbiko haisimbuki ila ..............................................................

(r) **Eleza** maana ya misemo ifuatayo. (alama 3)

(i) Msumari wa moto juu ya kidonda.

(ii) Pasulia mbarika.



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(iii)Giza la ukata.

(s) **Onyesha** kirai nomino, kirai kivumishi na kirai kielezi katika sentensi. (alama 3)

(i) Bawabu mzuri huandika ripoti ndefu mara kwa mara.

**9. MATUMIZI YA LUGHA**

**a) Akifisha**

Sikukuu ya madaraka nilikwenda eldama ravine kumwona yohana naye akasema atakuja kuniona pamoja na mkewe mariamu siku ya jumapili. Alama 3

b) **Andika katika usemi wa taarifa**

"Hivi vibanda vinatumiwa kulanguzia dawa za kulevya'', mkuu wa polisi alilalamika. Alama 2

c) **Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo pamoja na kivumishi – ingine Alama 2**

i) dau

ii) Urembo

d) **Tumia mchoro wa matawi kuichanganua sentensi ifuatayo.**

Mwanafunzi mzuri ametunukiwa zawadi. ( alama 3)

e) **Tumia <u>amba</u> katika sentensi hii.** Alama 1

Ua limealo huwa limetiwa mbolea.

f) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi. Alama 2

i) fisidi

ii) dhihaki

g) **Pigia mstari vielezi katika sentensi hizi kisha utambue ni vya aina gani.** Alama 4

i) Wezi walipigwa barabara

ii) Wezi walipigwa kwa bunduki

(h) **Tunga sentensi tatu tofauti zinazodhihirisha matumizi ya <u>Ka</u>.** (Alama 3)

**i) Kanusha**

Angelijua hasira yangu, angelifuata amri zangu. Alama 2

(j) **Tunga sentensi kwa kila mojawapo ya miundo hii.** Alama 2

i) Kishazi huru

ii) Kishazi tegemezi

k) **Sahihisha** Alama 2

i) Alikuja kunipea pesa zangu

ii) Umemwona mwenye ameenda sokoni

(l) **Tunga sentensi kutofautisha jozi hizi kimaana.** Alama 2

i) Kua

ii) Kuwa

m) **Sentensi sahili ni sentensi ya aina gani? Tunga sentensi kudhibitisha maana.** Alama 2

Maelezo ..............................................................................................................................

Sentensi

n) Andika kitenzi hiki katika kauli ya kutendeka Alama 1

La

o) **Tunga sentensi ukitumia misemo hii** Alama 2

(i) Fanya kikaka

(ii) Jia kikuku

p) **Tumia kiunganishi hiki katika sentensi.** Alama 1

Japo



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

q. **Andika udogo na ukubwa wa nomino - <u>ng'ombe</u>** Alama 2
r. **Andika visawe vya.** Alama 2
Masaibu
i) Kiwewe
s) **Tunga sentensi moja ukitumia kihusishi cha - a** Alama 1
t) **Kamilisha methali** Alama 1
Mti mkuu ukigwa

**10.MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) **Akifisha sentensi ifuatayo**

je utakuja kwetu siku ya alhamisi. (alama 2)

b) **Onyesha kundi Nomino (KN) na kundi Tenzi (KT) katika sentensi zifuatazo**(alama 4)

(i) Filamu hiyo nzuri ilivutia

ii) Mtoto ataimba vizuri

c) **Andika sentensi zifuatazo ukizingatia maagizo uliyopewa katika mabano:-(**alama 2)

Magari yote yalitiwa vidhibiti mwendo (mazoea)

(ii) Alichora akatuzwa (ngali ya masharti)

d) **Tofautisha sentensi zifuatazo kimaana kwa kuongozwa na vivumishi vilivyopigiwa mistari:**

(alama 2)

(i) Mtoto <u>mwenyewe</u> ndiye huyu

(ii) <u>Mwenye</u> mtoto ndiye huyu.

(e ) **Bainisha viambishi awali na tamati katika sentensi ifuatayo** (alama 2)

Walipigiana

(f ) **Tunga sentensi kwa kutumia viunganishi vifuatavyo:-** (alama 4)

Jinsi

ii) Sembuse

**Kwa kuzingatia upatanishi wa Kisarufi ufaao, tunga sentensi sahihi ukitumia**

**nomino zifuatazao.** ( alama 4)

Ulezi

Mate

h) **Andika sentensi hizi tena bila kutumia kirejeshi "amba''**

(i) Mtahiniwa ambaye husoma kwa bidii ndiye ambaye hufaulu mtihani wake

Vizuri (alama 2)

(ii) Mtahiniwa ambaye amefaulu vizuri mtihani wake hujiunga na chuo kikuu(alama 2)

**(i) Tambua aina za vielezi vilivyotumika katika sentensi zifuatazo.**



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(i) Nilipomdai pesa zangu alinijibu kimzahazaha (alama 1)

(ii) Wanafunzi wanacheza uwanjani (alama 1)

j) **Ichanganue sentensi hii kwa njia ya vitawi**

Mama alimpikia mtoto uji kwa sufuria. (alama 4)

k) **Kwa kutumia maneno machache, eleza tofauti iliyoko katika sentensi zifuatazo.**

Alichekelewa alipofika

Alichekesha alipofika

Alichekelea alipofika (alama 3)

**l) Geuza usemi huu uwe wa taarifa:**

" Sikubaliani nawe unaposema mambo haya ni ya kweli". Msemaji mmoja akamwambia mwingine. (alama 2)

m) **Tunga sentensi <u>tatu</u> kulingana na maagizo haya:**

(i) Sentensi sahili (alama 1)

(ii) Sentensi ambatano (alama 1)

(iii) Sentensi ya changamano (alama 1)

n) **Tambua aina za vishazi vilivyotumika katika sentensi hizi zifuatazo**

Juma aliyecheza vizuri alituzwa vyema (alama 2)

## 11. MATUMIZI YA LUGHA

Konsonanti hizi zinatamkiwa wapi? ( alama 3)

n ………………………………………………………………………………………

k ………………………………………………………………………………………

p ………………………………………………………………………………………

**Tambulisha** aina za vielezi vya namna katika sentensi zifuatazo (alama 2)

Nyanya hutembea kwa mkongojo

Mwalimu alimkemea kijeshi

**Eleza** matumizi ya kiambishi 'ji' katika sentensi zifuatazo

Mtoto ame<u>ji</u>kata kidole.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Yeye ni mchoraji.

**Ainisha** sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (alama 5)

Wao watarudi mapema lakini mimi nitabaki.

**Kanusha** sentensi ifuatayo (alama 2)

Huyu ndiye nimtakaye

**Bainisha** virai na utaje ni vya aina gani (alama 3)

Atapona baada ya juma moja.

Alimnyemelea kwa woga

**Andika** sentensi zifuatazo katika hali ya udogo. (alama 2)

Chungu changu kimevunjika.

Ng'ombe wangu ana ndama mkubwa.

**Andika** katika kauli ya kutendeshea. (alama 1)

Kwa nini unamfanya mtoto wake kulia?

**Ainisha** mofimu za sentensi ifuatayo. (alama 3)

Alimlia

**Badilisha** maneno yaliyopigiwa mstari yawe katika hali iliyopigiwa mstari. (alama 2)

Alimtia <u>hasira</u> alipotoa uamuzi huo. (kitenzi)

Kazi hii imefanywa kwa ustadi. (kielezi)

**Andika** katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Sisi tunapenda mchezo wa soka," Otieno alisema

**Bainisha** yambwa kitondo na yambwa kipozi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

Rama aliwapikia wageni wake chakula kitamu.

**Akifisha**. (alama 2)

Riwaya ya siku njema imesomwa na wengi.

**Andika** katika ukubwa. (alama 1)

Nguo zake zimeloa maji.

**Akifisha** sentensi ifuatayo kwa njia tatu kuleta maana tatu tofauti. (alama 3)

Mashaka akasema amempata.

Tumia 'A' unganifu katika sentens kudhihirisha matumizi ya: (alama 2)

Kivumishi

Kiwakilishi



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

**Andika** katika wingi (alama 1)

Baka lililoko kipajini linatisha.

Ni hisia zipi zinazodhihirika katika matumizi haya ya vihusishi?

Maskini! Alianguka mtihani wa kitaifa.

Mashala! Mtoto huyu ameuubwa akaumbika.

## 12. MATUMIZI YA LUGHA.

a) **Onyesha kitenzi kikuu na kisaidizi katika sentensi hii.**

Nimewahi kumkumbusha makosa yake. (al 2)

b) Umepewa aina tofauti za nomino. Tunga sentensi idhihirishayo kila aina ya nomino; (al 3)

Nomino ya wingi

Nomino ya kitenzi jina

Nomino ya kipekee

c) **Tunga sentensi kutofautisha maneno haya.** (al 2)

(i) Dhamini

(ii) Thamini

d) **Tunga sentensi kuonyesha matumzi ya viakifishi hivi.**

(i) Alama hisi (al 1)

(ii) Parandesi (Al 1)

(iii) Alama za mtajo / usemi (Al 1)

e) Andika konsonanti mbili zinazotamkiwa kwenye ufizi. (al 2)

f) Eleza maana ya msemo huu.

Maisha ya kitwea (al 2)

g) Geuza vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli ya kutendeana, kisha uvitungie sentensi.

(i) Ja (al 2)

Pa. (al 2)

h) Eleza maana mbili ya "La" (Al 2)

(i) Unda vitenzi viwili kutokana na kila moja ya majina

Mtukufu (Al 1)

Mchumba (Al 1)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

j) Tumia – ndi- pamoja na viashiria vya ngeli kujaza pengo (Al 2)

(i) Wewe ninayekufuta.

(ii) Nyingi mnaoongoza.

k) Andika kinyume cha;

(i) Tandaza zulia kubwa (Al 1)

(ii)Mtweke mchukuzi mzigo huu. (Al 1)

l) Vitaje vipashio vitatu muhimu vya lugha. (Al 3)

m) Andika kwa msemo wa taarifa (Al 3)

"Lo! Umeweza kuubeba mzigo huu pekeyo?"

Mama alishangaa.

n) Tumia "O" rejeshi katika sentensi zifuatazo (al 2)

(i) Mikeka ambayo hufumwa Turkana ni madhubuti.

Uchunguzi ambao wangojewa umewadia.

o) Eleza matumizi ya "KU" katika sentensi hii.

Kucheza huku hakufai (AL 2)

p) Tofautisha nyakati (Al 2)

(i) Akimbia

(ii) Anakimbia

q) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii (Al 2)

Anamolala mna viroboto wengi.

## 13.MATUMIZI YA LUGHA

(a) Andika kwa kinyume:

(i) Nje kulikuwa kweupe. (alama 1)

(ii) Mzizimo (alama 1)

(b) Eleza matumizi ya "po" katika sentensi hizi.

(i) Mjomba aliniuliza "Je, sikukuambia kuwa akomeleapo mwenyeji nawe mgeni koma papo? (alama 2)

(ii) Eleza matumizi ya "kwa" katika sentensi hii:

Mwanariadha alijikaza kisabuni tulipomshangilia kwa nguvu. (alama 1)

(c) Akifisha sentensi zifuatazo:

(i) lahaula sijui kama kazi hii itamalizika (alama 2)

(ii) siku ya jumapili mwezi wa aprili mwaka huu tutaenda mombasa (alama 1)

(d) Eleza maana ya misemo hii :



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(i) Kulia ngoa. (alama 2)
(ii) Kuwa mjango. (alama 3)

(e) Kamilisha methali hii:
(i) Atupaye tope ____________________________________________(alama 4)
(ii) Cha mkufuu mwanafuu ha, na akila hu, ________________________(alama 5)

(f) Tumia kivumishi kwenye vifungo kukamilisha sentensi:
(i) Tuleteeni ng'ombe yeyote _________________________ (-dogo) (alama 1)
(ii) Ngoma ________________________, ndiyo iliyotakikana. (-le) (alama 1)

(g) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo uliyopewa:
(i) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ikiwa unatumia msumeno. (Anza: "Ni rahisi … ) (alama 2)
(ii) "Kuna chai?" Mtoto aliuliza. Maliza na …. Chai) (alama 2)
(iii) Tabasamu yake ilipotea haraka alipoambiwa kuwa alipatikana na hatia ya kuwa mlevi na kukosa adabu. (Anza Aliishiwa na ….) (alama 2)

(h) Geuza sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea:
(i) Mtoto unavyomlea ndivyo anavyokuwa. (alama 2)
(ii) Matunda yanayoiva ndiyo yanayotundwa. (alama 2)

(i) (a) Mke wa mwanao utamwitaje? (alama 1)
(b) Yohana na Selemani ni ndugu, pia wataitanaje? (alama 1)
(c) Msichana ambaye hajavunja ungo huitwaje? (alama 1)

(j) Eleza muundo/mpangilio wa sentensi hii:
Amenikasirisha (alama 3)

(k) Tumia maneno haya katika sentensi.
(a) Hapiki hapakui. (alama 2)
(b) Hana kazi hana bazi.

(l) Tumia amba katika sentensi hii.
Mtoto anayelia amepigwa na mwizi vibaya sana. (alama 1)

## 14.

(a) Akifisha kifungu kifuatacho

"Baba Wafua, ona barua iliyotoka kwa mwanao. Hata hati haisomeki" "Lo" baba watoto akamaka. Hii barua kweli imetoka kwa mwanangu Wafua. "Waniuliza mimi?" mama akamjibu "Tazama maandishi na anwani basi. Shule ya Msingi ya Burungani S.L.P 128

Vuga" (alama 5)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(b) (i) Andika sentensi ifutayo kwa wingi

Uwanja mwingineo umechimbuliwa kuongezea ule wazamani (alama 1)

(ii) Unda jina kutokana na kivumishi hiki

<u>Refu</u> (alama 1)

(iii) Tunga sentensi moj a ukitumia-ki-yamsahrti (alama 1)

(c) (i) Tunga sentensi tano kuonyesha matumizi matano tofautiyaneno ,

KWA (alama5)

(ii) Tumiaviunganishivifuatavyokatika sentensi

I) Mighairi ya

II) Maadam

(alama 2)

(d) Sentensi ifuatavyo ina maanambilitofauti. Zieleze

Huyu amekuja kutuliza (alama 2)

(e) Tofautisha maana

(i) Ningekuwa na uwezo ningesafiri kwenda ng'ambo

(ii) Ningalikuwanauwezoningalisarikikwendang'ambo (alama2)

(f) Ainisha sehemu zote sarufi katika sentensi ifuatayo

Ninaondoka

(g) Unda jina moja kutokana na majina yoyote mawiliyaKiswahilisanifti (alamal)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

## 15.

(a) SahiWshamakosayaliyomokatika sentensi hizi mbili zifuatazo

(i) Bei za vitu zimepanda juu sana siku hizi

(ii) Weka mizigo kwa gari (alama2)

(b) Elezamaanaya sentensi hizi

(i) mikono yao imeshikana

(ii) mikono yao imeshikamana (alama2)

(c) Andika sentensi zifuatazo ukitumia kinyume cha neon lililoandikwa kwa herufi za mlazo;

(i) Usijaribu *kupaaza* sauti unapoimba (alamal)

(ii) Huyu ni mtu *mwenye busara* (alamal)

(iii) Binadamu hawezi *kumuumbua* mwenzake (alama 1 )

(d) Akifisha kifungu kifioatacho:

Bwana mwenyekiti mgeni wetu wa leo wazazi waalimu wote hata wanafunzi leo ni siku muhimu je mngependa niwafahamishe msaada tuliopokea kutoka kwa wizara ya elimu

(alama 4)

(e) Tunasema: <u>Mtoto huyu mzuri anapendeza</u>

Ukitumia majina yafuatayo kamilisha sentensi ukifuata mfano ulio hapo juu

(i) Ngome (alamal)

(ii) Mitume (alamal)

(iii) Heshima

(iv) Ng'ombe (alamal)

(v) Vilema (alamal)

(h) Kutokana na vitenzi tunaweza kuunda maj ina, na pia kutokana na maj ina tunaweza kuunda vitenzi. Mfano:



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Jina Kiteado

Mwuzaji uza

Muzo uza Wimbo imba

Sasa kamilisha:

Jina Kitendo

(i) Mnada __________

(n) Kikomo __________

(iii) ______ ______ ruhusu

(iv) _____________ ashiki

(v) ____________ husudu (alama5)

(i) Andika katika msemo halisi

Mvulana, alimwambia baba yake kuwa alitaka kwenda sokoni (alama 2)

(n) Andika katika msemo wataarifa

Nitakuwa nikija hapa kila siku kukuona",Kamau alimwambia shangazi yake ' Eleza matumizi ya' Po' katika sentensi hii Nilipofika nilirnwona pale alipokuwa amesimama

(alama 2)

(k) Mtu akicheza mchezo mahali fulani tunaweza kusema alicheza hapo ukifuata mfano huu, tumia vitenzi vilivyoko l^tika mabano lojkamilisha:

(i) Ali __________________________ hapo (la)

(ii) Ali __________________________ hapo (fa)

(iii) Ali __________________________ hapo (oa)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

# 16.

*Jibu maswali yafutayo kulingana na maagizo*

**(a)** ***Andika katika msemo wa taarifa***

Mzazi 'lieshonatokaufikenyumba Mtoto:

"Nitajaribu, lakini mwalimu alisema tutafanya mtihani jioni

(alama4)

**(b)** ***Badiisha katika <u>udogo</u> kisha <u>uukanushe</u> udogo huo***

(i) Guu lake limepona baada ya kuumwa na jibwa la jijini (alama2)

(ii) Nyumba yenyewe ilijengwa bondeni karibu na mto (alama2)

**(c)** ***Andika katika kauli ya kutendesha***

(i) Nataka upike chakula hiki vizuri (alamal)

(ii) Toa ushuru forodhani (alamal)

**(d)** ***Sahihisha bila kubadilisha maana*** **;**

(i) Usikuje hapa kwetu kwani sitakuwamo (alamal)

(ii) Basi la shule limeharibika moshi nyingi inatokea dirishani na maji inatiririka ovyo

(alamal) (e) *Eila kubadilisha maana andika sentensi zifuatazo ukitumia kirejeleo cha ngeli kifaacho*

(i) Nyumba alishinda farasi kukimbia (alamal)

(ii) Milango yote yajifunga ovyo nenda ukafunge (alamal)

(iii) Hamisiamekatanyasivizuri (alamal)

(iv) Jiwe lile liliangukia matunda (alamal)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(f) *Eleza matumizi manne tofautiya* - na - (alama 4) (g) *Eleza maana mbili mbili zinazotakana na sentensi zifuatazo*

(i) Mtoto alitimua mbio, kuona nyoka (alama 2)

(ii) Juma alifagia chakula (alamal)

(iii) sisikii vizuri (alama2)

(h) *Tunga sentensi ya neno moja ambayo ina visehemu vifuatavyo vya sarufi*

-kiima,

-Wakati

-kirejeleo

- Kiwakilishi kitendwa

-Kitenzi (alama 5)

(i) *Bila kunyambua andika maneno mawili ambayo yanatokana na shina moja na neno:*

Imani

# 17.

1. (a) *Akifisha kifungu hiki:*

nilipomwendea aliniangalia kisha akaniambia siamini kuwa ni wewe uliyeandika barua (alama3)

(b) *Onyesha viunganishi vingine badala ya vile vilivyotumiwa katika sentensi hizi:*

Watu wanne walipeperushwajuu kwajuu na upepo mkali (alama 4)

(c) *Tumia viunganishi vingine badataya vile vilivyotumiwa katika sentensi hizi:*

(i) Anayetafuta hachoki hata akichoka keshapata (alama 1)

(ii) Ngojeeni hadi washiriki wote wafike (alama 1)

(d) *Tumia kiulizio –pi-kukamilisha:*

(i) Nimitume........... ........... aliowataja? (alama 1)



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) Ni kiziwi .................... aliyemwona akipita? (alama 1)

(e) *Tunatumia viashiria vya kuthibitisha kwa mfano:-*

Kitabu kiki hiki
*Sasa kamilisha:*

Ni mbwa ................ aliyekula chakula cha mtoto (alama 1)

(f) *Andika upya sentensi ifutayo ukitumia kirejeshi (kihusiano cha ngeli cha mwisho* Mwanafunzi anayefanikiwa maishani ni yule anayesoma kwa bidii na pia anayetii

wakuu wake. (alama 2)

(g) Jaza viambishi vifaavyo katika sentensi zifuatazo:

(i) Ukuta..........enyewe uria hyiifa nyingi lakini fundi....ote anaweza

kuukarabati (alama2)

(ii) Maji yalizoa changarawe....ote na vitu....ingine....o ufuoni mwa bahari

# 18.

A. (a) *Jaza kiambishi kifaacho:*

Ume_______ona kalamu nyekundu zili____potea? (alama 2)

(b) *Andika kwa umoja:*

Tumewaondoleeni matatizo yenu yafaa mtushukuru (alama 2)

(c) Nyambua vitenzi vifiiavyo ili kupata majina (nomino) mawili tofauti:

(i) Kumbuka........................................................

(ii) Shona..............................................................

(m) Cheka...........................................................

(d) *Ondoa* - *amba-bila kubadilisha maana:*

(i) Kuimba ambako kulisifika siku nyingi sasa kunatia shaka (alama 1)

(ii) Mibuni ambayo hupandwa wakati wa mvua hustawi (alama 1)



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

(e) Sahihisha:

Siku hizi mahitaji imezidi na pesa haitoshi (alama 1)

(f) Akifisha:

Sijaona kitabu kizuri kama hiki utaniazima siku ngapi Bashiri alimwuliza Sijaona

(alama4)

(g) *Eleza maana mbili za sentenzi:*

Jua nisemalo ni muhimu kwetu (alama2)

(h) Kiambishi-U-hutambulisha majinayangeliyaU (umoja), Hatahivyobaadhiya majina haya huchukua viambishi tofauti katika wingi. Orodhesha maj ina matano kama hayo, kisha . uonyeshe viambishi hivyo tofauti vya ngeli (katika umoja na wingi) (alama 5)

# ISIMUJAMII

1. Eleza juhudi tano zinazotumika kukiendeleza Kiswahili

2.` (a) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha wa maabadini

(b) Matumizi ya lugha yoyote ile huthibitiwa na mambo fulani. Fafanua **matano** kati ya hayo

3. **AZIZ** : Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao kenyatta, railways!
**SHIKU** : Namba nane ngapi?
**AZIZ** : Mbao ingia, blue.
**SHIKU** : Nina hashuu.
**AZIZ** : Blue Auntie.
**SHIKU** : Sina.
**AZIZ** **:** Ingia. 46 Adams mbao, kenyatta railways gari bebabeba.
**AHENDERA** : Mimi sinako shirini. Chukuako tu kumi.
**AZIZ** : Dinga inakunywanga petrol mzee.
**AHENDERA**: Kumi mingi.
**AZIZ** : Haaya ingia twende. Driver imeshon twende.

**Maswali**
(i) Eleza muktadha wa mazungumzo haya
(ii) Taja sifa **sita** za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

4. ***Kifuatacho ni kifungu kifupi cha mazungumzo. Kisome kisha ujibu maswali yaliyoulizwa:-***

Mzee Oluoch : ....................................................................ni kweli hayo!

Mzee Mwenda : Ndio. Huyu mtoto wangu nimemsomesha mpaka akahitimu chuo kikuu na anafanya kazi ya uhasibu.

Mzee Oluoch : Na wangu amehitimu na sasa ana shahada ya uzamili. Yeye ni mhandisi mkuu. Chukua tu mbuzi hamsini na utukubalie kujenga uhusiano wa ukwe.

Mzee Mwenda : Je, mbuzi hao ni wa 'mfuko' au ni .......?

Mzee Oluoch : Kuna wa mfuko ......thelathini na hao wengine ishirini.

Mzee Mwenda : Basi lete hao ulio nao. Wengine hamsini watabaki deni. Utakuwa ukinilipa polepole. Idhini yangu nimetoa ili mipango iendelee.

(a) Mazungumzo ya aina hii hutokea katika muktadha wa aina gani?

(b) Eleza sifa **nane** za lugha inayotumika katika wa aina hii

5. **ISIMUJAMII**

Bwana mwenyezi, muumba wa ardhi na mbingu, twaja mbele yako asubuhi hii kukuomba uendelee kutulinda na kutumiminia kila kilicho chema. Bariki ibada ya leo na sheshe ya sindikiza ya kina mama tutakayokuwa nayo alasiri. Ninaomba haya machache kwa jina la yesu Kristo mkombozi wetu, Amina.

(a) Taja muktadha wa makala haya. (alama 2)

(b) Taja sifa zozote tatu za sajili hii zinazojitokeza katika makala haya.(alama 3)

(c) Taja sifa zingine za lugha ambazo hazikuhusishwa katika makala haya kwa mujibu wa sajili hii.

## 6. ISIMU JAMII

**Ponda mali:** Karibu! Wamama wang'are mali safi ambayo huwezi kupata popote duniani.

**Amina**: Unauzaje hilo rinda?

**Ponda mali**: Bei ni kusikilizana, hatuwezi kukosana.

**Amina**: Nitakupaa shilling hamsini, naona ni mtumba.

**Ponda mali**: Mama hilo rinda ni original kutoka Marekani kwa meli.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

**Amina**: Nitaongeza shilingi kumi basi.

**Ponda mali**: Ongeza kidogo, usiniue.

(a) (i) Hii ni sajili gani? (alama 1)

(ii) **Eleza** sifa za sajili uliyotaja hapo juu (alama 4)

(b) **Eleza** sifa zozote tano za sajili ya kidini. (alama 5)

**7. ISIMU JAMII**

"Semeni Amen. Na ndugu atamsaliti mtoto na watoto wataondoka juu ya wazazi wao na kuwafisha. Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka".

**Maswali**

a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. ( alama 2)

b) Fafanua sifa ya lugha iliyotumika katika mazungumzo haya. ( alama 5 )

c)Eleza sababu zinazofanya mazungumzo yanayotokea katika mazingira mbalimbali kuwa na sifa tofauti tofauti za kimatumizi ya lugha. ( alama 3 )

## 8.ISIMUJAMII (ALAMA 10)

***Soma nakala hii kasha jibu maswali***

"Ni ya leo mama ni ya leo.Ni ya leo baba ni ya leo. Bidii yako ndiyo bahati yako.Tishati na hamsa, shati arubaini........Mali kutoka ng'ambo; chagua ufungiwe. Ni ya leo, ni ya leo............."

**MASWALI**

(a) **Taja** mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika makala haya. (alama 4)

(b) Huku ukirejelea makala, **pambanua** watumizi na mahali pa matumizi. (alama 2)

(c) **Taja** sifa za lugha inayopatikana katika sajili hii. (alama 4)

9. **ISIMU JAMII**

**Mahojiani baina ya daktari na mgonjwa.**



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Daktari: Karibu ndani.
Mgonjwa: Ahsante.
Daktari: Unaitwa nani baba?
Mgonjwa: Naitwa Ali Makame.
Daktari: Unaishi wapi?
Mgonjwa: Ninaishi mtaa wa Majitu
Daktari: Una shida gani baba?
Mgonjwa: Mimi ninahisi baridi sana. Hata wakati ambapo jua linawaka, mimi huhisi baridi na kutetemeka.
Daktari: (Anachukua kipima joto na kukiingiza kwenye kwapa la mgonjwa) Hali hii ilianza lini?
Mgonjwa: Tangu juzi.
Daktari: Ni jambo gani linalokusumbua.
Mgonjwa: Naumwa na kifua bwana tabibu
Daktari: Je, baba unatumia sigara?
Mgonjwa: Nilikuwa nikivuta, lakini sasa nimeacha
Daktari: Unakohoa?
Mgojwa: Awali nilikuwa nikikohoa vibaya sana lakini sasa kikohozi kimepungua
Daktari: (Akiangalia kipima joto) Ala! Una joto jingi sana.
Mgonjwa: Nami huku naumia kwa baridi kali kabisa.
Daktari: Hebu tupime kifua chako (Anatoa stethoskopu shingoni na kudunga masikioni kisha anamwekea mgonjwa mgongoni). Vuta pumzi ndani! Vuta tena. Basi toa pumzi nje. Basi kifua chako si kizuri sana. Itakubidi uchukuliwe picha ya eksirei (uyoka). Ninataka upimwe katika maabara kama una viini vinavyosababisha malaria.
Mgonjwa: Ninachotaka bwana mganga ni kupona tu.
Daktari: Utapona. Usiwe na wasi wasi (Anaita mwuguzi). Nitakudunga sindano moja ya kuteremsha hicho kiwango chako cha joto. Kisha nenda ukapewe dawa nilizokuandikia.
Mwuguzi: Nimefika daktari.
Daktari: Mchukue huyu mgonjwa umpeleke katika maabara apimwe malaria, baadaye achukuliwe picha ya eksirei.

**Jibu maswali haya**

a) Jadili sifa za lugha inayotumiwa. Alama 6

b) **Eleza maana ya vifaa vifuatavyo ambavyo hutumika katika mazingira ya hospitali** Alama 4

(i) Uyoka
(ii) Kipima joto
(iii) Machela
(iv) Mwuguzi

10.. **Yasome mazungumzo haya kisha ujibu maswali yafuatiayo**

- MPOTEVU: Nataka pande za Kaya. Hapa Mkanyageni nimejaribu kutafuta rafiki wa kufaa, nimekosa. Sasa nakaa kule mji wa Kale katika bweni la wageni.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

KUPE: Lahaula! Umeshampata mwenyeji atakayekutimizia haja zako zote

MPOTEVU: Ni yupi huyo?

KUPE: Kutafuniwa umeshatafuniwa; kulikobaki ni kumeza tu

MPOTEVU: Mbona sikuelewi?

KUPE: (Akijongeza kiti chake karibu) Basi tuyaache hayo.
Kwani hasa umeletwa na shughuli gani huku kwetu?

MPOTEVU: Oh! Ni kama kufanyafanya biashara na kutalii kidogo ili kutazama ulimwengu wa Walimwengu

a) Mbinu ya majina iliyotumiwa yatosha kufasri mada. Jadili. (alama 3)

b) "Lahaula! Umeshampata mwenyeji atakayekutimizia haja zako zote"
Ni mwenyeji gani anayezungumziwa hapa? (alama 2)

c) Hebu tegua kitendawili kilichomo:"Kutafuniwa umeshatafuniwa; kulikobaki ni kumeza tu. (alama 2)

(d) Taja sajili ya mazungumzo haya (alama 1)

(e) Zitaje sifa mbili za sajili hii. (alama 2)

# 11.<u>ISIMU JAMII</u>

***<u>Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.</u>***

**Kijana**: Mama unakwenda?

**Mama**: Kwenda wapi?

**Kijana**: Ala, wapi kwingine ila mjini?

**Mama**: Siendi.

**Kijana**: Haya basi. Dere wacha mioto! Beba mmoja, kwako! Dada njoo, usisafirie mtumba…. Nafasi ya mtu mmoja, Commercial….. usiachwe, gari ni ishirni tu…… bei ya chini kuliko mkate.

**Dada**: Nina ashu, utanibeba?

**Kijana**: Ah, dada! Ongeza dada, tayari nimekupunguzia kwa kukwambia mbao. Kawaida huwa ni finje

**Dereva**: Auntie anasema nini?

**Kijana**: Ananyonga ashuu.

**Dereva**: Basi mbebe sare.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

**Kijana**: Dada dere amekulipia. Basi dere gari iko seti, stage ya kwanza jijini.

## Maswali

(i) Mazungumzo haya hutokea katika muktadha gani? (alama 1)

(ii) Toa ushahidi. (alama 3)

**Eleza** sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu mbali na ulizotaja katika (a) (ii) hapo juu. (alama 6)

## 12.ISIMU JAMII

Wananchi huoyee! Kiti juu!

Leo ni ile siku tuliyoingojea kwa hamu na ghamu. Imefika, haijafika? Naona nyuso zenu zinatangaza ushindi wa kiti.Naona hamjadanganywa na mpinzani wangu atembeaye na kupaka matope jina langu. Ni nani hajaona maendeleo niliyoleta hapa tangu mnichague nyinyi wenyewe? Kwa hiari yenu mlinichagua niwe mtumishi wenu nami niko chini ya nyayo zenu. Sasa huu ni wakati mwingine naomba, nawasihi, nawanyenyekea mnikabidhi tena hilo jukumu zito la kuwatumikia.

Mpinzani anawapa pesa kuwahonga, ela nasema kula kwa mpinzani wangu, lakini kura ni kwangu jamani. Kiti juu!

**Maswali**

A Taja muktadha wa matumizi ya lugha hii (Al 2)

B Eleza sifa za lugha hii . (Al 4)

C Jadili mbinu za lugha zilizotumika katika lugha hii . (Al 4)



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

# USHAIRI

1. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-***

**CHEMA HAKIDUMU**

Chema hakidumu, kingapendekeza,
Saa **ikitimu**, kitakuteleza,
Ukawa na hamu, kukingojeleza,
Huwa ni vigumu, kamwe hutaweza.

Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,
Japo mara tumbi, kinshaniliza,
Na japo siombi, kipate n'ongeza,
Mtu haniambi, pa kujilimbikiza.

Chema mara ngapi, kinaniondoka,
Mwahanga yu wapi? Hakukaa mwaka,
Kwa muda mfupi, aliwatilika,
Ningefanya lipi, ela kumzika?

Chema wangu babu, kibwana Bashee,
Alojipa tabu, kwamba anilee,
Na yakwe sababu, ni **nitengenee**,
Ilahi wahhabu, mara amtwee.

Chema wangu poni, kipenzi nyanyangu,
Hadi siku hini, Yu moyoni mwangu,
Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu,
**Ningamtamani**, hatarudi kwangu.

**Maswali**

(a) Eleza dhamira ya mwandishi
(b) Fafanua umbo la shairi hili
(c) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari
(d) Taja na kutoa mfano mmoja wa tamathali yoyote ya lugha inayojitokeza katika shairi
(e) Taja mbinu nne za uhuru wa mshairi huku ukitolea kila mbinu mfano

(f) **Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na vile yalivyotumika**:-
(i) Nitengenee
(ii) Ningamtamani



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

(iii) Ikitimu

2. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-***

1. Ni sumu, sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako zako leweshi
Za kupanda ngazi
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa wazazi

2. Ni sumu, sumu hasiri
Unahasiri watoto
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

3. Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi
Ya daima kunywa 'moja baridi'
Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klabu
Hadi saa nane usiku
Huku yakijenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

4. Ni sumu, sumu jeruhi
Unajeruhi watoto kwa pesa,
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye madawa ya giza baridi
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili
(b) Fafanua maudhui ya shairi hili
(c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta?
(d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzitolee mfano
(e) Eleza umbo la shairi hili
(f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi ;
(i) Giza baridi
(ii) Yanakufunga katika klabu

***Soma shairi hili, kisha uyajibu maswali yanayofuata:***

**3.** 1. Dunia yanishangaza, kwa mikiki na myujiza,
Yajaa sana kuwaza, ama nitajiumiza,
Kwa maovu kuigiza, nimejigeuza pweza,
Mola naomba ya jaza, nanuia kuwa mwema.

2. Utu uzima wangia, masoma namalizia,
Michezo yanizidia, rafiki wana udhia,
Sipati wala tulia, masomo sijafalia,
Mwenyewe najichukia, vitabu sijavishika.

3. Siku nazo zayoyoma, kesho nitasema nini?
Nitanena sikusoma, nitamdanganya nani?
Wazazi pesa wachoma, kunipeleka shuleni,
Kwa kuwa nimebaini, heri nitie bidii.

4. Mawi yamenizunguka, mungu wangu nibariki,
Kujiasa ninataka, nifanye yote ya haki,
Ningependa kuamka, utepetevu sitaki,
Nyuma sipendi kubaki, ningependa kufaulu.

5. Marafiki naeleza, kuwa nimeshachapuka,
Habari nazieneza, wala msije kumaka,
Ukweli ninawajuza, horomo nimeondoka,
Uvivuni nimetoka, niondoeni kundini.

6 Panda nalipulizia, kwa wa hapa na wa kule,
Nadhani nimesikia, mkazo natia shule,
Ukunguni nasusia, nataka kusonga mbele,
Sitaki zenu kelele, nidhamu naifwatile.

7. Leo nisipokazana, kesho nitakula nini?
Nitawakidhije wana? Nitakuwa mtu duni!
Riziki takuwa sina, nitaitwa mkunguni,
Moto najipaliani? Heri nijikuze sasa.

8. Mtegemea cha ndugu, atakufa maskini,
Ama atakuwa pwagu, aishie kifungoni,
Kwa nini niote sugu, na kweli i hadharani,
Sitajitia shimoni, nitayapenda masomo.

9. Baibai masahibu, msipende kunighasi,
Nitavisoma vitabu, mitihani niipasi,



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Nigeuke mahabubu, na mtu aso muasi
Hayana ya wasiwasi, yenu nyingi hayawani.

10. Jongoo nimemtupa, na mti wake pamoja,
Sitataka tapatapa, ninaitafuta tija,
Nyingi pigeni malapa, hatavishwa makoja,
Kuna siku itakuja, mtakuja kuhiliki!

**Maswali:**

(a) Andika kichwa mwafaka kinachofaa kuelezea shairi hili. (alama 2)
(b) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu zako. (alama 2)
(c) Marafiki wa mwandishi wana tabia gani? (alama 4)
(d) Ni nini dhamira ya mtunzi? (alama 2)
(e) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 5)
(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi
(i) Mikiki (ii) Kuyoyoma (iii) Mkunguni
(iv) Panda (v) Sugu

**4. <u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali :</u>**

1. Ukitazama dunia, umbo lake huarifu,
Kuwa imeandaliwa, wageni watukufu,
Tayari kuwapokea, na mambo sufufu,
Ndani yake yamejaa, viumbe kuwanadhifu.

2. Umbile huonyesha, namna ilivyotimu,
Yangoja kukaribishwa, katika mastakimu,
Yenye kila tamasha, machungu na matamu,
Maisha yanapokwisha, huiacha inadumu.

3. Ajae ardhi hii, kutoka katika mimba,
Mzizini au yai, au katika kitumba,
Milki hakinai, ya mali wala mashamba,
Mwisho wa uhai, kaburi lake jemamba.

4. Halii choyo kaburi, mtu uzima ukisha,
La upana shubiri, urefu pima yatosha,
Wala hadai fahari, tena hujifaharisha,
Akiwa hai fikiri, anavyopenda tamasha.

5. Yalipo maziara, masikani ya maiti,
Huonyesha ishara, na pengine tofauti,
Dhaifu na bora, hawagombi hawateti,
Wazima kila mara, Pato linawasalitia.



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

6. Mtu hashibi pato, hili huonyesha nini?
Laonyesha kama pito, kuwa yumo safarini,
Enda kuitika wito, bora usio kifani,
Ambao kila mtoto, wa Adam hutamani.

7. Yumo katika safari, kila mwanadamu,
Haraka au usiri, kwenda imelazimu,
Epusha roho kahari, yake na Jahanamu,
Iwe katika fahari, mwili ukiwa kuzimu.

**Maswali:**

(a) Pendekeza kichwa cha shairi hili. (alama 2)
(b) Mshairi amevitaja vitu aina ngapi vyenye uhai? Vitaje. (alama 4)
(c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 5)
(d) Eleza vina na mizani katika shairi hili. (alama 3)
(e) Eleza ujumbe wa mshororo:
"Halii choyo kaburi, mtu uzima ukishe." (alama 2)
(f) Onyesha vile uhuru wa kishairi ulivyotumiwa. (alama 4)

## 5. Vita vya ndimi

Huyo! Amshike huyo!
Hakuna bunduki wala kifaru
Bomu na risasi hata hawazijui!
Lakini mno wanashambuliana.
Kwa ndimi zilizonolewa kwa makali
Vipande vya matusi silaha zao.

Yu imara mmoja wao.
Akirusha kombora la neno zito!
Limtingishe adui wake
Na kumgusa hisia kwa pigo kuu.
Pigo linalopenya moyoni kama kichomi
Kuchipuza joto la hasira na kisasi
Katika mapigano yaso na kikomo.

Filimbi ya suluhu inapulizwa kuwaamua!
Ni nani anayekubali suluhu?
Roho zinakataa katakata
Huku ukaidi ukinyemelea na kutawala
kote
Mapandikizi ya watu yakipigana
Vitu shadidi visivyo ukomo
Vita vya ndimi!

Magharibi sasa
Jua linapungia mkono machweo
Nalo giza likinyemelea kwa kiburi na
kasi
Sisikii tena sauti za misonyo
Mate ya watesi yamekauka



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Makanwa yao yamelemewa na uchovu
Sasa wameshikana mikono
Nyuso zao zikitabasamu
Ishara ya suluhu!



**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)

(b) **Eleza** sifa za utunzi alizotumia mshairi. (alama 4)

(c) **Taja** kwa kutolea mifano tamathali za usemi zozote tatu zilizotumiwa katika shairi hili.(alama 3)

(d) **Fafanua** mishororo hii:

(i) Akirusha kombora la neno zito!

(ii) Makanwa yao yamelemewa na uchovu (alama 4)

(e) **Zungumzia** mgogoro katika shairi na namna unavyomalizika. (alama 6)

(f) **Toa** maana ya msamiati huu

(i) Kichomi

(ii) Misonyo (alama2)

6.***Soma mashairi ya A na B kisha ujibu maswali***.

A

Mtu ni afya yake, ndio uzima wa mtu
Mtu ni kuwa na chake, hakuwi ela kwa kitu
Mtu ni bahati yake, kupendekeza kwa watu
Mtu si fakhari kwako, kuitwa nyama ya mwitu

Mtu ni ulimi wake, kunena vyema na watu
Mtu ni kijungu chake, kuweka mawe matatu
Mtu ni mwenda kwa lake., mtoshawa na kula kitu
Mtu si uzuri kwake, kuitwa nyama wa mwitu

Mtu ni mwenye nadhari, apimaye kula kitu
Mtu ni moyo hariri, mwenye imani na watu
Mtu ni alo na ari, shika sana mwana kwetu
Mtu si yake fakhari, kuitwa nyama wa mwitu

Mtu ni mkono wazi, mtasadaku na watu
Mtu ni mwenye maozi, kuoneya kula kitu
Mtu ni alo tulizo, asopenda utukutu
Mtu si jambo pendezi, kuitwa nyama wa mwitu

Mtu ni mwenye ahadi, ndio u'ngwana na utu
Mtu ni alo baridi, mbembeleza wa watu
Mtu ni moyo asadi, asoonewa na mtu
Mtu si yake ifadi, kuitwa nyama wa mwitu

Mtu niliyoyanena, pima sana ewe mtu
Mtu sikuja tukan, kukirihi nyoyo watu
Mtu nakupa maana, wende <u>nyendo</u> za kiutu
Mtu si uzuri sana, kuitwa nyama wa mwitu
Mtu ni mtenda njema, atwiiye Mola wetu
Mtu ni mbele na nyuma, pima sana mwana kwetu
Mtu natiye <u>khatima</u>, fafanua kula kitu
Mtu si yake hisima, kuitwa nyama wa mwitu.

**B**

**MTU HACHAGUI KAZI**

Naamba kazi ni kazi, vyovyote vile iwavyo
Madamu si <u>ubazazi</u>, kwa mwanaadamu ndivyo
Kushona na upagazi, pia vile vyenginevyo
Kazi ni kitu azizi, wala vyenginevyo sivyo
Mtu hachagui kazi.

Mtu hadharau kazi, ile ahisiyo duni
Ayuzuie machozi, walilia jambo gani
Ukulima na ukwezi, na uvuvi baharini
Hizi nazo njema kazi, yafaa uzibaini
Mtu hachagui kazi

Si laiki kubughudhi, hakuna iliyo duni
Hayo makubwa maradhi, na tena uhayawani
Kazi zote zina hadhi, hivyo tusibagueni
Inafaa tuziridhi, tuzitende kwa yakini
Mtu hachagui kazi.

Ni wajibu kuipenda, na kuikiri moyoni

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

Na kwa dhati kuitenda, kwa juhudi na makini
Matatizo huyashinda, na uvivu kuuhuni
Hapo mtu atashinda, na magumu kumhuni
Mtu hachagui kazi

**MASWALI**

(a) Lipe shairi la A kichwa mwafaka. (alama 1)

(b) Kwa mifano mwafaka **fafanua** bahari katika shairi la **A** na **B**. (alama 4)

(c) Toa sababu za mwandishi kuchagua "Mtu hachagua kazi" kama kichwa cha shairi la **B**. (alama 1)

(d) Mtunzi alikuwa na ujumbe gani katika mashairi haya? (alama 4)

(e) **Andika** ubeti wa pili wa shairi A katika lugha nathari. (alama 4)

(f) **Eleza** muundo wa shairi la B. (alama 4)

(g) **Eleza** maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika mashairi haya. (alama 2)

(i) Nadhari

(ii) Ubazazi

## 7. *Soma shairi lifuatalo kisha uiibu maswali*

Duniani husifiki;
Wala hupati thamani,
Yalisemwa hukumbuki?
Na wazee wa zamani,
"Mkono haurambiki,
Bila kitu kiganjani"

Wangapi watu azizi,
Fulani bin Fulani,
Waliokichinja mbuzi,
Kukirimu mitaani,
Sasa kama wapuuzi,
Kwa hali kuwa ta'bani

Walifanya makubeli.
Wakaapa hadharani,
La uongo huwa kweli,
" Kubishika kitaani,
Na tangu kukosa mali,
Wakawa kama nyani!

Walifanya mahashumu.
Kuwaliko masultani,
Ushekhe na Ualimu,
Kufasiri vitabuni,
Na leo wana wazimu,
Kama si wanachuoni.

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

**Maswali**

(a) Kwa maneno yako mwenyewe **eleza** ujumbe wa shairi hili. (Alama 3)
(b) **Eleza** jinsi mshairi anavyosisitiza huo ujumbe katika shairi lote. (Alama 4)
(c) **Eleza** kwa tafsili umbo la shairi hili. (Alama 5)
(d) **Andika** ubeti wa kwanza katika lugha nathari. (Alama 3)
(e) **Eleza** maana ya maneno haya kama yalivyo tumika katika shairi;
   (i) Kiganjani.
   (ii) Kukirimu.
   (iii) Makubeli.
   (iv) Mahashumu.
   (v) Wanachuoni (Alama 5)

**8.** ***Soma shairi lifuatalo kisfea ujibu saaswali vanavofuata:***

Niliusiwa zamani, babu aliniusia, N
ili bado utotoni, hapo aliponambia,
Babu yaweke kitwani, yasije yakapotea,
Penye nia ipo njia, usikate tumaini.

2. Wewe bado ni mgeni, katika hii dunia,
Mimi ndiye wa zamani, mengi nimejionea,
Sasa niko uzeeni, uzee umewadia,
penye nia ipo njia, usikate tumaini.

3. **Mtima** ndio **sukani**, waongoza'kila ndia,
Weka mkazo moyoni, kila unalofwatia,
Moyoni mwako amini, kuwa utalifikia,
Penye nia ipo njia, usikate tumaini.

4. Kama uko safarini , waongoza kila ndia,
Bahari kuu kinani, mawimbi yakuchachia,
Usikate tumaini. hapo ndipo penye ndia,
Penye nia ipo njia, usikate tumaini.

5. Hapo hapo mawimbini, wewe hapo pigania,
Hapo ndipo milangoni, mawimbi yakuzuia,
Mtima utie kani, bandarini utangia,
Penye nia ipo njia, usikate tumaini.

6. Na iwapo ni shuleni, masomo yakutatia,
Usiasi masomoni, kusoma ukakimbia,
Kidogodogo bongoni, elimu itakungia,
Penye nia ipo njia, usikate tumaini.

7. Kama wenda uchumini, biashara **waania**.
Usihofu asilani, hasara ikitukia,
Leo ukipata duni, na kesbo litazidia,
Penye nia ipo njia, usikate tumaini.

(a) **Andika** methaii ambayo ingetumiwa kujumuisha ujumbe katika ubeti wa pili. (Alama 1)
(b) Kutokana na shairi hili, ni katika nyanja zipi za maisha tunapopaswa kujikakamua? Tujikakamue vipi? (alama 6)
(c) **Taja** arudhi ambazo zimetumiwa kuusarifu ubeti wa kwanza. (Alama 4)
(d) Huku ukitoa mfano mmoja **bainisha** uhuru wa kishairi ambao umetumiwa katika ubeti wa 3.

(alama 1)
(e) **Andika** ubeti pili kwa lugha ya nathari. (Alama 4)
(f) **Eleza** maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi.
   (i) Aliniusia.
   (ii) Mtima.
   (iii) Sukani
   (iv) Waania.
   (Alama 4)

**9. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

**Kaka**: Kusoma nilikosoma, kambiwa sipati kazi,
Yapata mwaka mzima, nategemea shangazi,
Wasiojuwa husema, ‘ sababu sina ujuzi,’
Huno uhaba wa kazi, mesababishwa ni wake.

**Dada**: Mbona watuingilia, kaka acha ubaguzi,
Likukeralo twambia, tulijuwe waziwazi,
Au unalochukia ni wake kufanya kazi?
Mambo ya siku hizi,watu ni bega kwa bega.

**Kaka**: Siwangilie kwa nini, nanyi mwatukopa kazi
Kwani tokea zamani, hazikuwa shida hizi,
Mtu kitoka shuleni, kibaruwa si tatizi,
Leo hatupati kazi, kisa nyinyi wanawake

Dada: Hapo kaka hujasema, kuwa wake ndiyo chanzi,
Chanzo cha hii nakama, waume kukosa kazi,
Bure mwatupa lawama, wenyewe mna ajizi,
Mtindo wa siku hizi, watu ni bega kwa bega.

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

**Kaka**: Hayo unayotamka, yote niya upuuzi,
Mumetoroka kupika, kazi yenu toka enzi,
Bilashi mwahangaika, kushabihi vijakazi,
Sasa hatupati kazi, kisa nyinyi wanawake.

**Dada**; Mbona wafanya ukali, ishakuwa ni chukizi?
Hata na yangu kauli, umekuwa husikizi,
Nisemaye ni halali,ukweli uliowazi,
Mtindo wa siku hizi, watu ni bega kwa bega.

**Kaka**: Yana uhalali gani, mbona basi huelezi?
Kipita maofisini, mumejaa kama inzi,
Mwataka tuwe mekoni, wala halitupendezi,
Na nje hakuna kazi, kisa nyinyi wanawake.

**Dada**: kakangu una matata, kuyaelewa siwezi,
Wasema unamopita, wambiwa hakuna kazi?
Na sisi wake twapata, haraka pasi ajizi,
Sababu siku hizi, watu ni bega kwa bega.

**Kaka**: Sisi kazi hatupati, wengi wetu ni mijizi,
Elanyi muna bahati, mabosi hawawaizi,
Hampotezi wakati, ni kidogo pingamizi,
Nasi hatupati kazi, kisa nyingi wanawake..

**Dada**: kakangu wanichekesha, hadi sina kizuizi,
Vipi lakukasirisha, sisi tukifanya kazi?

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

Hujui ndivyo maisha, yaendavyo siku hizi?
Mtindo wa siku hizi, watu ni bega kwa bega.

**Kaka**: Huna haja ya kucheka, nisemayo si upuzi,
Kazi inayojulika, yenu ni kukuna nazi,
Kisha mwenda zianika, mukaziuze takizi,
Leo hatupati kazi, kisa nyinyi wanawake.

**Dada**: Yalikuwa ni ya kale, kuuza chicha za nazi,
Ela leo twenda mbele, na nyuma hatujibanzi,
Hakuna aliyelele, kushiriki usingizi,
Kwani mambo siku hizi, watu ni bega kwa bega.

**Kaka**: kulla kitu mwakitaka, kiwe chenu siku hizi,
Ishakuwa na miaka, pia mwataka ihozi,
Nasikia mwatamka, mwaka huno wa ledizi,
Mwisho mutataka myezi, iwe yenu wanawake.

Hai mana kubishana, nikashabihi mkizi,
Mengi niliyoyanena, yafanyie uchunguzi,
Iwapo tutafanana, yupi taleya vizazi?
Sisi hatupati kazi, hadi murudi mekoni.

**Dada**: Baba mbele mama nyuma, yamekuwa simulizi,
Muradi sote twasoma, soteni tuwe walezi,
Wake haturudi  nyuma, tunataka mapinduzi,
Maisha ya siku hizi, watu ni bega kwa bega.

**MASWALI**

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (Alama 2)

b)Dada anatoa sababu gani ya wanawake kuajiriwa maofisini? (Alama2)

c) Kaka anataja sababu zipi za wanaume kukosa kuajiriwa kazi? (Alama2)

d) Eleza umbo la shairi hili (Alama3)

e)Dondoa na ueleze mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi katika shairi(Alama4)

f) Kwa mujibu wa shairi hili, kazi za wanawake ni zipi? (Alama2)

g) Eleza ubeti wa mwisho kwa maneno yako mwenyewe (Alama2)

h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. (Alama3)

(i) Kulla

(ii) Nakama

(iii) Ajizi

10.**Soma shairi hili kasha ujibu maswali**.

1. Pasi kuhofu lawama, imenibidi kunena,
Nina mengi ya kusema, ambayo ni ya maana
Kwetu sote ni lazima, viumbe kuambizana,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema.

2. Sahau I akilini, yataka kukumbushana,
Madamu tu duniani, la kosa huelezana,
Ili tuwe hadharini, tujilinde na fitina,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

3. Uchochezi ukitiwa, uwongo unapofana,
Lolote laweza kuwa, hata watu kupigana,
Fitina yaweza ua, binadamu wengi sana,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema.

4. Fatani anapojua, jamii yasikizana,
Aweza leta adawa, ya fitina kugombana,
Hata akawa baguwa, ndugu wakafarikana,
Yashinda kifo fitina, fatani si ntu mwema.

5. Nahakikisha wenzangu, fitina ina laana,
Fitina kwa Bwana Mungu, katu hataki iona,
Yasaliti walimwengu, mume mke kuachana,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema.

6. Fitina si kitu safi, nazidi toa bayana,
Fitina ina makofi, muda ukijulikana,
Fitina ni ukorofi, mfano wake hapana,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema.

7. Fitina yashinda tusi, uovu wa kutukana,
Fitina ina maasi, madhambi ya kujazana,
Fitina ina utesi, tena usowezekana,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema

8. Fitina si masihara, yashinda hata khiana,
Fitina ina madhara, nchi zaweza gongana,
Fitina aina izara, na aibu nyingi sana,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema.

9. Fitina haina shaka, ni mbovu nasema tena,

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

Fitina mali hakika, ya ghibu nawe waona,
Fitina ina mashaka, na dhiki kila namna,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu mwema.

10. fitina kitu haramu, tamati zaidi sina,
Fitina na binadamu, wawe wakichukiana,
Fitina ni mbaya sumu, ya au sifa na jina,
Yashinda kifo fitina, fatani si mtu, mwema.

**Maswali:**

(a) Bainisha athari tano za fitina kulingana na mshairi (alama 5)

(b) Ubeti wa sita umechukua mikondo na bahari tofauti tofauti. Zitaje na utoe mifano (alama 4)

(c) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari (kawaida) (alama 3)

(d) Mshairi ametumia mbinu zipi kufanya jumbe zake zieleweke kwa bayana zaidi. (alama 4)

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi.

(i) Adawa

(ii) Fatana

(iii) Wakafarikana

(iv) Tusi (alama 4)

**11.Soma shairi hili kisha ujibi maswali yanayofuata.**

1. Tusitake kusimama, bila kwanza kusimama,
Au dede kuwa hima, kabla hatujakaa,
Tutakapo kuchutama, kuinama inafaa,
Tujihimu kujinyima, makubwa kutoyavaa.

2. Tusitake kuenenda, guu lisipokomaa,
Tujizonge na mikanda, inapochagiza njaa,

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

Na mazuri tukipenda, ni lazima kuyandaa,
Tujiase kujipinda, kujepusha na balaa.

3. Tusitake uvulana, au sifa kuzagaa,
Tushikaye nyonga sana, tunuiyapo kupaa,
Kama uweza hapana, tutoelee dagaa,
Tujiase hicho kina, maji yajapokujaa.

4. Tusitake vya wenzetu, walochuma kwa hadaa,
Wanaofyatua vitu, na kasha vikasambaa,
Uwezo hatuna katu, umaskini fazaa,
Tujihimu kula vyetu, siendekeze tamaa.

5. Mtaka kuiga watu, kufata kubwa rubaa,
Vyao vijaile kwetu, vifaa vingi vifaa,
Tunamezwa na machatu, tusibakishwe dhiraa,
Tujihimu kilo chetu, hata kama twapagaa.

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)

(b) Eleza madhumuni ya shairi hili (alama 2)

(c) shairi hili ni bahari gani? Toa sababu. (alama 4)

(d) Bainisha umbo katika ubeti wa kwanza na wa mwisho ukizingatia vina na mizani. (alama 4)

(e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)

(f) Taja mbinu moja ya kisanii inayoibuka katika ubeti wa nne. Kwa nini imetumiwa? (alama 2)

(g) Eleza msamiati ufuatao kama unavyotokea katika shairi. (alama 3)

(i) Kuiga

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

(ii) Dede

(iii) Tujizonge.

# FASIHI SIMULIZI

1. a) **Taja sifa za tanzu zifuatazo za fasihi simulizi**

    i) Hurafa
    ii) Mighairi
    iii) Miviga

    b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamii
    c) Eleza umuhimu wa mafumbo
    d) Eleza tofauti kati ya malumbano ya utani na mawaidha

2. (a) Huku ukizingatia sifa za kimuundo za methali, jadili matumizi ya tamathali za usemi sifuatazo:-
    (i) Istiari/sitiari
    (ii) Tashihisi
    (iii) tashbihi

    (b) Vitanza ndimi vina dhima gani katika jamii?
    (c) Taja majukumu matatu ya nyimbo katika fasihi simulizi
    (d) Eleza sifa tatu za ngano za mtanziko
    (f) Eleza sifa tatu za Nyiso
    (e) Fasihi simulizi ina sifa ya kuhifadhiwa akilini. Eleza udhaifu wa uhifadhi wa akilini (al. 4)

3. (i) Eleza maana ya vitanza ndimi.
    (ii) Taja na ufafanue umuhimu wa vitanza ndimi katika jamii

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

# MASWALI YA KARATASI LA TATU

# CHOZI LA HERI

1) "Mwanangu, usimpake tope baba yako. Amekulea kwa miaka yote hii kama mwanawe, japo kwa kweli hakuzaa wewe."

*(a)* *Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)*

*(b)* *Kwa kurejelea wahusika wengine wanne wa kike katika riwaya, thibitisha matatizo manne yaliyowakumba katika jamii ya Chozi la Heri. (alama 4)*

2) "Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike; yule anayesimuliwa katika visakale vya majirani zetu."

*(a)* *Eleza mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)*

*(b)* *Onesha jinsi wahusika wa kike katika riwaya walivyojitahidi kuleta mabadiliko yenye*

*(c)* *manufaa katika nchi ya Wahafidhina. (alama 16)*

3) ."Ni kweli watu wana haki ya kusamehewa, kwani hakuna binadamu hata mmoja aliyekamilika." Kwa kurejelea riwaya, jadili kauli hii.

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

4) "Hakujali kuwa amemwacha mwenzake akitapatapa na maumivu ya kusalitiwa." Onesha vile mwandishi ameshughulikia maudhui ya usaliti.

5) ."Mtu anayekusikiliza atadhani kwamba umekulia katika mazingira sawa na Sisi wanyonge ambao uwepo wetu unaamuliwa na matajiri."

*(a)* *Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)*

*(b)* *Fafanua tamathali ya usemi iliyotumika na msemaji wa kauli hii.. (Alama 4)*

*(c)* *Fafanua sifa za mrejelewa katika kauli hii. (Alama 12)*

6) "Wakati wa mabadiliko umefika. Wimbi la mabadiliko limevamia jamii yetu." Jadili mabadiliko yaliyotokea na athari zake katika nchi ya Wahafidhina.

7) Ndio. Sijui kwa nini watu hawa hawajifunzi kutokana na majanga yanayowakumba wenzao...

*(a)* *Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)*

*(b)* *Onesha changamoto zilizomkabili msemaji na wenzake katika kuwashughulikia wanaolengwa katika siku za awali. (Alama 6)*

*(c)* *Fafanua majanga kumi yanayowakabili watu wa rika la warejelewa katika dondoo. (Alama 10*

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

8) "Ni kweli binti yangu, kwa kutumia falsafa hii, una haki ya kusema Sisi tu watoto wa miaka hamsini."

(a) *Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)*

(b) *Eleza maana ya kauli: 'tu watoto wa miaka hamsini' kwa mujibu wa dondoo. (alama 2)*

(c) *Tetea ukweli wa kauli hii kwa kurejelea matukio katika riwaya. (alama 14)*

9) "Nilipojaribu kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika.

(a) *Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)*

(b) *Fafanua mambo mbalimbali yaliyomfika anayesema maneno katika dondoo hili. (Alama 8)*

(c) *Ridhaa aliyapitia maisha kama ya mhusika kwenye dondoo. Yataje. (Alama 8)*

10) "Moja ya mambo yanayijitokeza katika Chozi la Heri ni migogoro ya kinasaba." Jadili.

11) Jadili maudhui ya nafasi ya mwanamke katika riwaya ya Chozi la Heri.

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

12) "Si kufua, si kupiga deki, si kupika, almradi kila siku ilikuwa na adha zake."

*a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)*

*b) Eleza mbinu ya lugha ambayo imetumika kwenye dondoo. (alama 2)*

*c) Eleza kwa kifupi madhila aliyoyataja msemaji. (alama 2)*

*d) Eleza kwa mifano jinsi haki za watoto zimekiukwa katika riwaya ya Chozi la Heri. (alama 10)*

13) "Hakuna msiba usiokuwa na mwenzake."

*a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)*

*b) Eleza tamathali ya usemi katika dondoo hili.*

*c) Eleza sifa za anayerejelewa.*

*d) Fafanua matatizo wanayoyapitia wakimbizi wa ndani kwa ndani.*

14) *"Mabadiliko ni aushi*". Huku ukirejelea riwaya ya Chozi la Heri, thibitisha kauli hii.

15) Eleza jinsi Uongozi bora umedhihirika katika riwaya ya chozi la heri

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

16) Onyesha jinsi Udhaifu wa uongozi umebainika katika jumuiya ya chozi la heri

17) Fafanua Mbinu ambazo viongozi wanatumia kujidumisha mamlakani katika chozi la heri

18) Ukiukaji wa haki za binadamu ni jambo la kawaida katika chozi la heri. Jadili

19) Utamaduni umeangaziwa kwa mapana katika chozi la heri. Jadili

20) Eleza jinsi mwanamke amesawiriwa kwa njia chanya katika riwa ya chozi la heri

21) Riwaya ya chozi la heri imemsawiri mwanamke kwa njia hasi .jadili

22) Eleza jinsi mwanamke anavyoendeleza ukiukaji wa haki za binadamu katika chozi la heri

23) Jadili Nafasi ya vijana katika ujenzi wa jamii

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

24) Fafanua jinsi Vijana wamechangia kurudisha nyuma maendeleo ya jamii katika chozi la heri

25) Dhuluma imekita mizizi katika jumuiya ya chozi la heri. Jadili

26) Eleza jinsi Suala la ukoloni mamboleo limejitokeza katika riwaya ya chozi la heri

27) Suala la ufisadi limeshughulikiwa katika Chozi la heri kwa njia mbalijnbali. Fafanua njia hizo

28) Fafanua matumizi ya mbinu ya Sadfa katika chozi la heri

29) Hotuba ni kipengele cha kimundo. Eleza jinsi kipengele hiki kimetumiwa katika kufanikisha ploti wa riwaya ya chozi la heri

30) Fafanua matumizi ya mbinu ya Uigizaji/Tamthilia ndani ya riwaya ya chozi la heri

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

# MASWALI ZAIDI YA MUKTADHA

*Tia dondoo katika muktadha wake*

1) "Hii ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mungu amenifidia yule mwanangu aliyekufa"

2) " Usiku umekuwa mpevu, twende tusije tukamtia mama kiwewe''

3) " Huenda nikapata mbinu ya kujinasua baadaye''

4) " Di, usijali. Mimi nitawakimu kwa viganja hivi vyangu. Hamtapungukiwa na lolote''

5) "Basi Doc, nakubaliana na rai yako"

6) " Huyu hapa ameletwa  na wasamaria wema leo asubuhi''

7) " Je ni yule aliyeletwa jana usiku wa kuamkia jana''

8) " Hatuwezi kumkabidhi mzee wetu huyu kifaranga kitekite hivi, tutakuwa tunampagaza uzazi"

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

9) “ Yako ya arubaini imefika”

10) “ Wenye hadhi na mali wanahitaji wafanyikazi wa kuwaendelezea biashara zao’’

11) “ Usiwe na mawazo finyu na hasi kuhusu kumpanga mtoto’’

12) “ Karibuni naona mmetuletea kilaika’’

13) “ Tulipata ombi lenu kuhusiana na suala la kumpanga mojawapo wa watoto wetu’’

14) “ Ndugu zako wako hai na bila shaka mtakutana”

15) Yote haya yamewezekana kutokana na mwongozo mlionipa nyinyi. Zaidi , utulivu nilioupata nilipoambulia familia hii ulinipa msukumo kila mara nilipokabiliwa na ndaro

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

# MASWALI YA KIGOGO

1.... Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha kichwa! Mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana....

a. Weka dondoo hili hili katika muktadha wake (Alama 4)
b. Fafanua mbinu mbili za sanaa alizozitumia mwandishi (Alama 4)
c. Ukirejelea tamthilia ya Kigogo, dhihirisha kuwa mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana.(alama 12

2. Utawala wa majoka katika jimbo la sagamoyo umejaa sumu ya nyoka''. Jadili usemi huu(alama 20)
3. "Wamenimaliza… Wamenigeuka…″.
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (Alama 4)
   b) Eleza namna msemaji amemalizwa na kugeukwa? (Alama 4)
   c) Eleza umuhimu wa msemaji. (Alama 4)
   d) Eleza jinsi wahusika wengine walivyomaliziwa katika tamthilia. (Alama 8)
4. "Mataifa mengi ya Afrika yamekumbwa na tatizo la uongozi mbaya." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya kigogo. (al 20)
5. Uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mapenzi!
   a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)
   b) Andika mbinu mbili za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili. (alama 4)
   c) Taja hulka za mnenaji unaojitokeza katika dondoo. (alama 2)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

d) Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia. (alama 10)

6. Ni bayana kwamba viongzoi wengi katika nchi zinazoendelea wamejawa na tamaa na ubinafsi. Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia ya kigogo. (alama 20)

7. “Unayazika matumizi yetu .Unaifukia kesho yetu.”
   a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b. Onyesha jinsi anayeambiwa maneno haya anavyoifukia kesho ya wenzake (alama 16)

8. ”Msiba wa kujidunga hauna kilio.” Thibitisha kauli hii kwa kurejelea ya Kigogo (alama 20)

9.
   a) Utawala wa sagamoyo unatumia mbinu nyingi kubakia mamlakani. Fafanua zozote kumi (alama 10)
   b) Mwanamke ni nguzo imara katika ujenzi wa jamii. Eleza kauli hii ukirejelea tamthilia ya kigogo (alama 10)

10. “Tuacheni kufumbatia maji kama jiwe. Sagamoyo inahitaji mabadiliko, damu nyepesi ili kuufungua ukurasa mpya”
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Kwa kutoa mifano taja tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili(alama4)
   c) Kwa nini sagamoyo inahitaji mabadiliko? (alama 10)
   d) Taja sifa moja ya msemaji inayojitokeza katika dondoo hili (alama 4)

11. Kwa kurejelea mifano mbalimbali thibitisha dai kuwamwandishi huyu amemlika uhalisia wa jamiiya Kenya (al. 20)

12. Ona sasa! Mnaniharibia biashara. Nimewapa dakika moja muione nyumba hii paa. Nikiwapatahapa, mtajua kwa nini wananiita………

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
b) Tambua kwa kutolea mfano mbinu moja ya lugha inayojitokeza katika muktadha huu. (al.2)
c) Kwa kurejelea mifano mbalimbali eleza madhara/matokeo ya shughuli za msemaji katika dondoo hili kwa jamii husika (al. 14)

13. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika Tamthlia hii. (alama 20)
   a) Kinaya
   b) Majazi

14. Ami ? Tangu lini ukawa ami yangu?
   a) Eleza muktadha wa dondoo (Alama 4)
   b) Taja mbinu iliyotumika katika dondoo hili (AIama 2)
   c) Eleza sifa za msemaji (AIama 8)
   d) Bainisha maudhui ya nafasi ya mwanamke ukizingatia mhusika huyu (AIama 8)

15. Uongozi mbaya ni tatizo sugu linalokumba mataifa mengi ya Afrika. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya kigogo. (alama 20)

16. ``Haja zako ni haja zangu, shida zako ni shida zangu, kiu yangu ni kiu yako. ``
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. Alama 4
   b) Kwa kurejelea dondoo taja na ueleze sifa nne za msemaji na msemewa. Alama 8
   c) Taja tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondoo alama 2
   d) Kwa kurejelea tamthilia ya kigogo eleza jinsi mbinu zifuatazo zimejitokeza

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

a. Nyimbo
b. Jazanda
c. Majazi alama 6

17. “Mimi ni mtu wa vitendo, si wa vishindo.”

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama. 4)

(b) Kwa kurejelea dondoo eleza sifa mbili za mnenaji (alama. 4)

(c) Thibitisha ukweli wa kauli ya mnenaji. (alama. 12)

18. Ukiukaji haki na uvunjaji sheria ni mambo yaliyokithiri katika jimbo la Sagamoyo. Thibitisha. (alama. 20)

19. “………..Acha porojo zako . Kigogoo hachezewii watafuta maangamimi!”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Fafanua sifa za muzungumzaji (alama 4)
c) Eleza jinsi msemewa alivyokuwa akimchezea kigogo katika muktadha huu. (alama2)
d) Kwa kurejelea hoja kumi kutoka kwenye tamthilia Onyesha ukweli kuwa ‘Kogogo hachezewi (alama 10)

20. Kwa kirejelea tamthilia ya kigogo, jadili mbinu - ishi tunazojifunza kutokana na kijana Tunu. (alama 20)

21. “Ukitaka kukula asali kaa na nyuki!”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. [alama 4]
b) Bainisha mbinu iliyotumika katika dondoo hili. [alama 2]
c) Eleza jinsi wahusika hawa walivyofaidika kutokana na kukaa na nyuki. [alama 14]
    i. Chopi
    ii. Kenga

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

iii. Ngurumo
iv. Mamapima

22. Eleza jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya majazi.
[alama 20]

23. “Shika hamsini zako wewe ... Hatutaki kufanya nira na mtu ...”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)

(b) Eleza tamathali ya usemi iliyotumika.
(alama 2)

(c) Uongozi wa Majoka umesheheni sumu ya nyoka. Thibitisha kwa kudokeza hoja kumi na nne. (alama 14)

24. . Utawala mbaya ni tatizo sugu linalozikumba nchi nyingi za kiafrika. Jadili, kwa kurejelea matukio ishirini katika tamthilia ya Kigogo (alama 20)

25. “Ulitaka wahamie wapi siku kama hizi? Wamekuja kuuguza majeraha yao ya kufungiwa soko.”

a) Weka maneno haya katika muktadha wake.
(alama 4)

b) Tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili
(alama 2)

c) Kando na kufungiwa soko, Wanasagmoyo wanauguza majeraha yepi mengine yanayosababishwa na utawala wa Majoka
(alama 5)

d) Fafanua sifa za msemaji wa dondoo hili.
(alama 9)

26. "Si haki. Unayazika matumaini yetu. Unaifukua kesho yetu. Unatupoka utu na heshima yetu."

a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Eleza tamathali iliyotumika kwenye dondoo hili. (alama 2)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

c) Onyesha vile mrejelewa alivyoyazika matumaini na alivyofukua kesho yao. (alama 14)

27. Tamthilia ya Kigogo ni taswira kamili ya matatizo yanayokumba mataifa mengi barani Afrika. Fafanua ukirejelea Tamthilia nzima. (alama 20)

28. “Kitabu si jalada, fungua ndani usome mambo. Kitanda usichokilalia kunguni wake huwajui.”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Kwa kurejelea tamthilia ya kigogo, thibitisha ukweli wa dondoo hili. (al.14)

c) Taja tamathali za usemi zilizotumika katika dondoo hili. (al.2)

29. Eleza mbinu alizotumia majoka kuendeleza uongozi wake. (al.20)

30. “Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka……”

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapinduzi? (alama 8)

c) Taja sifa zozote nane za muhusika huyu (alama 8)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

# 3.TUMBO LISILOSHIBA

1. **Alifa chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na hadithi nyingine**

"Doa ndio kawaida inayobainisha maisha ya mwanadamu."Onyesha ukweli wa kauli hii kwa mujibu wa hadithi za: **Shogake Dada ana Ndevu, Mame Bakari, Shibe Inatumaliza na Mtihani wa Maisha. (alama 20)**

2. Na kwa nini hazitaki kuukemea mfumo huu wa maisha? Mfumo wa mwenye nacho kuendelea kupata na msinacho kuendelea kukosa?
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua maudhui mawili yanayodhihirika katika dondoo hili (alama 4)
   c) Tambua na ueleze sifa sita za msemaji (alama 6)
   d) Eleza athari ya " msinacho kuendelea kukosa" katika jamii husika (alama 6)

3. Fafanua jinsi suala la elimu limeshughulikiwa katika *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* kwa kurejelea hadidhi zifuatazo:
   *a) Mapenzi ya Kifaurongo alama 5)*
   b) *Shogake Dada ana Ndevu* (alama 5)
   c) *Mtihani wa Maisha* (alama 5)
   d) *Mwalimu Mstaafu* (alama5)

4. ***"… Basi niache nitafute pesa. Muhimu mniunge mkono…"***
   (a)Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

(b) Fafanua sifa zozote nne za mzungumziwa (alama 4)

(c) Fafanua athari ya vitendo vya mzungumzaji wa maneno haya katika jamii (alama 12)

**5.** Jadili suala la uozo wa maadili katika jamii huku ukirejelea hadithi zozote nne katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (alama 20)

**6.** Eleza nafasi ya vijana katika jamii ukerejelea hadithi fupi zifuatazo.

a) Mapenzi ya kifa urongo

(alama 5)

b) Shogake Dada anaDevu

(alama 5)

c) Mame Bakari

(alama10)

**7.** Ndoto ya mashaka: Ali Abdalla Ali

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

***"Sasa nimechoka mja. Nimechoka hata naradua kufa kuliko kuishi. Hadilini haya mashaka ya kutengenezwa? Mashaka ya mashaka!***

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika (alama 4)

c) Fafanua mambo sita yanayomfanya mrejelewa aradue kufa. (alama12)

**8.** "Kwetu tunapigania mikono ielekee vinywani. Mzoea vya sahani, vya vigae haviwezii"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al 4)

b) Tambua tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili

c) Fafanua sifa nne za msemaji (al 4)

d) Jadili maudhui ya utabaka ukirejerea hadithi husika (al 10)

**9.** Jadili maudhui ya usaliti katika hadithi;

a) Mapenzi ya kifaraurongo (al 10)

b) Mame Bakari (al 10)

**10.** "Madhila ya mtoto mvulana katika karne ya ishirini na moja ni mengi." Tetea kauli hii kwa hoja ishirini ukirejelea hadithi ya

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

*Mapenzi ya Kifaurongo*, *Masharti ya Kisasa* na *Ndoto ya Mashaka*. (alama 20)

**11. Salma Omar: *Shibe Inatumaliza***

***(a)" Sijali lawama mnonilaumu"***

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) DJ na wenzake wanaonekana kufurahia maudhui ya wimbo huu. Thibitisha. (alama 6)

(b) **Alifa Chokocho: *Shogake Dada ana Ndevu***

"…tumshukuru kwa jinsi alivyomwongoza na kumwelekeza kwenye njia iliyonyooka" Ukirejelea wasifu wa Safia, tetea na upinge kauli hii. (alama 10)

**12.** Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifaurongo, onyesha jinsi jamii imegawanyika kitabaka kuegemea.

i. Kielimu
ii. Kikazi
iii. Kiuchumi (alama 20)

**13.** SHIBE INATUMALIZA

***"Ndugu yangu kula kunatumaliza"***

***"Kunatumaliza au tunakumaliza***"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)

b) Fafanua maana kitamathali katika kauli 'Kula tunakumaliza' (al. 10)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

c) Kwa mujibu wa hadithi hii, kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza? (al.6)

14. ‘**MAME BAKARI’**

Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake, onyesha kwa mifano mwafaka. (al. 10)

‘**MASHARTI YA KISASA’**

“............... mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukandamizaji, ni ushabiki usio na maana.”

Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi. (al. 10)

15. Jadili jazanda za anwani katika hadithi zifuatazo

16) Shibe Inatumaliza (alama8)

17) Mtihani wa maisha (alama6)

18) Mkubwa

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

(alama 6)

16. ***MAPENZI YA KIFAURONGO***

***"Kutazama shule za vijijini kumwibua bingwa katika mtihani wa kitaifa ni kama kutarajia kupata maziwa kutoka kwa kuku."***

a. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b. Tambua mbinu moja ya lugha kwenye dondoo hili. (alama 2)

c. Jadili maudhui yafuatayo katika hadithi hii

   i) Mabadiliko (alama 5)

   ii) Uozo (alama 5)

**17.** ***"... maendeleo yanadai mchango wa kila mtu, maskini na tajiri"***

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja na ueleze sifa nne za msemaji katika dondoo hili. (alama 4)

c) Mambo yepi mengine ambayo msemaji huhojiana na wenzake wanapokutana ? (alama 6)

d) Taja na ueleze maudhui matatu yanayojitokeza katika dondoo hili.(alama 6)

**18.**Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, 'Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.' Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi.(alama 20)

19. ***"…..ilmuradi mawazo yanamwadhibu sasa"***

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b. Fafanua sifa za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)

c. Onyesha mawazo yanayomwadhibu anayerejelewa na dondoo hili. (alama 10

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

20.

a. ***“ Mamangu siku ile aliniamsha mapema.”***

i) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)

ii) Tathmini umuhimu wa usimulizi wa mzungumzaji katika kuendeleza dhamira ya hadithi hii. (a 8)

b. Onyesha jinsi mashaka linavyomwafiki mhusika mwenyewe katika hadithi ya “Ndoto ya Mashaka”(alama 8)

21. i) Sekta ya elimu ina changamoto nyingi.Thibitisha kwa kurejelea hadithi zifuatazo :(alama 20)

a) Mapenzi ya Kifaurongo
b) Shogake dada ana Ndevu
c) Mwalimu Mstaafu
d) Mtihani wa maisha

22 ‘’ Hakikubakia hata chakula kidogo cha sadaka ya mwenye njaa… ‘’

i) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja kumi ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba (al 10)
ii) Jadili uhalisia wa hadithi ya Tumbo Lisiloshiba katika jamii ya leo kwa kutoa hoja kumi. (al 10)

23. "Mame Bakari" (Mohamed Khelef Ghassany)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

***"Dunia we' dunia. Dunia ya mwenye nguvu, si ya mimi dhaifu wa nguvu. Dunia ya msumari moto juu ya donda bichi."***

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

(b) Ni mbinu ipi iliyotumika katika dondoo hili? (alama 2)

(ch) Taja baadhi ya maamuzi ya maana yaliyofanywa na msemaji wa dondoo.(alama 6)

24. **"Tulipokutana Tena" (Alifa Chokocho)**

***"Hivi ndivyo maisha yapasavyo kuwa-huru kabisa."***

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Ukirejelea hadithi, thibitisha kuwa mmoja wa wahusika hawa hakuishi maisha ya awali inavyopasa. (alama 16)

***25. Fafanua maudhui ya umaskini yanavyojitokeza katika hadithi Tumbo Lisiloshiba na Tulipokutana Tena. Zingatia hoja nne nne kwa kila hadithi.*** (alama 20)

26.. **"Shogake Dada ana Ndevu" (Alifa Chokocho)**

***"Halindwi, hujilinda yeye mwenyewe. Hujilinda ndani sikwambii nje."***

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

(b) Onesha tamathali mbili za usemi kwenye dondoo. (alama 2)
(ch) Fafanua sifa saba za anayerejelewa katika kauli hii. (alama 14)

**27.** ***Kwa kurejelea hadithi zozote tatu katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine, jadili vile waandishi walivyoshughulikia suala la mapuuza katika jamii.*** **(alama 20)**

**28. "Mtihani wa Maisha" (Eunice Kimaliro)**

***"ilmuradi mawazo yanamwadhibu sasa. "***

(b) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(c) Fafanua sifa sita za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)

(d) Taja mambo mbalimbali yanayochangia adhabu ya mrejelewa wa dondoo hili. (alama 10)

**29..*****Kwa kurejelea hadithi zozote tatu katika Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine, onesha vile waandishi walivyotumia mbinu ya taswira. (alama 20)***

**30.** ***"Kauli yake ni kama maji ya moto yasiyoweza kuchoma nyumba."***

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

b) Taja na ueleze umuhimu wa tamathali moja ya usemi iliyotumika katika dondoo. (Alama 2)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]

c) Fafanua sifa za wapuuzaji wa kauli iliyotolewa. (Alama 8)

d) Jadili dhima sita za mrejelewa katika dondoo. (Alama 6)

Call/sms/Whatsapp Mr.Mosomi @0748842695 for the marking schemes[answers]